

10 JUNI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Arobaini na Sita - Tarehe 10 Juni, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 367

Mafunzo ya Wajasiriamali Wanawake – Mbeya

MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. CYNTHIA H. NGOYE) aliuliza:-

Wanawake wa Mkoa wa Mbeya wameitikia wito wa kuanzishwa kwa vikundi vya uzalishaji mali ikiwemo uanzishwaji wa vyombo vya akiba na mikopo:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia mafunzo ya ujasiriamali Wanawake wa Mkoa Mbeya?

(b) Je, Serikali iko tayari kuhamasisha benki mbalimbali kusogeza huduma karibu na wananchi ili kukidhi azma yao ya kupatiwa mikopo na kujiwekea akiba?

10 JUNI, 2013

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA,
URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (*NEEC*) ilifanya utafiti katika mkoa wa Mbeya na kubaini kuwa wananchi wengi wakiwemo wanawake wameanzisha vikundi vya uzalishaji mali ikiwemo uanzishwaji wa vikundi na mikopo.

Kutokana na juhudi hizo, Baraza kwa kutumia Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi Kiuchumi yaani "*Mwananchi Empowerment Fund*" imeanza kutoa udhamini wa mikopo kwa wananchi wa Mbeya hususan *Chimala SACCOS*.

Aidha, utaratibu na mpango wa kutoa mafunzo umeandaliwa na mafunzo yatatolewa mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2013/2014. Mafunzo hayo yatawahusisha pia wanaume kwa vile *SACCOS* ya Chimala ina wanachama ambao ni wanaume. Mafunzo ya aina hii yameishatolewa katika mikoa ya Dodoma, Ruvuma, Tanga, Manyara, Rukwa na Dar es Salaam. Hivyo, awamu inayofuata mafunzo yatatolewa katika mikoa mingine ukiwemo Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na inaendelea kuhamasisha benki mbalimbali na Taasisi za fedha kusogeza huduma karibu na Wananchi ili kukidhi azma yao ya kupatiwa mikopo na kujiwekea akiba.

Hata hivyo, benki na taasisi za fedha hufikia uamuzi wa kufungua matawi baada ya kufanya utafiti na kubaini uwepo wa wateja wa kutosha katika eneo husika. Changamoto inayowakabili wakopaji wadogo katika taasisi hizo ni riba kubwa inayotozwa kutokana na *risk* zinazoambatana na mikopo inayotolewa.

10 JUNI, 2013

Serikali itaendelea kuzihamasisha benki na taasisi za fedha kupunguza riba na masharti mengine ya mikopo ili wananchi wengi zaidi wenye mitaji midogo waweze kunufaika na fursa hiyo na kujiongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwahamasisha wananchi wa mkoa wa Mbeya pamoja na mikoa mingine kuendeleza jitihada za kujiunga na vyama vya akiba na mikopo (*SACCOS*), *VICOBA* na vikundi vingine vya uzalishaji mali, ili waweze kukopa kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Mara kwa mara Serikali inakiri kwamba riba za benki ni kubwa sana, lakini pia wakati wote imekuwa inasema itazungumza na benki ili hizo riba zipungue. Ni lini sasa watanzania na hasa wale maskini wataelezwa kwamba, riba za benki hizi zimepungua ili waweze kufaidika na mikopo hiyo.

Swali la pili, Waziri anasema ni taasisi moja tu ya *SACCOS* kule Mbeya, Chimala, ambayo imepewa udhamini na *Mwananchi Empowerment*. Ni taasisi ngapi za wakopeshaji ambazo zinastahili kukopeshwa; *VICOBA* na *SACCOS*, katika mkoa wa Mbeya na nchi kwa ujumla ambazo zinafaidika na utaratibu huu wa *Mwananchi Empowerment*, ili wengi zaidi waweze kufaidika na mikopo hii?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imekuwa inafanya mazungumzo na jitihada mbalimbali za kuimarisha uchumi ambao pengine ndiyo unge-*reflect* kupunguza riba kwa mikopo inayotolewa kwa wananchi.

10 JUNI, 2013

Hata hivyo, ninachosema ni kwamba, kama Serikali hatuna uwezo na nguvu ya kupunguza kwa nguvu, ni lazima tufanye mazungumzo na kwa kufuata utaratibu na sheria za nchi zilizopo za nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jitihada hizo zitaendelea lakini siwezi kusema ni lini zitapungua. Wote tungependa zipungue, lakini nafikiri tunaendelea vizuri, sasa hivi benki zimekuwa nyingi, ushindani ni mkubwa na hivyo riba imeanza kupungua. Serikali itaendelea kuongeza nguvu ili angalau riba hizi zipungue kabisa, lakini pia na mkakati wa jumla wa kuimarisha uchumi wetu wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Chimala imepata udhamini, lakini uwezo wa mfuko huu ni mdogo sana hivyo hauwezi kutoa udhamini sehemu nyingi. Chimala ilianza siku nyingi na ndiyo iliyochaguliwa katika mkoa wa Mbeya kupewa udhamini, na pia waliomba. Nafikiri jambo la kwanza ni lazima kuwepo na vikundi vinavyojitokeza kuomba, halafu mfuko huu wa *Mwananchi Empowerment* unachagua kulingana na sifa za waombaji. Uwezo nao ni mdogo, lakini mwaka huu tumemaliza katika mikoa hiyo niliyoisema na tunaingia Mbeya.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nimkumbushe Mheshimiwa Weston Zambi, kwamba katika mikoa ambayo imenufaika sana na mifuko ya taasisi mbalimbali ni pamoja na Mbeya. Itakumbukwa katika miaka mitano mingine iliyopita kuanzia mwaka 2005 tulikuwa na programu moja inaitwa *Rural Financing Support Programme* ambayo ilikuwa pale makao makuu Mbeya. Ilifanya kazi Mbeya, Iringa na mikoa mingine miwili. Kazi kubwa imefanywa kuelimishwa *SACCOS* na kutoa uwezo na mitaji katika mkoa wa Mbeya.

Programme hii sasa imefungwa na imekuja *MIVAF* na yenyewe itatoa *programs* kama hizi katika nchi nzima. Mbeya ndiyo champion waliokuwa wanatekeleza mradi mmoja pekee wa Benki Kata. Benki Kata ni *programme* iliyobuniwa na Mbeya, ikatekelezwa vizuri na ilikuwa ya mfano.

10 JUNI, 2013

Lengo letu tulikuwa tunafikiri kwamba hizi benki kata baadaye zingeweza kuunganika na kuanzisha benki yao kamili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkoa wa Mbeya pamoja na kwamba, Mzee Godfrey Zambi anaomba tutoe *support* zaidi, Serikali imekuwa inatoa *support* sana katika programs mbalimbali hasa hii ya *Rural Financing Support Programme* ambayo imekaa Mbeya pale kama makao makuu na imefanya kazi kwa zaidi ya miaka kumi.

SPIKA: Naomba mjibu maswali kifupi na nyie mnaouliza mwulize kifupi la sivyoo swali moja litachukua dakika kumi (10).

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, amekiri kuna awamu ya pili ya mafunzo inayokuja kwa wajasiriamali na ameutaja mkoa wa Mbeya kuwa ni mmojawapo, naomba kujua kama mkoa wa Singida umo. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nadhani jibu kama upo au haupo, basi, hakuna habari zingine.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa sasa naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mbeya nina uhakika nayo, mikoa inayofuata sina uhakika nayo. Hata hivyo, baada ya Bunge ninaweza nikamsaidia Mheshimiwa Mbunge kujua ni mikoa gani mingine kwa sababu nilikuwa nime- *concentrate* kwa muliza swali.

Mheshimiwa Spika, pia tujue kwamba, mwaka huu kwa mara ya kwanza tumepitisha fedha za bajeti hapa kwa ajili ya Mfuko wa Vijana, Mfuko wa Wanawake ambao ulikuwa hautengewi fedha, tumetenga fedha mwaka huu.

10 JUNI, 2013

Kwa hiyo, pamoja na huu mfuko tunaosema wa *empowerment* unaojikusisha zaidi katika kutoa elimu na dhamana, mwaka huu tujue halmashauri zetu zitaendeleza kwa kasi sana zoezi la ukopeshaji katika vikundi vya vijana na wanawake kutokana na fedha ambazo zimetengwa mwaka huu.

SPIKA: Waziri amejibu kwa kirefu na tumetumia dakika 10 katika hilo swali moja. Sasa twende kwenye swali linalofuata, Mheshimiwa Dustan Kitandula.

Na. 368

Utekelezaji wa ahadi za Rais Wilaya ya Mkinga

MHE. DUSTAN L. KITANDULA aliluliza:-

Wakati wa ziara yake Wilayani Mkinga, Mheshimiwa Rais aliahidi kujengwa haraka hospitali ya Wilaya ya Mkinga. Kutokana na kukipandisha hadhi kituo cha afya cha Maramba ili kitoe huduma za hospitali ikiwemo upasuaji:-

(a) Je, ni hatua gani zimekwishachukuliwa hadi sasa katika utekelezaji wa ahadi hizo?

(b) Je, ni lini utekelezaji wa ahadi hizo za Rais utakamilika?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dustan L. Kitandula, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mwaka 2010 Mheshimiwa Rais alipotembelea wakazi wa Mkinga aliahidi kupandisha hadhi kituo cha afya cha Maramba ili kiweze kutoa huduma za dharura. Pia aliahidi kuharakisha ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Mkinga.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi hizo Serikali imetumia jumla ya shilingi milioni 132.1 kuboresha miundombinu ya kituo cha afya cha Maramba ili kiweze kupandishwa hadhi na kutoa huduma zinazokaribia huduma za hospitali.

Kazi zilizofanyika ni pamoja na upanuzi wa eneo la kituo hicho kwa kuhamisha makazi ya watu wanne (4) na kuwalipa fidia, kufanya ukarabati wa chumba cha upasuaji, kuweka upya mfumo wa umeme na maji taka, kununua kontena kwa ajili ya kutengeneza chumba cha mapokezi, kununua mashine ya dawa ya usingizi na mashine ya kufua nguo.

Aidha, Serikali kwa mwaka 2011/2012 imenunua gari la wagonjwa, Toyota Hardtop lenye usajili Na. SM 8991 na kuongeza idadi ya watumishi hadi kufikia 35.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Mkinga, Serikali imekwishatoa shilingi milioni 221.4 ambapo shilingi milioni 21 zimeishatumika. Ujenzi huu ambao upo katika hatua ya msingi umesimama kutokana na mkandarasi kutoroka. Halmashauri imefungua kesi mahakamani na imeomba mahakama itoe kibali maalum ili ujenzi uweze kuendelea wakati kesi ikiwa inaendelea. Kwa mwaka 2013/2014 Serikali imeidhinisha shilingi milioni 16.2 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa kituo cha afya cha Maramba kinatoa huduma zote muhimu isipokuwa upasuaji kwa wajawazito. Chumba cha upasuaji kipo katika hatua ya mwisho ya ujenzi na kinatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Julai, 2013. Chumba hicho kikikamilika wataalam wa afya watakwenda kukagua na wakiridhika Serikali itatoa kibali cha kupandishwa hadhi kwa kituo hicho.

MHE. DUSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo kimsingi hayaniridhishi, naomba kuuliza maswali mawili ya yongeza.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipotoa ahadi ile, alifanya hivyo kwa kuelewa kwamba eneo lile la mji mdogo wa Maramba lina watu wengi, karibu watu 30,000. Mheshimiwa Waziri anayo habari kwamba, watu wa Tanzania Building Agency walipofanya utafiti walisema ili theatre ile ikamilike zinahitajila milioni 300 na kwamba, leo hii ni sehemu ndogo ya chumba kidogo tu ambapo hata hicho chumba kidogo hakijafanyiwa ukarabati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kutokana na ukubwa wa tatizo katika eneo lile, hao wataalamu walioopo pale tuna madaktari watatu tu, registered nurse mmoja, nurse midwives watano tu. Je, Waziri yuko tayari kuja kutembelea kituo kile cha Maramba ili ajionee hali halisi na ikiwezekana waongeze wahudumu haraka iwezekanavyo?

SPIKA: Ahsante sana. Naomba muulize maswali kwa kifupi, la sivyo tutakuwa na swali moja na jibu moja.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Spika, kwanza *theatre* huhitaji gharama ya shilingi milioni 300 au zaidi kutegemeana na *design* ambayo mtu anataka kujenga. Hata hivyo, cha msingi ni kwamba jengo hilo la *theatre* liko katika hatua za mwisho kukamilika. Serikali imenunua mashine ya ganzi ya kutolea dawa ya usingizi, vitanda vya kufanyia upasuaji, taa za kufanyia upasuaji, seti zote za kufanyia upasuaji, *schizerian set*, *laboratory set* na nyinginezo zote zipo pale tayari. Kuna waganga; *AMOs* wako watatu ambao pia wanaweza wakawa na uwezo wa kufanya hizo operations kwa ajili ya akina mama, *clinical officers* watano na vilevile manesi wako tisa.

Pia katika mgao wa watumishi wilaya ya Mkinga imepata watumishi wapya 12 wapya. Jana tu nilizungumza na mganga mkuu wa wilaya, alikuwa ananiambia wako *AMOs* sita (6). Pamoja na madaktari ambao wataongezwa, kuna *MDs* wawili. Naamini wakati tunaendelea kujenga hospitali ya wilaya, kituo hiki cha afya kitaweza kufanya kazi mara tu baada ya ujenzi kukamilika na kukabidhiwa.

10 JUNI, 2013

SPIKA: Swali la kwamba utakwenda.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Spika, ombi la kwenda kutembelea. Naweza nikasema tu nipo tayari kwenda kutembelea na utaratibu ni kuangalia namna ambavyo tunaweza kuzunguka nchi kwa sababu, nikisema nitaenda kutembelea haina maaana kwamba nitaenda kesho. Kwa hiyo, anaweza kunivumilia, pale tutakapokuwa tumepata fursa basi nitaenda kupatembelea.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Wilaya yetu ya Misenyi ni sawa na nadhani na wilaya iliyopita ambayo Mheshimiwa Waziri alikuwa akiiongelea. Wilaya yetu ina zaidi ya miaka minane tangu imekuwepo, lakini hatujapata hospitali ya wilaya na mpaka leo tunatumia *DDH* ya Mgana ambayo wakati mwingine inaweza kufanya vitu kulingana na utaratibu wa kanisa ulivyopangwa.

Je, lini Misenyi tutapatiwa hospitali ya Wilaya?

SPIKA: Swali jipya kabisa hilo, na wewe mwenyewe unaliona ni jipya kabisa. Mheshimiwa Waziri ukipenda jibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Spika, kila Wilaya pale ambapo hatuna hospitali ya Serikali na kukawa na hospitali ya Misheni au hata ya mtu binafsi, tumekubali na tumekuwa na utaratibu huo wa kufanya makubaliano kati ya halmashauri na hospitali husika ili iweze kuingizwa katika mpango mahsusi wa Serikali kuweza kulipia baadhi ya gharama ili wananchi katika eneo hilo husika waweze kupata huduma. Hizo hospitali ndizo zinazoitwa *DDH*.

Sasa kama kwenye wilaya husika ipo hospitali ambayo ni *DDH*, Serikali inagharamia kulipia watumishi, kupeleka dawa, vitendeakazi pamoja na vifaa vya maabara.

10 JUNI, 2013

Kwa hiyo, katika utaratibu huo ni matumaini yetu kuwa wananchi watakuwa wanaendelea kupata huduma pale, pale ambapo huduma hizo haziridhishi au haziwafikii watu wengi, wilaya haikatazwi kufikiria kuweza kutenga eneo kwa ajili ya kuanza mchakato wa kujenga hospitali ya Serikali. Hata hivyo, pale ambapo hospitali hiyo inaendelea kuhudumia na watu wengi wanaweza kulifikia hilo eneo, hakuna ulazima wa kuwa na hospitali nyingine.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, swali la msingi linahusu ahadi za Rais, na kwa kuwa kwa muda mrefu hapa Bungeni Wabunge wengi hasa wa CCM wamekuwa wakilalamika kwamba ahadi nyingi zinakuwa hazitekelezwi, na majibu yamekuwa kwamba, Ilani ile ya uchaguzi ni miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, hata kile kipindi cha kwanza kuna ahadi ambazo hazikutekelezwa. Sasa swali langu, je, hatuoni kuna sababu muhimu ya kuhakikisha kwamba, Marais wanaotoa ahadi na kumaliza kipindi chao bila ahadi zile kutekelezwa wanapelekwa mahakamani? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Susan Lyimo, swali la nyongeza ambalo lipo nje kabisa ya mfumo wa swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais na Marais wote wamekuwa wakitoa ahadi kwa namna mbalimbali, lakini kwanza ahadi ya msingi ni Ilani, lakini pia zipo ahadi ambazo binadamu yeyote akifika mahali hata yeye huwa ana ahadi kwa watoto wake vilevile. Ukifika mahali unajikuta lazima utoe ahadi, na kwa kadri ya uwezo Serikali ya CCM imekuwa inajitahidi kutekeleza hizo ahadi. Na Rais akishatoa ahadi haiwi rahisi kuwa ahadi ya Rais inakuwa ahadi ya nchi.

10 JUNI, 2013

Kwa hiyo, itatekelezwa kwa fedha za Serikali siyo fedha za Rais, kwamba ahadi za Kikwete siyo kwamba atatekeleza yeye Serikali ndiyo itatekeleza. Na Serikali inatekeleza kwa bajeti na kwa uwezo wa nchi na siyo vinginevyo.

Kwa hiyo, kama Serikali imeweza kutekeleza itatekeleza kama imeshindwa kutekeleza itatoa maelezo na Serikali ni endelevu, Rais huyu anapomaliza siyo kwamba anamaliza anaondoka na nchi yake, nchi inabaki.

Kwa hiyo, atakayekuja atakuja kutekeleza zile ahadi kwa sababu zinabaki kwenye rekodi kama ahadi za Serikali siyo ahadi za Rais kwa mtu kwa jina. Kwa hiyo, hakuna mtu wa kushtakiwa hapa kwa sababu nchi inaendelea na Marais wataendelea kuwepo. (*Makofi*)

SPIKA: Jamani, sawa naomba msihutubiane mimi ninaona tabu kabisa hapa mkihutubiana. Naomba muwe *brief* jamani.

Na. 369

Kupunguza Msongamano Katika Magereza

MHE. LETICIA M. NYERERE aliuliza:-

Magereza ya Mkoa wa Mwanza yana msongamano mkubwa na wa kutisha kwa mfano, Gereza Ngudu linahifadhi mahabusu na wafungwa wanaozidi 160 badala ya 60, hali hiyo huchangiwa pia na ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi za mauaji ambazo huchukua muda mrefu.

Je, Serikali itarekebisha lini jambo hili la msongamano katika magereza yetu hasa Gereza Ngudu ili kuepuka ukiukwaji wa haki za binadamu?

10 JUNI, 2013

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua matatizo ya msongamano wa wafungwa katika magereza nchini kote likiwemo Gereza Ngudu. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Jeshi la Magereza kupitia Bajeti inayotolewa na Serikali imekuwa ikiyatatua matatizo haya kwa awamu kwa kufanyia ukarabati magereza yaliyopo, kukamilisha na kujenga magereza mapya katika Wilaya ambazo hazina Magereza. Lengo ni kuongeza nafasi za kuhifadhi wafungwa Magerezani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi za mauaji ambazo huchukua muda mrefu, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imeshachukua hatua za kuunda Kikosi Kazi (*Task Force*) chini ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini, kazi kubwa kwa kikozi hiki ni kushughulikia tatizo la msongamano Magerezani kwa kubainisha vyanzo na sababu za msongamano huo na kutoa mapendekezo yake kwa Serikali juu ya hatua za kuchukua. Serikali itashirikiana na Kikozi Kazi hicho na kutoa ushirikiano wa kufanya marekebisho yanayostahili kukabiliana na tatizo la msongamano Magerezani nchini kote likiwemo Gereza Ngudu.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba msomganano Magerezani utapunguzwa na ongezeko la Magereza hii ni sawa na mtu anakuuliza watu wengi Tanzania wanakufa kwa malaria ukamwambia kwamba tunayo makaburi mengi ya kutosha kuwazika.

10 JUNI, 2013

Naomba swali langu la kwanza atueleze mbali na ongezeko la magereza ambalo ni kuchochea uhalifu, kuna utaratibu gani au kuna njia gani ya kupunguza ongezeko la mahabusu au kupunguza msongamano magerezani?

Mheshimiwa Spika, la pili, hivi karibuni nilitembelea magereza nchini likiwemo gereza la Ngudu nilibaini kwamba kuna mahabusu wanawake ambao wanajifungulia gerezani na uendelea kukaa gerezani na watoto wao. Jambo ambalo hupelekea watoto hao kuunganishwa na watuhumiwa jambo ambalo ni kinyume cha haki za binadamu. Ninaomba sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atoe kauli leo ni jinsi gani wataachana na dhana hizi za kuwaunganisha watoto na watuhumiwa jambo ambalo ni ukiukwaji wa haki za binadamu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, awali ni kwamba kimsingi Serikali hahitaji magereza na siku zote inasema kwamba ni vyema wananchi waachane na matatizo ya kihalifu ambayo yanaweza kupelekea wao kupelekwa magerezani. Wanaowapeleka magerezani watu au wananchi ni jamii ambayo inasema kutenda hili ni kosa na ukihukumiwa ufanywe vile.

Lakini Serikali siku zote ina programu ya kuhakikisha kwamba uhalifu unapungua na watu ambao wanaenda magerezani wanabaki wachache iwezekanavyo ni gharama. Kuongeza gereza ni gharama kuwalisha na ni gharama kuwatunza. Kwa hiyo, jambo muhimu kwa wananchi ni kuhakikisha kwamba wanatii sheria zilizopo ambazo sisi Wabunge ndiyo tunao zitunga.

La pili, kuhusu watoto na wajawazito. Gerezani mara nyingi wanakwenda watuhumiwa na si kwamba watuhumiwa ambao wanakuwa wajawazito wanaweza wasifanye uhalifu au wananchi ambao ni wajawazito wanaweza wasifanye uhalifu. Sasa kuwapeleka Magerezani wajawazito ni jambo ambalo wakati mwingine haliepukiki.

10 JUNI, 2013

Hata hivyo, fursa ya mtoto anayezaliwa gerezani ipo ya kuwa aondolewe kwenye gereza kama familia ya mtuhumiwa inaweza ikawa tayari kumtunza mtoto. Pamoja na hivyo, Serikali inalifanyia kazi suala la kuwa na magereza kwa ajili ya watoto ili matatizo haya yasichanganywe na matatizo ya watu ambao ni wahalifu watukutu.

MHHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, suala la mlundikano wa wafungwa magerezani ni kubwa hasa ukiangalia pia katika gereza la Ukonga; na kwa kuwa, kuna utaratibu ule wa kuweza kuwafunga wengi kwa kutumia kifungo cha nje jambo ambalo lingeweza likasaidia sana kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani.

Je, Serikali inasemaje kuhusu suala nzima la kushauri Mahakama ili iweze kutumia kifungo hicho cha kuwafunga wafungwa walio wengi nje ili kupunguza msongamano huo magerezani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nilivyosema kwamba tumeunda Kikosi Kazi moja katika kazi zake ni kuishauri Serikali vipi tunaweza kwa sheria zilizopo au tutakazorekebisha kuhakikisha kwamba tunatoa vifungo au adhabu ya kufungwa nje wananchi wengi kutokana na si tu tatizo la msongamano, lakini pia kuwafunga wananchi kifungo cha nje kuwasaidia kwanza, kuacha familia zisisambaratike, lakini pia kupunguza gharama za chakula na usimamizi wa wafungwa magerezani.

Kwa hiyo, Serikali ina sheria hiyo na imeishaunda *Task Force*, lengo ni kuhakikisha kwamba hao wahalifu wengi ambao wanahukumikiwa wanabaki kwenye jamii na wanarekebisha huko kuliko ndani ya magereza.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maji, maana tumeuliza maswali matatu tu mpaka nusu saa.

10 JUNI, 2013

Na. 370

**Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya
Usambazaji Maji Mlandizi**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO (K.n.y. MHE. ABUU
HAMOUD JUMAA)** aliuliza:-

Mwaka 2010 Kampuni ya China ilipewa jukumu la kuboresha miundombinu ya usambazaji maji katika Mji Mdogo wa Mlandizi na baada ya mradi kukamilika *DAWASCO Ruvu* iliweka utaratibu wa kutoa huduma hiyo lakini utekelezaji huo haukufanikiwa kutokana na malipo ya huduma ya maji yaliyolipwa na wananchi kwa Meneja wa *DAWASCO Ruvu* kutoingizwa kwenye akaunti ya *DAWASCO* hali liyomfanya Mkurugenzi kumfukuza kazi Meneja *DAWASCO* na fedha za wananchi kupotea.

(a) Je, Serikali itawasaidiaje wananchi wa Mlandizi kupata haki yao?

(b) Je, kwa nini kunatokea mgao wa maji mara kwa mara usio wa lazima wakati maji yanayotoka Ruvu Juu kwenda Dar es Salaam yanapita Mlandizi ambao ndiyo wenye jukumu la kulinda chanzo hicho cha maji?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya Septemba, 2011 na Machi, 2012 wananchi kadhaa wa Mlandizi walifanya malipo ya ankara za maji kwa wafanyakazi wa *DAWASCO* na fedha zao kutokuingizwa kwenye akaunti ya *DAWASCO*.

Suala hili lilipelekea wananchi hao kukatiwa huduma ya maji pamoja na wafanyakazi wanne (4) wa kituo cha *DAWASCO* Mlandizi kuachishwa kazi. Hata hivyo,

10 JUNI, 2013

DAWASCO iliwarudishia huduma wananchi 185 waliokumba na kadhia hiyo na kuwataka walipie ankara za kila mwezi kuanzia kila mojawapo aliporejeshewa huduma.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi walioachishwa kazi walifungua kesi katika Tume ya Usuluhishi na Upatanishi (*CMA*) wakipinga kuhusika kwao na adhabu waliopewa. Hivyo, Serikali inawaomba wananchi walioathirika kusubiri maamuzi ya kesi hiyo ili kupata hatma ya fedha zao pamoja na madeni waliyokuwa wameyalimbikiza.

(b) Mgao wa maji katika maeneo yanayohudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu unatokana na uwezo mdogo wa uzalishaji maji katika mtambo huo ambao haulingani na mahitaji halisi ya maji kwa sasa. Kwa hali hiyo, maji machache yaliyopo hugawanywa kwa zamu katika maeneo yanayohudumiwa na mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Katika juhudi za kuondoa taitzo hilo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mardi wa maji wa Ruvu juu utakaoongeza uzalishaji wa maji kutoka lita za ujazo milioni 82 kwa siku za sasa hadi lita milioni 196 kwa siku ifikapo mwezi Juni, 2015. Ongezeko hilo la maji litamaliza tatizo la mgao wa maji unaoendelea ikiwa ni pamoja na kufikisha maji kwenye mabomba ambayo hayatoi maji kwa sasa. Ikiwa ni pamoja na yanayoitwa mabomba ya mchina.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante, na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Je, sasa kwa sababu wananchi hawa wanaonekana wapo *very innocent*. Serikali ipo tayari kwenda kufanya mkutano kwa wananchi hawa na kuwaeleza juu ya hali hii ili wasiendeleo kuleta kero kwa Mheshimiwa Mbunge na katika Serikali ya Wilaya?

La pili, kwa vile imekwishazungumza na Mheshimiwa Waziri wa Maji mara nyingi juu ya tatizo la maji katika Mji wa Mbinga. Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kuwasaidia wananchi wa Mbinga kuwapelekea fedha ili waweze kuleta mabomba mengi zaidi na kuleta maji katika Mji wa Mbinga?

10 JUNI, 2013

SPIKA: Haya Mheshimiwa Waziri ujibu, nasikia mmezungumza.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Abuu Jumaa kwa kufuatilia kwa makini sana jambo hili katika ofisi zetu Dar es Salaam, katika ofisi zetu hapa na kuuliza maswali hapa Bungeni. Napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba tupo tayari kufanya mkutano na wananchi wa Mlandizi ili kuwaelezea tatizo hili na kumaliza kadhia ambayo inawakabili.

Mheshimiwa Spika, pili, ninatambua na kumshukuru sana Mheshimiwa Kayombo kwa kazi kubwa anayofanya kuhimiza utekelezaji wa miradi ya maji katika eneo la Mbinga na tupo tayari kuendelea kushirikiana katika kutekeleza miradi hiyo.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na jitihada za Waziri amesema atakwenda kukutana na wananchi ili kutatua tatizo hilo. Lakini bado kuna tatizo la upatikanaji wa maji na mwenyewe katika majibu yake ya msingi amekiri kwamba kuna uhaba wa maji katika mto Ruvu.

Je, huoni kwamba hawatendewi haki wananchi wanazunguka mto Ruvu kwa kukosa huduma ya maji na kupeleka Dar es Salaam pamoja na kwamba maji hayo ni machache?

Je, yupo tayari kusema ni lini atawahakikishia wananchi hawa wanapata maji ili waweze kuendelea maendeleo yao?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wanaozunguka bomba kuu Ruvu Juu wanayapata maji hayo kwa mgao, na bomba hili linatoa maji katika maeneo ya Kibaha Vijijini pamoja na Jiji Dare es Salaam.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, maji yanatolewa sasa kama tulivyoeleza katika swali la msingi hayatoshelezi mahitaji ya sasa ya eneo lote ambalo linahitaji maji hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuzingatia kwamba wananchi wa wanaoishi karibu na Ruvu ndiyo wanaolinda bomba hilo, wananchi hao katika maeneo ya Mlandizi na Kibaha Mjini wanapata maji mara tatu kwa wiki ukilinganisha na wale wa Dar es Salaam ambao wanapata maji mara mbili kwa wiki. Jawabu la suala hili ni jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 182 za sasa na kufikia milioni 196 mwezi Juni, 2015. *(Makofi)*

Na. 371

Ahadi ya Ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea – Mtwara

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliluliza:-

Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, iliahidi kujenga Kiwanda kipya cha mbolea Mkoani Mtwara pamoja na kuboresha mbolea zinazozalishwa na kiwanda cha Minjingu, Arusha ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa mbolea nchini.

Je, hatua hizi zimefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara na Shirika la Maendeleo ya Taifa (*NDC*) imeendelea na juhudi za kuanzisha viwanda vya kemikali na mbolea kwa kutumia gesi asili ya Mtwara.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutekeleza llani ya Uchguzi ya CCM ya kujenga kiwanda kipya cha mbolea Mkoani Mtwara, Makampuni matatu (3) *Deepak Fertilizer and Petrochemical Ltd* ya India; *TATA Chemicals Ltd* ya India na *Polyserve group Ltd* ya Misri), kati ya kampuni 10 yaliyojitokeza yalichaguliwa katika awamu ya kwanza ili baadaye yachujwe kupata mwekezaji mahiri. Mchakato huu bado unaendelea ili kumpata mwekezaji mahiri.

Aidha, Kampuni ya *Paradeep phosphate Ltd* kutoka India, vilevile imekwishaleta maombi mwezi Aprili, 2013 ya kuwekeza katika ulizaishaji wa mbolea huko Kanda ya Kusini. Kiwanda hicho kinatarajia kuzalisha tani 750,000 kwa mwaka, kitagharimu dola bilioni 1.5 na kitaajiri watu 3,000 kitakapokamilika. Kampuni ya Ujerumani iitwayo *Ferrostal*, pia imeonyesha nia ya kujenga kiwanda cha mbolea Kusini mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tayari upembuzi yakinifu na uchimbaji wa visima zaidi vya gesi vimefanyika ili kupata umeme wa *MW 300* na kuunganisha katika *grid* ya Taifa pamoja na malighafi ya kutosha ya kuzalisha mbolea aina ya Urea na kemikali ya *Methanol* kwa matumizi ya viwanda vipya vinavyotarajiwa kujengwa.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu mkubwa wa mbolea nchini, kampuni ya Minjingu *Mines and Fertilizer Ltd (MMFL)* inayozalisha mbolea aina ya Minjingu *Rock Phosphate (MRP)*, imefanya upanuzi (*expansion*) na sasa kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani 100,000 za *MRP* kwa mwaka, ikilinganishwa na tani 75,000 za awali. Minjingu wana mpango wa kupanua uwezo wa uzalishaji hadi kufikia tani 600,000 kwa mwaka.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo

10 JUNI, 2013

ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, swali langu limesema je, hatua hizi zimefikia wapi *timeframe*?

Mheshimiwa Spika, lakini tumeanza suala hili kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, leo 2010/2015 bado tupo kwenye upembuzi yakinifu, lini viwanda vya mbolea vitajengwa katika nchi hii ili wananchi wapate mbolea ya kutosha? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa sababu wananchi walio wengi hasa wakulima wa Mbozi, Mbeya na Watanzania walio wengi ambao wanaotumia mbolea ya Minjingu walishakosa imani kwa mbolea hiyo kwa sababu hai-*perform* vizuri kwa mbolea hii kwenye uzalishaji hasa wa mahindi, Serikali inachukua hatua gani kuwarudishia wananchi imani kwamba mbolea ile inaweza ikafaa sasa kwa kilimo?

SPIKA: Mheshimiwa hata Waziri wa Kilimo unaweza kujibu.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, naomba niongezee majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kama alivyojibu katika majibu ya msingi hayo Makampuni matatu ambayo sasa yamekidhi vigezo kati ya kumi hiyo yenyewe ni hatua, kwa sababu Makampuni yanavyokuja huwezi ukayalazimisha sasa nenda yaanze kujenga.

Kimsingi Serikali hatujengi viwanda ni Makampuni ndiyo yanaona kwamba sasa tunaweza tukajenga viwanda na baadhi ya Makampuni hayo mimi mwenyewe nimeongea nayo wengine wanazo *conditions* wanataka mpaka wahakikishiwe ni kiasi gani cha gesi watapewa kabla hawajawekeza kwenye viwanda hivi.

Kwa hiyo, hizi ndizo baadhi ya changamoto ambazo

10 JUNI, 2013

Serikali inaendelea nazo ili zikamilike.

Kuhusu hii mbolea ya Minjingu *Local Phosphate* mimi nafikiri tumeeleza mara nyingi kwamba tayari kiwanda kile kimefanya maboresho kwa kuongeza virutubisho kwenye ile mbolea ya Minjingu *Local Phosphate* sasa hivi haiitwi hivyo tena inaitwa Minjingu Mazao baada ya kuongezewa virutubisho na mwaka jana imefanya kazi vizuri sana.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, kazi ya Serikali ni kubaini matatizo ya wananchi na kutafuta suluhu ya matatizo haya na katika tatizo la msingi si kuendelea kutegemea watu binafsi ndio watatue matatizo ya wananchi.

Je, ni lini Serikali itaona katika suala hili la mbolea kuna umuhimu wa kufanya maamuzi ya haraka kupitia mpango wa PPP kujenga viwanda vya mbolea na kuondoa tatizo hili sugu kwa wakulima?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nadhani Wabunge kama mnavyosema ni kwamba Serikali imeshaamua na sio mambo ya kukisia wala sio mambo ya kuomba wawekezaji. Kuna Kampuni zaidi ya sita ambazo zimeonyesha nia ya kujenga viwanda vya mbolea na wala sio hizi Kampuni ndogondogo za wachuuzi tunaongelea hapa.

Kwa hiyo, napenda kuwahakikishia Watanzania kwamba viwanda vya mbolea vitajengwa na Makampuni ambayo mengine yana viwanda zaidi ya mia moja duniani. Kwa hiyo, cha maana hapa endeeleni kuwahimiza watu wa Mtwara wakubali kwamba ile gesi inaweza kujenga viwanda vya mbolea. Ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea, leo umesaidiwa Naibu Waziri wa

10 JUNI, 2013

Viwanda na Biashara.

Na. 372

Kuzuiwa Kwa Uvuvi - Pori la Muyowosi

MHE. FELIX F. MKOSAMALI aliuliza:-

Wananchi wamezuliwa kufanya shughuli za uvuvi kwenye mabwawa yaliyoko kwenye pori la Muyowosi-Wilayani Kibondo:-

(a) Je, Serikali itaanza lini kutoa vibali ili wananchi waendeleo na shughuli zao za uvuvi, ajira ambayo waliitegemea sana?

(b) Kwa kuwa, Afisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya naye ameshindwa kazi zake hivyo ameomba wananchi wapewe vibali waendeleo na uvuvi kwani Samaki hao wakibaki bila kuvuliwa watakwenda wapi na kwa faida ya nani?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

(a) Rasimu ya Mpango Kamambe (GMP) wa Pori la Akiba la Muyowosi hauna shughuli za uvuvi pia Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori ya Na. 5 ya Mwaka 2009 hairuhusu shughuli za uvuvi ndani ya Pori la Akiba.

Sheria ya zamani iliruhusu kutoa vibali kwa wananchi kufanya shughuli za uvuvi ndani ya Pori la Muyowosi ambayo ilileta mgongano wa matumizi katike eneo moja, ambalo shughuli ya Uwindaji wa Kitalii pia inafanyika kwenye eneo hilo hilo, kwa kuwa uwindaji hutumia risasi za moto, hivyo endapo wawindaji watawinda katika eneo ambalo wapo watu wengine wanaopitapita, kuna hatari ya kusababisha

vifo au kujeruhi.

Mheshimiwa Spika, Upande wa Mto Malagarasi ambao ni mpaka wa Pori la Akiba Muyowosi, shughuli za uvuvi zinaruhusiwa hivyo wananchi wanaruhusiwa kwenda kuvua kwenye maeneo hayo kwa kuwa yapo kwenye ikolojia hiyo. Aina za samaki wanaopatikana ndani ya Pori hilo pia wanapatikana katika Mto Malagarasi.

(b) Mheshimiwa Spika, ningependa kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mfumo wa ikolojia kwa asili unajiimarisha wenyewe kwa kutumia viumbe hao hupata chakula chake kwa kutegemeana (*Prey-Predator System*). Hivyo ni dhahiri samaki wasiovuliwa wanatumika kuimarisha ikolojia ya bwawa katika pori, kwa kuliwa na mamba na ndege pamoja na wanyamapori wengine walao samaki.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza baadhi ya maeneo yenye uhifadhi shughuli za uvuvi zinafanyika watu wanachunga ng'ombe wanatozwa fedha na wafanyakazi wa Wizara hii. Kwa nini Wizara hii inawazuia wananchi wa Kibondo kufanya shughuli za uvuvi wakati maeneo mengine kama Tabora wanafanya uvuvi na shughuli zingine, hiyo moja.

Swali la pili, kwenye ilani ya CCM ya mwaka 2010 CCM mliahidi kwamba mtahakikisha wananchi ambao wanazunguka maeneo ya hifadhi wanakwenda kufanya shughuli zao ndogondogo za kiuchumi, ikiwemo Kibondo na Kasulu. Kwa nini mliwadanganya wananchi mwaka 2010 na mnaendelea kuwazuia na mmejipanga vipi kuwadanganya mwaka 2015?

SPIKA: Hayo maneno mengine hayana tija naomba majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa mujibu wa sheria ambayo imewekwa hapa Bungeni na kwa mujibu wa matakwa ya Serikali

10 JUNI, 2013

kutekeleza sheria ambazo zinapitishwa na Bunge hili mapori yote ya Akiba ikiwa ni pamoja na hili eneo la Muyowosi hairuhusiwi kufanya shughuli za uvuvi ndani ya mapori hayo na mtu yoyote ambaye ataonekana atathibitika tutamkamata akifanya hiyo kazi, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tutamkamata tutamchukulia hatua za kisheria.

La pili, ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ndiyo inayoongoza Serikali na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mkosamali Serikali imejikita katika kutekeleza ilani hii na moja ya mambo ambayo tumejiweka kutekeleza ilani ni kuhakikisha kwamba uhifadhi na maeneo yote yaliyohifadhiwa ambayo ni takribani asilimia 25 ya ardhi yote ya Tanzania yatabaki kuwa mikononi mwa wananchi yatahifadhiwa kwa maslahi ya kizazi hiki na vizazi vijavyo na tutahakikisha kwamba uhifadhi huu tunaulinda na tunauendeleza na wananchi wanaendelea kunufaika. *(Makofi)*

Na. 373

Bidhaa Zinazozalishwa Nchini Kuwa Ghali

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS aliuliza:-

Mkakati wa Serikali ni kuhimiza uwekezaji wa ndani na nje ya nchi katika Sekta ya Viwanda ili kupunguza mfumko wa bei wa bidhaa husika kama Saruji na kadhalika:-

Je, ni kwa nini bidhaa zinazozalishwa nchini bado ni ghali kuliko zinazoagizwa nje?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ughali wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani unatokana na ukweli kwamba

10 JUNI, 2013

viwanda vyetu hapa nchini kwa kiwango kikubwa hutegemea malighafi na ujuzi muhimu kutoka nje ya nchi kama vile mitambo, vipuri, mafuta, vilainishi, teknolojia na wataalamu. Pamoja na gharama za ununuzi wa malighafi, teknolojia na utaalumu, kuna gharama za usafirishaji ambazo pia huongeza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, bei ndogo ya bidhaa za nje mara nyingi husababishwa na ruzuku zinazotolewa kwa Viwanda hivyo katika nchi zao ili kukuza viwanda vya mauzo ya nje (*Export Industries*) na kuvijengea uwezo viwanda hivyo kwa kuwapa vivutio vya kuwafanya wazalishe na kuuza nje, kutengeneza ajira kwa wananchi wao na kuinua pato la nchi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi fulani, bei ndogo ya bidhaa za nje wakati mwingine zinazotokana na uaminifu mdogo wa wafanyabiashara ambao huagiza bidhaa zisizo na ubora na kuziua kwa bei nafuu ukilinganisha na bidhaa za ndani. Aidha, kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao huagiza bidhaa kwa njia za udanganyifu kama vile kukwepa kodi na ushuru na hatimaye kuuza bidhaa hizo kwa bei ndogo.

Mheshimiwa Spika, sababu zingine zinazochangia bidhaa za ndani kuwa za ghali ni bei kubwa ya umeme hapa nchini, gharama kubwa za usafirishaji wa bidhaa kutoka viwandani kwenda sokoni zinazotokana na miundombinu duni na kupanda mara kwa mara kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Pia, kuporomoka kwa thamani ya shilingi kwa nyakati tofauti huchangia kuongeza gharama za uzalishaji wa bidhaa katika viwanda vyetu. Aidha, kuwepo kwa viwanda vichache hapa nchini kunasababisha gharama za uzalishaji kuwa za juu kwa sababu hakuna mazingira ya wazalishaji katika eneo moja au wa aina moja kunufaika kupitia miundombinu iliyopo hususan bidhaa za umma (*public goods*), kuuziana malighafi za kati (*intermediate inputs*) na

10 JUNI, 2013

matokeo ya mafanikio kati ya kiwanda na kiwanda (*externalities*). (Makofi)

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo hayana matumaini nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kabla ya kuulizwa suala moja la nyongeza kwamba saruji inayozalishwa Dar es Salaam inauzwa palepale Dar es Salaam shilingi 15,000/= kwa pakiti moja ya kilo 50. Wakati saruji inayozalishwa katika Kiwanda cha Rasilemu *United Emirates* inauzwa kwa dilhamu 12 ambayo ni sawa sawa na shilingi 5,400/= tu za Tanzania. Je, Serikali inawaambia nini Watanzania sasa waendeleo tu kuumia kwa kutegemea bidhaa za ndani ambazo ni ghali sana au itaondoa vikwazo vya uagizaji bidhaa muhimu za nje ya nchi kama saruji, mabati, na sukari ili wananchi wapate nafuu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri umemuelewa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa pamoja na bidhaa kama hii saruji ambayo inazalishwa Dar es Salaam na inauzwa palepale pia ni ghali ukilinganisha na zile zinazotoka nje sababu nilizozitoa katika majibu yangu ya msingi ni kuwa bidhaa nyingine za nje zinakuja na ruzuku kutoka kwenye nchi zao na kwa hali hiyo kushusha bei zake kwa sababu haionyeshi hali halisi ya gharama iliyoingia katika kutengeneza bidhaa zile. Lakini vilevile gharama za malighafi zinavyoagizwa toka nje zinazolingizwa katika uzalishaji wa bidhaa kama saruji vilevile inachangia katika kuifanya saruji pamoja na kuwa imekuwa imetengenezwa Tanzania kuwa ghali zaidi. Serikali sasa hivi ina mikakati kwanza kusimamia uwingizwaji wa bidhaa ambazo zinakuja na ruzuku ambayo inaonyesha kabisa kuwa haionyeshi hali halisi kwa kuitoa ushuru unaostahiki.

Juzi tumepitisha Bajeti ya Wizara ya Fedha tukaonyesha jinsi ambavyo kuanzia sasa tutasimamia zaidi bidhaa zinazolingizwa ndani ya nchi kuhakikisha kama kweli

10 JUNI, 2013

zinalipia ushuru unaostahiki ili tufidie na sisi zile gharama ambazo wao wanakuja kutulundikia sisi. Kwa hiyo, nafikiri hiyo itasaidia katika kuonyesha kuwa Serikali sasa hivi tuko macho. *(Makofi)*

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, chanzo kizuri sana cha kodi ni Serikali kushirikiana na sekta binafsi yaani *(Public Private Partnership)* kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao hasa katika maeneo yenye uzalishaji mwingi wa mazao hayo. Kama kiwanda kikianzishwa itapatikana *corporate tax, payee, skill development levy* na kadhalika. Serikali iko tayari kuanzisha viwanda hivyo kwa mwaka huu wa fedha vingapi?

SPIKA: Betty hili linafanana kweli na lile swali la bei? Yaani jipya kabisa halifanani na la bei kabisa *not only that* viwanda, Mmm !!!! hebu jibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuhusisha sekta binafsi katika uzalishaji na ndiyo maana Serikali imejitoa kabisa katika masuala ya biashara. Lakini Serikali vilevile imeshatayarisha sera na sheria ya *PPP* ambayo itatumika sasa kuhakikisha kuwa sekta binafsi na Serikali wanaingia ubia wa kufanya biashara au viwanda katika kuzalisha bidhaa mbalimbali nchini. Siwezi kusema kwa uhakika viwanda vingapi lakini tayari tuna miradi ambayo itaingia katika mfumo huu wa *PPP* na ambayo tayari imeanza kufanyiwa kazi na ninaamini hii itakuwa ni chachu ya kuhakikisha kuwa kuanzia sasa sekta binafsi na Serikali inafanya miradi mingi zaidi. *(Makofi)*

Na. 374

Kuongeza Bajeti ya Afya

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuongeza Bajeti ya Afya ili ifikie Azimio la Abuja la asilimia 15?

10 JUNI, 2013

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mbunge za Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa Azimio la Abuja ambalo linataka Bajeti ya Afya ifikie asilimia 15 ili iweze kuboresha Sekta ya Afya Nchini. Ni kwell kwamba, Bajeti ya Afya haijafikia asilimia 15 kwa mujibu wa Azimio la Abuja. Hii ni kutokana na ufinyu wa mapato, lakini hata hivyo, Bajeti ya Afya imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka ili kufikia lengo la kutenga Bajeti ya Afya kufikia asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Sekta ya Afya inajumuisha Bajeti ya Afya katika Mikoa na Halmashauri ambapo Bajeti zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Bajeti ya Sekta ya Afya imefikia asilimia 10, mwaka 2011/2012 Sekta ya Afya ilikuwa na Bajeti ya shilingi bilioni 1,209 ambazo ni sawa na asilimia 10 ya bajeti yote ya Serikali baada ya kutoa *Consolidated Fund Services (CFS)* na mwaka huu wa fedha, Sekta ya Afya imetengewa shilingi bilioni 1,288 ambayo vilevile ni sawa na asilimia 10 ya Bajeti yote ya Serikali ukiondoa *Consolidated Fund Services (CFS)*. Serikali itaendelea kuongeza Bajeti ya Afya kadiri mapato yake yatakavyokuwa yakiimarika.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nitauliza maswali mawili ya nyongeza, la kwanza mfumo wa afya ili ukamilike unahitaji rasilimali fedha, rasilimaliwatu pamoja na miundombinu kwa maana ya majengo. Tanzania tumewekeza zaidi kwenye miundombinu, lakini hali ilivyo mpaka sasa rasilimali fedha na rasilimaliwatu hazitoshi. Ni vipi tutaweza kuendeleza mfumo huu bila kuweka uwekezaji wa makusudi wa fedha za kutosha kwenye Bajeti ya afya?

Swali la pili, ni lini Serikali itatengeneza *formula* mpya

10 JUNI, 2013

ya kutoa *differential incentives* ambazo zitaweweza watumishi kwenye sekta ya afya wanaofanya kazi pembezoni wapewe posho maalum za kufanya kazi katika mazingira magumu ili waweze kuwa na motisha ya kufanya kazi watoe huduma bora zaidi kwa wananchi?

SPIKA: Kuna swali atajibu Waziri wa Fedha nyingine atajibu *Part Two* atajibu Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Spika, ni kweli mfumo wa afya ili ukamilike unahitaji miundombinu pamoja na rasilimali watu na rasilimali fedha. Kuhusiana na hilo suala la kuongeza rasilimali fedha ningependa tu kulihakikishia Bunge lako na Mheshimiwa Mbunge aliyeliza swali kuwa kwa sasa hivi iko mikakati ambayo sisi wenyewe kama Serikali tunaweza tukaifanyia kazi hususan kusimamia vizuri zaidi mapato yanayoingia katika sekta hii. Lakini vilevile itambuliwe kuwa kuna mapato mengi yanayoingia katika mfumo huu kwenye sekta hii ya afya ambayo haupitii moja kwa moja Serikalini.

Pengine itabidi ifikie mahali sasa na sisi tusimamie zaidi hata hizo fedha zinazolingia kwenda moja kwa moja kwenye sekta hii bila ya kupitia Serikalini ili tuone kama hizo nazo pia zinafanya ile kazi muhimu ambayo inahitajika. Suala lingine ambalo nafikiri Serikali inaweza kulisimamia vizuri zaidi ni kuhakikisha kuwa kila mwananchi wa Tanzania anaingia katika mfumo wa Bima ya Afya. Hii itakuwa ni njia rahisi na nzuri zaidi kuhakikisha kuwa kila mwananchi anayehitaji kuhudumiwa kiafya anapata huduma hiyo hata kama hana fedha mfukoni na hii ningependa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge sheria zitakapoletwa hapa kubadilisha Sheria ya Afya kuhusiana na masuala ya Bima ya Afya basi tukubaliane wote kuwa hii iwe ni wajibu wa kila Mtanzania kuwa mwanachama wa Mfuko huu wa Bima ya Afya.

Hii ndiyo njia moja rahisi ninayoiona itakayotuhakikishia kuwa rasilimali fedha ya kuhudumia sekta hii inapatikana kwa urahisi zaidi.

10 JUNI, 2013

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshapitia na kuainisha maeneo ya mazingira magumu na imo katika mchakato wa kuainisha posho maalum katika yale maeneo ambayo yatakuwa yanaitwa yenye mazingira magumu. Pale itakapokuwa tayari nafikiri itatangazwa na yale maeneo watumishi watakaokuwa kule itakuwa ni watumishi wote, sio wa Waziri ya Afya peke yake, itahusisha watumishi wote wanaofanya kazi kule wakiwemo Walimu na watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la rasilimali watu, moja katika changamoto ya Wizara ya Afya ni suala hili ambalo Mheshimiwa Dkt. Kigwangala yeye alikuwa Mjumbe katika Kamati ya Huduma za Jamii analifahamu vizuri kwamba tumekuwa na mkakati mahsusi kabisa wa kuboresha eneo hili kwa kuongeza udahili wa wanafunzi ambao wanaingia vyuoni kutoka wanafunzi 3,000 ambao walikuwa wakiingia miaka minne, mitano iliyopita hadi sasa wanaingia wanafunzi takribani 8,000 na kusudio ni kufikia wanafunzi 10,000 pale itakapokuwa inafika mwaka 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwenye eneo hili tutaweza kupunguza tatizo la uwepo wa watumishi ingawa tukumbuke ongezeko la Watanzania kila mwaka ni milioni moja, pamoja na ongezeko hili la watumishi lakini tutachukua muda mrefu ili kuweza kukidhi na kupunguza tatizo hili moja kwa moja.

Na. 375

Biashara kwa Wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

MHE. GOSBERT B. BLANDES aliuza:-

Jumuiya ya Afrika Mashariki ilishipitisha mkataba wa kuruhusu biashara kwa wananchi wa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo bila vikwazo vyovyote lakini wananchi wengi hawajafahamishwa juu ya fursa hiyo.

10 JUNI, 2013

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa umma wa Watanzania juu ya fursa hiyo?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imetekeleza yafuatayo ikiwa ni hatua ya kutoa elimu kwa umma wa Watanzania juu ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na fursa zilizopo:-

- (i) Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi vya luinga na redio katika vituo vya televisheni vya *TBC1, ZBC, Star TV* na *SIBUKA* pamoja na redio za *TBC, SIBUKA FM* na *Redio Free Afrika*. Vituo vingine vitaongezwa.
- (ii) Wizara imeanzisha utaratibu wa utoaji wa elimu kwa pamoja na mipakani (*joint border sensitization*) kwa kushirikiana na nchi wanachama. Wizara imekwishafanya ziara hizi katika mipaka ya Mtukula, Murongo, Kabanga Mkoani Kagera, Namanga Mkoani Arusha, Holili Mkoani Kilimanjaro na Sirari Mkoani Mara, Shimoni kule Mombasa na Kaskazini Pemba.
- (iii) Wizara inaendelea na majadiliano na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Wizara ya Viwanda na Biaashara ili kuwezesha uhuishaji wa masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mipango na bajeti za

Halmashauri na hivyo kuwezesha suala la elimu kwa umma kutolewa katika ngazi ya Halmashauri. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa maafisa viungo ambao tunawaita *focal person's* kutoka katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa inayojumuisha Mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga na Mara na katika Kanda ya Kaskazini Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Maafisa viungo hawa watasaidia sana Wizara kutoa elimu ya Jumuiya juu ya mambo ya Afrika Mashariki katika Halmashauri zao.

- (iv) Wizara imeendelea kufanya semina kwa makundi mbalimbali katika jamii kama vile wanazuoni, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wafanyabiashara, viongozi na watendaji mbalimbali pamoja na waandishi wa habari. Kutokana na semina ambazo Wizara imefanya kwa Waheshimiwa Wabunge, Wizara inawaomba Waheshimiwa Wabunge wanapokwenda kwa wapigakura wao waendeleo vilevile kutoa elimu kwa umma juu ya Mtangamano wa Afrika Mashariki kwani suala hili sio la Wizara pekee bali ni la Taifa kwa ujumla.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

- (i) Kwa kuwa kuna nyaraka muhimu ambazo zinatakiwa wananchi wawenazo katika kupeleka bidhaa zao nje ya nchi na kwa kuwa nyaraka hizi zinapatikana katika Makao Makuu ya Mikoa, kwa hiyo wananchi

hulazimika kusafiri umbali mrefu sana zaidi ya kilometa 200. Je, ni kwa nini Serikali isipeleke nyaraka hizi katika Makao Makuu ya Kata au ikiwezekana Makao Makuu ya Vijiji?

(ii) Kwa kuwa kuna malalamiko mengi sana ya wafanyabiashara hasa kucheleweshewa mizigo yao kuvuka kutoka kwenye nchi yetu kwenda nchi zingine za Afrika Mashariki, nilitaka nijue je, Serikali inalifahamu tatizo hili la kucheleweshewa mizigo yao kwenda nchi zingine na kama inalijua ni hatua gani za haraka na za makusudi ambazo inakusudia kuchukua?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, nyaraka za uhalisia kutoka katika Mikoa na zinatolewa na *TCCIA*, kwa kweli hili ni swali zuri na ni swali ambalo tunalichukua kwa ajili ya kutoa mapendekezo kama inatawezekana basi kuundwe muundo wa pamoja wa kuweza kuhusisha hawa maafisa viongo walau kwa ngazi ya Halmashauri waweze kutoa hizi huduma za kutoa nyaraka za uasilia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Blandes nakushukuru sana kwa hili, wazo lako ni zuri na sisi tutakaa pamoja na Wizara ya Biashara na Viwanda ili hawa maafisa wa *TCCIA* waweze kushirikiana na Halmashauri pamoja na hawa maafisa viungo wetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hili jambo sisi tulilibaini wakati tunafanya ziara zetu za mipakani na tumechukua hatua tatu ambazo ni muhimu sana; ya nne inabidi Bunge pia nalo lihusike. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuweka mkataba maalum katika Halmashauri au Wilaya zile mbili za mpakani, mpaka wa nchi jirani na mpaka wa kwetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili vilevile kuna utaratibu wa kutengeneza *One Stop Border Post* ambapo hivi ni vituo maalum vya mpakani vinavyoweza kurahisisha kabisa huduma zote kwa pamoja ikiwa ni pamoja na mambo ya afya, huduma za mazao, huduma za uhamiaji na ukazi, zinafanywa kwa pamoja, kwa hiyo hii itasaidia wafanyabiashara wawe wanapita kwa urahisi zaidi.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu kabisa tulibaini na hili ningependa sana nilizungumze hapa na naomba unipe nafasi, tulipokuwa tunakwenda katika ile mipaka tuligundua kwamba kuna Sheria ambazo zipo na watendaji wanasema hizi Sheria kama hazijahaulishwa basi sisi tutaendelea kufanya hivihivi. Kwa hiyo, ni jambo la mahusiano juu ya Sheria za Afrika Mashariki na Sheria za ndani. Kwa hiyo, Wizara yetu tayari imeshapitisha taratibu za kuhaulisha zile Sheria katika Wizara za kisekta, zikija hapa Waheshimiwa Wabunge naomba msaidie kuzi-*amend* ili ziwe zinawiana na zile za Afrika Mashariki.

SPIKA: Muda wa maswali umekwisha. Tunao wageni wetu na ni wale ambao walikuja kushirikiana na Wabunge Wanawake kwenye mafunzo waliyokuwa nayo jana na juzi. Kwa hiyo, ni Mheshimiwa Baroness Armstrong, *Member of the House of Lords*, kuna Mheshimiwa Baroness Thornton, yeye ni *Opposition Spokesperson for Equalities Office, also is a Member of the House of Lords*, tuna Mrs Tracey Jessup, yeye ni *Deputy Principal Clerk Assistant*, tunaye Mrs Hellen Haywood, *Deputy Director CPA-UK Branch*. *Thank you very much, we shall be meeting in the afternoon at my office, your welcome. (Makofi)*

Kuna wanafunzi 12 na Walimu wao kutoka shule ya viziwi ya Mugeza-Bukoba, wasimame. Tumefurahi kuwaona na siku nyingine mje kututembelea. *(Makofi)*

Pia wapo Madiwani 18 na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Erick Ambakisye. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi H. Chana, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 10, watakuwa na mkutano katika ukumbi namba 231.

10 JUNI, 2013

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Iddi Azzan, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge matokeo ya michezo ya mpira wa miguu na mpira wa pete iliyochezwa siku ya Jumamosi tarehe 8 Juni, 2013 katika ya *Bunge Sports Club* na timu ya *Uhuru Publisher* kama ifuatavyo:-

Mpira wa miguu (*football*), Bunge ilifunga magori mawili, *Uhuru Publisher* goli moja. Mpira wa pete (*netball*), timu ya Waheshimiwa Wabunge ambayo ni mabingwa wa Kombe la Mabunge ya Afrika Mashariki iliibugiza bila huruma timu ya *Uhuru Publisher* magoli 30 kwa 18. Nyota wa mchezo wa mpira wa pete alikuwa ni Mheshimiwa Rachel Mashishanga na nyota wa mchezo wa mpira wa miguu alikuwa ni Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa. Hongereni sana, hawa ndio nyota. Safari hii mchezaji wetu wa kawaida hakuwepo? Tunashukuru kupata wachezaji nyota wengine, hongereni sana. (*Makofi*)

Halafu ofisi inawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kutakuwa na maonyesho ya taasisi mbalimbali kwenye viwanja vya maonyesho vya Bunge. Maonyesho haya yameandaliwa na *EAG Group Ltd* na yatahusu taasisi za fedha, taasisi za *insurance*, taasisi za vyuo vikuu, taasisi za mawasiliano na taasisi za mafuta. Maonyesho haya yanaanza leo na yataendelea mpaka kesho. Kwa hiyo, mnaweza kwenda kuona na mkajifunza yaliyoko kule kwa faida yenu na faida ya wananchi. Karibuni sana.

Tunaendelea, Katibu!

MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2013 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment Bill, 2013)*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BILL SUPPLEMENT

No. 2

11th January, 2013

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 2
Vol. 94 dated 11th January, 2013*

Printed by the Government Printer Dar es Salaam by Order
of Government

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT,
2013

ARRANGEMENT OF SECTIONS

PART 1

PRELIMINARY PROVISIONS

Sections Title

1. Short title.
2. Amendment of Certain Written Laws.

PART II

AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT
(ELECTIONS) ACT

(CAP. 292)

3. Construction.
4. Amendment of section 114.

PART III

10 JUNI, 2013

AMENDMENT OF THE LAW REFORM COMMISSION ACT
(CAP. 171)

5. Construction.
6. Amendment of section 5.
7. Amendment of section 18.
8. Addition of section 24A.

PART IV

AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE ACT,
(CAP. 298)

9. Construction.
10. Amendment of section 6.
11. Amendment of section 14.
12. Addition of section 29A.

10 JUNI, 2013

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
10th January, 2013
Cabinet

OMBENI Y. SEFUE
Secretary to the

A BILL

for

An Act to amend certain Written laws.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title **1.** This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2013.

Amend- **2.** The Written Laws specified in various Parts of this Act
ment of are amended in the manner specified in their respective
certain Parts.
Written Laws

10 JUNI, 2013

PART II
AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT
(ELECTIONS) ACT,
(CAP. 292)

3. This Part shall be read as one with the Local Government (Elections) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Constru-
ction
Cap. 292

4. The principal Act is amended in section 114 by adding immediately after sub-section (3) the following new sub-section:

Amend-
ment
of section
114

"(4) Where an election petition is unlikely to be determined within eighteen months, the Minister responsible for legal affairs may, after consultation with the Chief Justice and by notice published in the *Gazette*, extend the prescribed time for further period not exceeding six months as he may determine."

PART III
AMENDMENT OF THE LAW REFORM COMMISSION ACT,
(CAP. 171)

5. This Part shall be read as one with the Law Reform Commission Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Constru-
ction
Cap. 171

6. The principal Act is amended in section 5(1), by deleting the word "six" and substituting for it the word "nine".

Amend-
ment of
section 5

7. The principal Act is amended in section 18, by deleting the word "Secretary" and substituting for it the words "Executive Secretary".

Amend-
ment of
section 18

Addition of new section 24A

8. The principal Act is amended by adding immediately after section 24 the following new section:

“Prohibition regarding Commission’s documents

24A. A person shall not use, disclose or publish any information or document of the Commission without an approval of the Commission.”

PART IV

AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE ACT,
(CAP.298)

Construction

9. This Part shall be read as one with the Public Service Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of section 6

10. The principal Act is amended in section 6(1), by adding immediately after paragraph (b) the following new paragraph:

“(c) oversee and ensure career development of employees in their respective organization.”

Amendment of section 14

11. The principal Act is amended in section 14, by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

“(2) The Secretary shall be the Chief Executive and accounting officer of the Commission and shall attend meetings of the Commission but shall not vote at such meetings:

Provided that, the Secretary shall not attend Commission’s meeting deliberating on the disciplinary referrals of an employee of the Commission.”

Addition of new section 29A

12. The principal Act is amended by adding immediately after section 29, the following new section:

“Delegation of functions and powers

29A. The Secretary may, by Notice published in the *Gazette*, delegate to any Chief Executive Officer the functions and powers of

10 JUNI, 2013

the Secretariat to conduct recruitment process in the Service.”

OBJECTS AND REASONS

The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2013 proposes amendment of the Laws specified in Part II to Part IV with a view to remove the shortfalls experienced in the course of administration and implementation of those laws.

The Bill is divided into Four Parts.

Part I of the Bill contains the preliminary provisions including the name of the proposed Act as well as the manner in which the laws amended by the Bill are to be construed.

Part II proposes amendment to the Local Government (Elections) Act, Cap. 292 by adding in section 114, a new subsection (4) that empowers the Minister responsible for legal affairs to grant an extension of time for a period not exceeding six months where an election petition is unlikely to be determined within eighteen months.

Part III of the Bill proposes amendment to the Law Reform Commission Act, Cap. 171. In this Part, clause 6 proposes amendment to section 5(1) by deleting the word “six” and substituting for it the word “nine” so as to increase the size of the Commission. In addition, clause 7 proposes amendment to section 18 by deleting the word “Secretary” and substituting for it the words “Executive Secretary” so as to conform to the current structure of the Commission approved in 2007. Again, Clause 8 proposes the addition of new section 24A that prohibits any person to use, publish or disclose any information or document of the Commission without the approval of the Commission.

Part IV of the Bill proposes amendment of the Public Service Act, Cap 298. In this Part, clause 11 of the Bill proposes amendment to section 14 of the Act by deleting sub-section (2) and substitute for it the new subsection (2) that designates the Secretary as the Chief Executive Officer of the Commission. In addition, the Secretary is empowered to attend the meetings of the Commission with the exception of meetings convened to deliberate the disciplinary referrals of employees of the Commission. Moreover, clause 12 of the Bill proposes the addition of new section 29A that empowers the Secretary to the Commission to delegate to any Chief Executive Officer the functions and powers of the Secretariat to conduct recruitment process in the Service.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2013 unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria zilizoainishwa katika Sehemu ya II hadi Sehemu ya IV kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa usimamizi na utekelezaji wa Sheria hizo.

Muswada umegawanyika katika Sehemu kuu Nne.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yakiwemo jina la Sheria inayopendekezwa pamoja na namna ambavyo masharti mbalimbali yaliyo katika Sheria inayopendekezwa yatatafsiriwa.

Sehemu ya Pili inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kwa kuongeza kifungu kwenye kifungu cha 114 cha Sheria hiyo, kifungu kidogo cha (4) kinachotoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Sheria baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kuongeza muda wa kusikilizwa kwa kesi za uchaguzi kwa kipindi kisichozidi miezi sita pale

10 JUNI, 2013

ambapo inaonekana dhahiri kwamba muda wa kawaida hautatosheleza kumaliza kesi hizo.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Tume ya Kurekebu Sheria Sura ya 171. Katika sehemu hii, ibara ya 6 inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 5(1) cha Sheria kwa kuondoa neno "six" na kuweka badala yake neno "nine" iliyoongeza idadi ya Wajumbe wa Tume. Aidha, Ibara ya 7 inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 18 cha sheria hiyo kwa kuondoa neno "Secretary" na kuweka badala yake maneno "Executive Secretary". Lengo kuu la marekebisho hayo ni kwenda sambamba na muundo mpya wa Tume uliopitishwa mwaka 2007. Vile vile, ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 24A ambacho kinazuia mtu yeyote kutumia kwa namna yoyote kuchapisha au kutoa taarifa au nyaraka yoyote ya Tume bila idhini ya Tume.

Sehemu ya Nne inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298. Katika Sehemu hii, ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 14 cha Sheria kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kipya cha (2) ambacho kinaelekeza kwamba Katibu atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Tume. Aidha, Katibu amepewa mamlaka ya kuhudhuria vikao vyote vya Tume isipokuwa vikao vyote vinavyoshughulikia rufaa za kinidhamu za watumishi wa Tume. Ibara ya 12 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 29A kinachotoa mamlaka kwa Katibu kukasimu kwa Afisa Mtendaji Mkuu yeyote, mamlaka na majukumu ya Sekretarieti ya Ajira ya kuendesha mchakato wa kuajiri watumishi.

Dar es Salaam
9 Januari, 2013

FREDERICK M. WEREMA,
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, katika kipindi cha bajeti tangu mlivyoanza mlikuwa mmeshajaza fomu kuomba uchangiaji. Kwa hiyo, hamkuwa na sababu ya kuomba wakati Muswada unasomwa. Leo tunarudia utaratibu wa kawaida ambapo wanaotaka kuchangia hii *Bill* wataomba kwa kuleta karatasi za maombi. Mheshimiwa Mtoa hoja!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013, naomba kutoa hoja kwamba Muswada uitwao Sheria ya Marekebisho wa Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2013 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments Act, 2013)*, kama ulivyorekebisha kwa mujibu wa jedwali la marekebisho sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako Tukufu liujadili na hatimaye liupitisha kuwa Sheria ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala na kupitia kwake niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ushauri wao na muda waliotumia katika kuboresha Muswada huu. Maoni na Ushauri wa Kamati yamezingatiwa na yamesaidia sana kuuboresha Muswada huu kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa kwenye Bunge lako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pamoja na jedwali la marekebisho, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria tatu kwa lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa matumizi ya sheria hizo, kuongeza masharti mapya katika sheria hizo na kufanya masahihisho ya kiuandishi na lugha ili kuondoa ukinzani wa tafsiri ya baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuleta utekelezaji madhubuti wa Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazolengwa ni Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura ya 292 yaani *The Local Government (Elections) Act, Chapter 292*. Pili, ni

Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171 yaani *The Law Reform Commission Act, Chapter 171* na tatu ni Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 yaani *The Public Service Act, Chapter 298*.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa yaani *The Local Government (Elections) Act, 292* Toleo la 2010, tunapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 114, kwa kuongeza kifungu kidogo cha (4) kinachotoa mamlaka kwa Mahakama zinazosikiliza kesi za uchaguzi wa Madiwani kuendelea kusikiliza na kutoa hukumu katika mashauri ambayo hayakumalizika ndani ya kipindi cha miezi 18 kama zitaridhika kwamba kutomaliza kesi hizo kutawanyima haki wahusika katika kesi hizo au kuleta matumizi mabaya ya Mamlaka ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria namba 7 ya mwaka 2010, kifungu hicho kilifanyiwa marekebisho na kuweka ukomo wa muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa Madiwani kuwa ni miezi 18 kama inavyoonyeshwa kwenye kifungu kidogo cha tatu (3) ambacho kinasomeka:-

"The court shall hear and determine each election petition within 18 months from the date of presentation of election petition."

Mheshimiwa Spika, Sheria ilivyo hivi sasa haitoi fursa kwa Mahakama kuendelea kusikiliza na kutoa uamuzi kwa shauri au mashauri ambayo haikuyakamilisha ndani ya muda uliowekwa kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa bajeti ya kuiwezesha kusikiliza mashauri hayo. Dhana ya kuongeza muda wa aina hiyo iliwekwa pia kwenye Sheria ya Taifa ya Uchaguzi yaani *The National Elections Act, Sura ya 343, Toleo la 2010* ambapo Bunge lako Tukufu lilitoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Sheria kuongeza muda usiozidi miezi sita inapoonekana dhahiri kwamba kesi za uchaguzi wa

Wabunge haziwezi kuhitimishwa ndani ya miaka miwili kama ilivyotakiwa na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapendekeza dhana hii ya kuongeza muda wa Mahakama kusikiliza mashauri ya kesi za uchaguzi wa Madiwani iwekwe pia kwenye sheria hii. Hata hivyo, ili kutoa haki kwa wahusika wa kesi ambazo muda wa kusikilizwa kwa kesi hizo umeshapita, tunapendekeza kama inavyoonesha kwenye jedwali la Marekebisho, sheria itoe fursa kwa Mahakama kuendelea kusikiliza kesi za uchaguzi za Madiwani ambazo muda wa kusikilizwa wa miezi 18 umeshakwisha. Hii itatoa nafasi ya wahusika kupata haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yanayohusu Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria (*The Law Reform Commission Act*), Sura ya 171, katika Ibara ya 6 ya Muswada, tunapendekeza marekebisho katika kifungu cha 5(1) ili kuweka ukomo wa Makamishna wa Tume kuwa tisa badala ya sita.

Mheshimiwa Spika, lengo la pendekezo hili ni kuongeza idadi ya Makamishna ili watekeleze majukumu ya Tume kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa na marekebisho yaliyomo kwenye Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.11 ya mwaka 2005, lakini ambayo kwa makosa ilirekebisha kifungu ambacho hakihusiki na yaliyotarajiwa, yaani Kifungu cha 6.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili kwenye Sheria hii ni lile ambalo lipo kwenye Ibara ya 7 ya Muswada, linalopendekeza kubadilisha cheo cha Katibu wa Tume kuwa Katibu Mtendaji kwa kufuta neno '*Secretary*' na badala yake kuweka maneno '*Executive Secretary*'. Marekebisho haya yanalenga kutekeleza Muundo mpya wa Tume uliopitishwa na Ofisi ya Rais, Utumishi mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 8 ya Muswada, tunapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 24A, ambacho kinabeba katazo la matumizi, kuchapisha, kutoa taarifa au nyaraka za Tume bila idhini ya Tume. Lengo

la marekebisho haya ni kuzuia matumizi mabaya na upotoshwaji unaoweza kufanywa na watu au taasisi juu ya taarifa hizo kabla hazijawasilishwa kwenye mamlaka zilizoiagiza Tume kufanya kazi hizo, au kabla ya mamlaka hizo zinazohusika hazijawasilisha taarifa za Tume Bungeni.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanapendekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma (*The Public Service Act*), Sura ya 298, Toleo la 2002. Marekebisho hayo yanahusu mambo yafuatayo:-

(i) Ni kufuta maneno *Director of Local Government Authority* na badala yake kuweka maneno *Local Government Authority* kwenye kifungu cha 6(1).

(ii) Kuongeza jukumu la Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma, kila Katibu Mkuu, Katibu Tawala wa Mkoa na Halmashauri za Serikali za Mitaa kuwa kama inavyopendekezwa kwenye Ibara ya 10 ya Muswada yaani kusimamia na kuhakikisha ustawi wa taaluma kwa watumishi wa taasisi hizo.

(iii) Katika Ibara ya 11 ya Muswada, tunapendekeza kwamba kifungu cha 14(2) kifutwe na kuandikwa upya na kiwekwe kifungu kipya cha 14(3) kama inavyoonesha kwenye sehemu A ya jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, lengo la masharti haya mapya ni kukifanya kifungu hicho kisomeke vizuri na pia kumwezesha Katibu wa Tume kuhudhuria vikao vya Tume bila ya kuwa na haki ya kupiga kura, lakini pia kumzuia asihudhurie kabisa vikao vya Tume vinavyojadili rufaa ya Watumishi wa Tume ambao wapo chini yake, kwa kuwa anahusika na masuala hayo ya rufaa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanazingatia haki ya asili au msingi kwenye utoaji wa haki, misingi ambayo inasema kwamba, mtu anayetoa uamuzi kuhusu haki ya mtu mwingine asiwe na maslahi kwenye jambo linalohusika,

kuepuka upendeleo na kumpa mhusika fursa ya kutoa utetezi wake kwa uhuru na kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ibara ya 12 ya Muswada ikisomeka na Ibara ya 12 ya Jedwali la Marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sehemu ya Sita ya Sheria Mama. Sheria hii isomwe pamoja na kifungu cha 29 kilichowekwa na Sheria Na. 18 ya mwaka 2007 (*The Public Service Amendment Act 2007*). Sheria hiyo, ndiyo iliyotoa mamlaka kwa Waziri kuanzisha Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma (*The Public Service Recruitment Secretariat*).

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Ukiangalia Sheria ya sasa kwenye kichwa kidogo cha habari, tunapendekeza baada ya maneno *special provisions* tuweke kichwa kidogo cha habari kipya "*The Public Service Recruitment Secretariat*" ambacho ndicho kilichokusudiwa kuchukua maudhui ya kifungu cha 29 kilichowekwa na Sheria Na. 18 ya 2007.

(ii) Baada ya kufanya hivyo, tunapendekeza kuvifuta vichwa vidogo vya habari (a), (b) na (c) na kuviandika upya kuwa (b), (c) na (d).

(iii) Kwenye Sheria hiyo pia tunapendekeza kuweka kifungu kipya cha 29A kama inavyoonyeshwa kwenye Ibara ya 13 ya Jedwali la Marekebisho. Marekebisho tunayopendekeza yanalenga kumpatia Katibu wa Tume ridhaa ya kugatua mamlaka yake ya kusimamia mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma, kwenda kwa Mtendaji wa Taasisi ya Umma au Halmashauri na kuweka masharti kwamba mchakato wa ajira uliogatuliwa ufuatae masharti ya Kanuni za Utumishi wa Umma zilizotengenezwa chini ya Sheria hiyo.

(iv) Katika Jedwali la Marekebisho neno Mtendaji Mkuu yaani *Chief Executive Officer*, limepewa tafsiri

10 JUNI, 2013

kwamba linajumuisha Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Umma au Mamlaka yoyote ya ajira.

(v) Neno *Council* limepewa tafsiri inayotumika kwenye Sheria ya Mamlaka za Wilaya au Miji yaani kuwa ni Halmashauri ya Mji au Mamlaka ya Mji. Marekebisho haya yataziwezesha Halmashauri nchini kuajiri kada za chini kama watakavyoomba na kukubaliwa na Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekezwa kufuta rejea ya maneno, *The Written Laws Miscellaneous Amendments Act*, popote yanapojitokeza kwenye Muswada na kuweka badala yake maneno *The written Laws Miscellaneous Amendments No. 2 Act*.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la marekebisho haya ni kutofautisha jina la Sheria hii inayopendekezwa na Sheria ambayo Bunge lako Tukufu liliipitisha mnamo tarehe 8 Februari, 2013 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, 2013*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kupitia kwako kuwaomba Wabunge kuujadili Muswada huu na kuupitisha katika hatua mbili yaani Kusomwa Mara ya Pili na Kusomwa ya Tatu. Nina imani kwamba Bunge lako litaridhia marekebisho yote haya yanayopendekezwa na litakubali marekebisho haya yawe sehemu ya Sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ambayo ilishughulikia Muswada huu. Mheshimiwa Pindi Chana!

MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2013 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, No. 2, 2013*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa taarifa hii, naomba taarifa hii yote iingie kwenye *Hansard*, nami nitasoma kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu kupata fursa ya kutoa maoni kwa niaba ya Kamati yangu. Hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la April, 2013, naomba nichukue fursa hii muhimu ili nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2013 (*The Written Laws Miscellaneous Amendment Act No.2, 2013*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kukabidhiwa Muswada huu, Kamati yangu ilianza kazi ya kushughulikia Muswada huu tarehe 7 Juni 2013, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), Aidha, kama tunavyofahamu utungaji wa Sheria una taratibu zake zenye madhumuni maalum. Kwa upande wa Bunge letu taratibu hizo zinaelezwa vizuri katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013. Miongoni mwa hatua muhimu ni ile iliyoelekezwa katika Kanuni ya 117(9) kuhusu utaratibu wa Kikao cha Kamati inayoshughulikia Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hii, tarehe 8 Juni, 2013, Kamati ilikutana na baadhi ya wadau kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti ya Ajira na Halmashauri za Manispaa na Wilaya. Aidha, Wabunge wengine pia walialikwa na kuhudhuria Vikao vya Kamati kwa ajili ya kutoa maoni yao.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho, Kamati ilipokea maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuhusu maudhui, mantiki, madhumuni na mpangilio wa Muswada. Napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliridhika na maelezo ya Mtoa Hoja, kuhusu sababu za msingi za mapendekezo ya Serikali, kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado kuna mambo ya msingi yaliyobainika na yanayohitaji kufanyiwa kazi zaidi baada ya Bunge kupokea maoni haya.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada. Kazi iliyotakiwa kufanyika wakati wa kuchambua Muswada huu, ni kutoa maoni na ushauri wa Kamati kwa lengo la kuwezesha utungaji wa Sheria bora. Kazi hii haikuwa na namna nyingine ya kuikamilisha pasipo kufanya uchambuzi wa Muswada uliosomwa na Mtoa Hoja. Katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilijikita kwenye mtazamo wa jamii na uchumi ambapo mambo muhimu yaliyozingatiwa kama ifuatavyo:-

(i) Njia inayoweza kutatua tatizo ndani ya Jamii kwa mapendekezo yanayotolewa na Serikali;

(ii) Njia ya kupata namna sahihi ya kurekebisha dosari za kisheria na uendeshaji; na

(iii) Faida na madhara ya kubadilisha au kutobadilishwa kwa Sheria kama inavyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada huu kwa kujielekeza kwenye mambo yafuatayo:-

(i) Kama Sheria inayolengwa kutungwa itajali misingi ya haki;

(ii) Umuhimu wa ufanisi;

(iii) Uzito wa kasoro za kisheria zinazokusudiwa kurekebishwa; na

(iv) Gharama za utekelezaji wa Sheria kabla na baada ya marekebisho yanayopendekezwa kwenye Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, katika tathmini na uchambuzi wa Muswada huu, Kamati ilijuliza maswali yafuatayo:-

(i) Je, Sheria zilivyokuwa kabla ya mapendekezo haya, zilikuwa na ufanisi?

(ii) Je, zilizingatia suala la usawa na haki?

(iii) Je, zilikubalika kijamii?

(iv) Je, zilikuwa na tija kiuendeshaji, kijamii, kisiasa na kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa majadiliano pamoja na ushauri na maoni ya Kamati. Kabla ya kuendelea na majadiliano wakati wa kuchambua Muswada huu, hatua ya kwanza tulipokea maelezo ya jumla ya Mtoa Hoja. Katika hatua hii, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa Muswada uliposomwa kwa Mara ya Kwanza ulikuwa na Ibara 12 tu. Hata hivyo, Mtoa Hoja alipokutana na Kamati aliwasilisha Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendment*) chini ya Kanuni ya 86(10)(b). Jedwali hilo lilibadilisha mambo makubwa manne katika Muswada tunaoujadili.

Mheshimiwa Spika, katika kuwasilisha, Mtoa Hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu unapendekeza kurekebisha Sheria tatu ambazo ni :-

(i) Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura ya 292 (*The Local Government (Elections) Act, Cap. 292*);

- (ii) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171 (*The Law Reform Commission Act, Cap. 171*); na
- (iii) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (*The Public Service Act, Cap. 298*).

Mheshimiwa Spika, Muswada mzima pamoja na mabadiliko yaliyofanywa kwa Jedwali lililowasilishwa kwenye Kamati una jumla ya sehemu nne. Sehemu ya kwanza, ni maelezo ya utangulizi na sehemu ya pili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kwa kuongeza Kifungu kwenye kifungu cha 114 cha Sheria, kinachotoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya Sheria baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kuongeza muda wa kusikilizwa kwa kesi za uchaguzi wa Madiwani kwa kipindi kisichozidi miezi sita, pale ambapo inaonekana dhahiri kwamba muda wa kawaida hautoshelezi kumaliza kesi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji sababu za mapendekezo hayo ya Serikali hususan sababu za kuongezwa muda wa kusikiliza kesi kufanywa na Waziri mwenye dhamana badala ya Jaji Mkuu kwani hii ni mihimili miwili tofauti. Kamati ilielezwa kuwa kwa namna Sheria ilivyo, kuna tatizo la kesi za chaguzi za Madiwani kutomalizika kwa wakati na haki kutotendeka ipasavyo kama hakutakuwa na marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pendekezo la Serikali katika kifungu cha 4 cha Muswada linahusu haki na demokrasia, umakini mkubwa ulihitajika. Wajumbe walihoji kwa kina na ikajitokeza mitazamo ya namna tatu. Wapo walioona kuwa hakuna sababu ya kuongeza muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa Madiwani na kwamba muda uliopangwa kwenye Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa miezi 18 unatosha. Vilevile, yalikuwepo mawazo kuwa badala ya kuongeza, yangeletwa mapendekezo ya kupunguza muda huo na mtazamo wa tatu, ulitaka muda uongezwe kama inavyopendekezwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, kila mtazamo kati ya hiyo, ulikuwa na hoja zake za msingi. Kwa mfano, mtazamo wa kutokuongeza muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa Madiwani ulijengwa kwa misingi kuwa muda unapoongezwa utamnyima haki ya kuongoza Diwani aliyetangazwa kwa vile atatumia muda mrefu kwenye kesi kuliko uwakilishi wa eneo lake. Aidha, wananchi wanaowakilishwa hawatawakilishwa vema na Diwani anayetumia muda mrefu wa madaraka yake kushughulikia kesi ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, sanjari na misingi hiyo, hoja nyingine ilikuwa kwamba, sababu za kuchelewa kusikilizwa kesi hizo hazitokani na Sheria bali ni kutokana na sababu nyingine zikiwemo upungufu wa fedha na rasilimali watu, hivyo utatuzi wake si wa kuirekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kukubalina na mapendekezo ya Serikali ya kuongeza muda wa kusikiliza kesi hizo, Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kwa kurejea Kanuni ya Sheria (*Legal Maxim*) inayoeleza kwamba "Justice delayed is justice denied". Kwa tafsiri tunasema "Haki inayocheleweshwa ni haki inayozuiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia kila kifungu, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Marekebicho ya Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Katika mapendekezo ya kurekebisha Sheria hii Kamati ina maoni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa hali halisi ya mwenendo wa kesi za uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa inaonesha kuhitajika kwa ongezeko la muda wa kusikiliza mashauri hayo na kwa kuwa muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa mwaka 2010 umekamilika na bado kuna kesi nyingi hazijakamilika, vifungu vya 3 na 4 vya Muswada vitawezesha kufanikisha jambo hilo. Aidha, Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria za Uchaguzi wa Mamlaka za

Serikali za Mitaa zinapaswa kulinganishwa na madhumuni ya pendekezo la Ibara ya 3 na Ibara ya 4. Msingi wa maoni haya ya Kamati ni umuhimu wa kuzingatia dhana ya haki kwa upana zaidi katika mashauri ya kesi za uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(ii) Kwa kuwa kifungu cha 137(3) cha Sheria ya Uchaguzi (*The National Elections Act, CAP. 343*), kinamruhusu Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Sheria kuongeza muda usiozidi miezi sita pale inapoonekana dhahiri kwamba kesi za uchaguzi haziwezi kuhitimishwa ndani ya miezi kumi na nane, kuna umuhimu mkubwa kwa Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nayo itoe Mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Sheria kuongeza muda kama inavyopendekezwa katika Muswada tunaogadili.

(iii) Mapendekezo ya Serikali yatawezesha kutekelezwa kwa dhana ya kupeleka madaraka kwa jamii kwa lengo la kusogeza madaraka kwa wananchi na kuboresha utoaji wa huduma. Kamati ina maoni kuwa kupitisha marekebisho haya ni jambo moja na utekelezaji wa Sheria ni jambo lingine. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri kuwa mara baada ya Bunge kupitisha Muswada huu na kusainiwa kuwa Sheria, Serikali iwezeshe utekelezaji wa Sheria ili kuendelea kuheshimu dhana ya utawala wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tume ya kurekebisha Sheria, Sura ya 171 (*Law Reform Commission Act, CAP. 171*). Katika Sheria hii, marekebisho yanayopendekezwa ni ya aina mbili. Kwanza, ni kuondoa neno "six" na kuweka neno "nine" ili wajumbe wa Tume ya Kurekebisha Sheria wawe tisa badala ya sita. Kamati ilihoji mantiki ya mabadiliko hayo na kuelezwa kuwa kuna umuhimu wa kuongeza ukubwa wa Tume na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, chimbuko la pendekezo hilo ni makosa yaliyofanyika mwaka 2005 ambapo Sheria Namba 11 ya mwaka huo, ilirekebishwa kimakosa Kifungu cha 6 cha Sheria Sura ya 171 badala ya Kifungu cha 5(1) kilichokusudiwa. Kamati ina maoni kuwa kasoro yoyote ya kisheria haipaswi kuachwa iendelee. Hivyo, Kamati ilikubaliana na marekebisho hayo.

Mheshimiwa Spika, maelezo yaliyotolewa yanaonesha kuwa kasoro inayorekebishwa kwa kifungu hiki cha Muswada ilidumu kwa takriban miaka tisa. Si jambo jema kuacha kasoro hii kwa muda mrefu kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa yanapatikana katika kifungu cha 18 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria ambapo inapendekezwa kwenye kifungu cha 7 cha Muswada liongezwe neno "*Executive*" na kusomeka "*Executive Secretary*" badala ya neno "*Secretary*" lililopo. Kamati ilihoji mantiki ya kufanya marekebisho hayo na kupewa ufafanuzi kuwa marekebisho yanayopendekezwa ni kutokana na mabadiliko ya kimuundo ambayo yalipitishwa mwaka 2007, yanayomtambua Katibu wa Tume kama Mtendaji Mkuu wa Tume. Baada ya ufafanuzi huo Kamati iliafiki marekebisho hayo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine kwenye Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria ni kuongeza kifungu kipya cha 24A kinachozuia matumizi yasiyofaa ya taarifa za Tume kutumika bila idhini ya Tume kabla ya kuwasilishwa Bungeni. Kamati ilihoji iwapo Sheria nyingine zinazohusu Machapisho kama vile "*Copyright and Neighbouring Rights Act*" hazitoshi kuzuia. Kwa ufafanuzi uliotolewa, Kamati ilibaini kuwa Sheria za Haki Miliki zinahusika na machapisho yaliyosajiliwa na siyo taarifa kama hizi za Tume.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Kama tunavyofahamu msingi wa

kurekebisha Sheria ni kasoro zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wake. Kwa kuzingatia ukweli kuwa kuna kasoro za namna mbili katika utekelezaji wa Sheria ya Tume ya kurekebisha Sheria, Sura ya 171 (*The Law Reform Commission Act, CAP 117*), Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kifungu cha 5 cha Muswada wa Sheria unaojadiliwa kina umuhimu wa kupitishwa na Bunge kama alivyowasilishwa na mtoa hoja. Sababu kubwa ya ushauri huu ni mahitaji ya Sheria yanayohitajika kwa utekelezaji bora ya Sheria ya Tume ya kurekebisha Sheria.

(ii) Kifungu cha 6 kinachopendekeza kuongeza ukubwa wa Tume kimejielekeza kwenye ufanisi wa Tume. Kamati inashauri kuwa pamoja na pendekezo hilo, jambo lingine muhimu ni kuiwezesha Tume hii kifedha na watumishi ili iweze kufikia tija inayokusudiwa. Hakuna ubishi kuwa matokeo ya kazi nzuri ya Tume ya kurekebisha Sheria yana mchango mkubwa kwa Taifa hili. Jambo muhimu ni kuhakikisha kuwa Tume hiyo inapewa rasilimali za kutosha kadiri ya mahitaji na uwezo.

(iii) Kwa kuwa Taarifa za Tume ya kurekebisha Sheria zinapowasilishwa Bungeni huwa wazi kwa namna, haki na sababu ya kuruhusu matumizi ya Taarifa hizo kabla hazijawasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Kamati inaafiki pendekezo linalotolewa na Serikali katika Ibara ya 8 ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwenye pendekezo la kurekebisha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Kamati ilihoji iwapo Sheria zilizopo bila marekebisho zisingetosha kuwezesha ufanisi wa Tume na kuzuia matumizi ya Taarifa zake bila kibali. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliridhika kuwa kuna umuhimu wa kurekebisha Sheria kama inavyopendekezwa. Sababu kubwa ni kuwa Sheria zilizopo zinahusu machapisho yaliyosajiliwa na kwamba Taarifa za Tume ziliwasilishwa mezani zinaweza kutumika kama rejea. Aidha, mapendekezo yanayotolewa yatasaidia kuweka misingi ya Sheria vizuri kwa ajili ya ufanisi wa Tume hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ilivutia mjadala mrefu kama ilivyokuwa kwa sehemu ya tatu. Aidha, Jedwali la Marekebisho limesababisha kuongezeka kwa kifungu kizima katika sehemu hii. Badala ya kuwa na Ibara 4 zinazohusu mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, Muswada umekuwa na Ibara 5.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inahusu Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (*The Public Service Act, CAP. 298*). Katika marekebisho ya Sheria hii Kamati ilizingatia mambo makubwa matatu:-

(i) Umuhimu wa kuwa na mchakato wa ajira wenye tija na unaozingatia mazingira wezeshi bila kuathiri ufanisi.

(ii) Misingi ya haki katika ufuatiliaji wa masuala ya kinidhamu.

(iii) Malalamiko ya Wabunge, watendaji na wananchi katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mapendekezo ya Serikali yanagusa mambo ambayo kiuhalisia yalikuwa yakilalamikiwa kwa muda mrefu, eneo hili pia lilikuwa na mjadala mrefu. Suala la Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ikihusianishwa na mchakato wa ajira katika Halmashauri nchini lilijadiliwa kwa kirefu na kupata maswali mengi yaliyohitaji majibu ya ufafanuzi. Kwa mfano, Kamati ilitaka kujua hali ilivyokuwa katika mchakato wa ajira kwenye Halmashauri kabla ya kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha kama sababu za kuuweka mchakato huo kwenye Tume zimekwisha au laa. Kamati pia ilitaka kupata njia yenye ufanisi na tija zaidi ili Sheria iweze kuwa bora kuliko ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 hadi 13 pamoja na marekebisho yanayofanywa katika Jedwali limezingatia mambo hayo muhimu. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa mchakato wa ajira si jambo la kuachwa bila kudhibitiwa na kusimamiwa ipasavyo. Ni vema Serikali ikahakikisha kuwa mchakato huo unazingatia Sera, Kanuni na misingi ya ajira kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma yalijadiliwa kwa kina. Ibara zinazohusika na marekebisho hayo ni Ibara ya 9 hadi ya 13 baada ya Jedwali la Marekebisho kwa ujumla kuna mambo makini mawili, kuhusu mambo hayo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa Ibara ya 13 ya Muswada pamoja na Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuongeza kifungu kitakachomruhusu Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kukasimu baadhi ya majukumu kwa Watendaji Wakuu wa Halmashauri na Makatibu Wakuu wa Wizara nchini, Kamati ina maoni kuwa pendekezo hili litasaidia kupunguza urasimu katika kuajiri. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ifanye mapitio ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 ili kuendana na marekebisho ya Sheria;

(ii) Kwa kuwa marekebisho haya yatakuwa na ufanisi kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kufika hadi Mikoani kwa mujibu wa Sheria, wakati umefika kwa Serikali kuiwezesha Sekretarieti hiyo kufika ngazi za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mwisho nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wajumbe wa Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala kwa utaalamu wao, kwa michango yao mahiri iliyojaa utaalam na iliyofanikisha Muswada huu kusomwa hapa leo. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Gosbert Bagumisa Blandes, Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir na Mheshimiwa Halima James Mdee.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Fredrick Werema, Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu wake Mheshimiwa Angelah J. Kairuki, pamoja na Naibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa ufafanuzi walioutoa kwenye Kamati. Nawashukuru pia Watumishi wa Bunge wakiongozwa na Dkt. Thomas D. Kashilillah pamoja na wasaidizi wake Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Peter Magati kwa uratibu mzuri ulioiwezesha Kamati kutekeleza jukumu hili ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Sasa nitamwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu. Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAMI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Sheria na Katiba juu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2013 yaani *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2013)*.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali ya 2013 ulichapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 11 Januari, mwaka 2013 na kusomwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Kumi wa Bunge lako tukufu. Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ya Sheria za Tanzania, Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171 ya Sheria za Tanzania pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma yaani Sura ya 298 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Muswada unapendekeza marekebisho ya kifungu cha 114 cha Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (4) kitakachompatia Waziri anayehusika na masuala ya sheria mamlaka ya kuongeza muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa Madiwani kwa kipindi kisichozidi miezi sita. Waziri atafanya hivyo pale itakapoonekana dhahiri kwamba muda wa kumaliza kesi hizo hautoshi na baada ya kushauriana na Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, kifungu cha 114(3) kama kilivyorekebisha na Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sheria Na. 7 ya mwaka 2010, kinaweka muda wa kumalizika kwa kesi za uchaguzi wa Madiwani kuwa ni miezi kumi na nane kutoka tarehe ya kufunguliwa kwa kesi husika. Kama ilivyoelezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali mbele ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala, lengo kuu la mapendekezo haya ya marekebisho "... ni kuwianisha masharti ya kifungu kinachopendekezwa na masharti ya kifungu cha 137(3)(sic!) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ... Sura ya 343 ambapo ... Waziri mwenye dhamana na masuala ya sheria anaweza kuongeza muda usiozidi miezi sita pale inapoonekana dhahiri kwamba kesi za uchaguzi wa Wabunge haziwezi kuhitimishwa ndani ya miaka miwili kama inavyohitajika."

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yanazua maswali mengi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iyatolee majibu mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwanza, hata kama mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 114 cha Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa yatakubaliwa kama yalivyo na kuwa Sheria, hakutakuwa na uwiano kati yake na masharti ya kifungu cha 115 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa kifungu cha 114 kama kilivyo sasa, muda wa kuhitimisha kesi za uchaguzi wa Madiwani ni mwaka mmoja na nusu tokea tarehe ya kesi kufunguliwa. Kwa mpangilio wa kifungu hicho, muda huo unajumuisha pia rufaa katika Mahakama Kuu dhidi ya maamuzi ya Mahakama za Hakimu Mkazi ambazo ndizo zenye mamlaka ya kusikiliza malalamiko ya uchaguzi wa Madiwani. Kwa mapendekezo haya ya marekebisho, muda wa juu kabisa wa kusikiliza kesi hizo sasa utakuwa miaka miwili tokea tarehe ya kesi kufunguliwa, ikiwa ni pamoja na muda wa rufaa katika Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, muda wa kusikiliza kesi za malalamiko ya uchaguzi wa Wabunge ni mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kufunguliwa kwa mashauri hayo katika Mahakama Kuu. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 115(2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 115(5) cha Sheria hiyo, Waziri anaweza kuongeza muda huo kwa kipindi kisichozidi miezi sita endapo itaonekana kwamba muda wa mwaka mmoja hautatosheleza kumaliza mashauri hayo na baada ya mashauriano na Jaji Mkuu. Kwa maana hiyo, muda wa juu kabisa ambapo Mahakama Kuu inaweza kusikiliza mashauri ya uchaguzi wa Wabunge ni miezi kumi na nane, sawa na muda wa sasa wa kusikiliza kesi za Madiwani katika Mahakama za Hakimu Mkazi na rufaa katika Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha 115(3) cha Sheria hiyo ya Taifa ya Uchaguzi, muda wa kusikiliza na kuamua rufaa katika Mahakama ya

Rufani ya Tanzania dhidi ya maamuzi ya Mahakama Kuu ni mwaka mmoja tokea tarehe ya kufunguliwa kwa rufaa husika. Kwa maana hiyo, muda wa juu kabisa wa kusikiliza mashauri ya uchaguzi wa Wabunge, ikiwa ni pamoja na rufaa, ni miaka miwili na nusu. Ni wazi, kufuatana na uchambuzi huu wa Sheria hizi mbili, kwamba mapendekezo ya marekebisha ya kifungu cha 114 cha Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hayawezi 'kuwianisha' kifungu hicho na masharti ya kifungu cha 115 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, namna pekee ya kuwianisha vifungu hivyo ni kukopa (*or to adopt*) masharti yote ya kifungu cha 115 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na kuyaweka katika kifungu cha 114 cha Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii sio tu itatenganisha muda wa kusikiliza mashauri katika Mahakama za Hakimu Mkazi na rufaa katika Mahakama Kuu, bali pia itaweka muda sawa wa kusikiliza kesi hizo na kesi za uchaguzi wa Wabunge katika Mahakama Kuu na rufaa zake katika Mahakama ya Rufani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba tatizo la kutokuwapo uwiano kwa kati ya muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa Madiwani na muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa Wabunge sio tatizo pekee katika Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tatizo kubwa na la muda mrefu kuhusiana na kesi za uchaguzi, ni matumizi mabaya ya haki ya kufungua mashauri ya uchaguzi chini ya vifungu vya 115(1)(a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Taifa, cha Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kifungu cha 111(1)(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi. Vifungu hivyo vinatoa haki kwa mtu aliyepiga kura au aliyekuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi husika kufungua mashauri Mahakamani kupinga matokeo ya uchaguzi huo hata kama yeye binafsi hakuathirika kwa namna yoyote na matokeo ya uchaguzi huo.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia vifungu hivyo vya sheria, Chama cha Mapinduzi (CCM) kimejenga utamaduni mbaya wa kurubuni wapiga kura ambao ni wanachama wa CCM kufungua mashauri ya uchaguzi Mahakamani dhidi ya wagombea wa vyama vya upinzani waliochaguliwa katika uchaguzi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, tunajadili Muswada, siyo siasa tunajadili Muswada, hivyo vya CCM vinatoka wapi? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni inasema tunapojadili Muswada tunazungumzia ubora au udhaifu wa Muswada, siyo mambo mengine. Mheshimiwa Mbunge, tafadhali tuelewane. *(Makofi)*

Naomba uendelee lakini tuelewane kwa sababu wewe mwenyewe unafahamu Kanuni zinavyosema.

MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, najadili vifungu vya Sheria hizi mbili.

MBUNGE FULANI: Sawasawa.

SPIKA: Sasa wapi wameandika CCM?

MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu kuna ushahidi kwamba inafanya matumizi mabaya ya hivi vifungu Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Tindu Lissu, kaa chini.

Waheshimiwa Wabunge, tunatunga Sheria, kuna tofauti, Miswada ile tuliyokuwa tunazungumzia wakati wa kuchangia mlikuwa mnazungumza mnavyopenda kwa sababu mnaji-*limit*, sasa tunapotunga Sheria ni Sheria.

Huwezi katika Sheria ukaandika habari ya CCM, huwezi!
(*Makofi*)

Mheshimiwa Tundu Lissu unajua Kanuni vizuri sana lakini ukipenda kuzikunja unazikunja. Wewe toa maoni yako kuhusu ubaya wa hiyo Sheria walioileta na mapendekezo yake. Hivyo ndivyo inavyotakiwa. Tunatunga Sheria sasa siyo tunahutubia kama tulivyokuwa tumemaliza kuhutubia. Hebu endelea na uelewe kwamba hii ni Kanuni. Mheshimiwa Tundu Lissu anafahamu Kanuni lakini akiamua kukunja anakunja. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, naona nitakuwa mbaya sana...

SPIKA: Tunga Sheria.

MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, najadili Muswada kama ulivyoletwa Bungeni na madhaifu yake. Sijakosea chochote kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama watu hawapendi kusikia wanasemwa vibaya wasiwe wanafanya mambo vibaya.

SPIKA: Hapana, tunatunga Sheria, fuata Kanuni tafadhali. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba tatizo la kutokuwapo uwiano kati ya muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa Madiwani na muda wa kusikiliza kesi za uchaguzi wa Wabunge siyo tatizo pekee katika Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka wa Serikali za Mitaa. Kwa maoni ya Kambi Rasmi Bungeni tatizo kubwa na la muda mrefu kuhusiana na kesi za uchaguzi, ni matumizi mabaya ya haki ya kufungua mashauri ya uchaguzi chini ya vifungu vya 115(1)(a) cha

Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Kifungu cha 111(1)(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi. Vifungu hivyo vinatoa haki kwa mtu aliyepiga kura au aliyekuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi husika kufungua mashauri Mahakamani kupinga matokeo ya uchaguzi huo hata kama yeye binafsi hakuathirika kwa namna yoyote na matokeo ya uchaguzi huo.

Kwa kutumia vifungu hivyo vya sheria, Chama cha Mapinduzi (CCM) kimejenga utamaduni mbaya wa kurubuni wapiga kura ambao ni wanachama wa CCM kufungua mashauri ya uchaguzi Mahakamani dhidi ya wagombea wa vyama vya upinzani waliochaguliwa katika uchaguzi. Katika kesi hizo, CCM na/au wagombea wake walioshindwa, wamekuwa wakilipia gharama zote za kuendeshea kesi hizo ikiwa ni pamoja na kuwalipa mawakili na gharama za usafiri, chakula na malazi ya wanaofungua kesi hizo na mashahidi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, kwa mfano, katika mara zote tatu ambazo Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dkt. Wilbroad Slaa alishinda uchaguzi wa Mbunge katika Jimbo la Karatu, yaani mwaka 1995, 2000 na 2005, alishtakiwa mara zote na watu waijijita wapiga kura, ambao hata hivyo hawakuwa wameathirika kwa vyovyote vile na matokeo ya uchaguzi huo. Katika chaguzi zote tatu, Dkt. Slaa hakuwahi kushtakiwa na wagombea mbalimbali wa CCM aliowashinda kwenye chaguzi hizo.

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ni wa kesi za uchaguzi zilizofunguliwa mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 31 Oktoba, 2010. Mara baada ya matokeo ya chaguzi mbalimbali za Wabunge na Madiwani kutangazwa ambapo CCM ilipoteza majimbo mengi ya Uchaguzi pamoja na Kata, aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM na Mjumbe wa Halmashauri Kuu yake Luteni Yusufu R. Makamba aliwaandikia barua Makatibu wa CCM wa Mikoa yote kuhusu '... Wagombea wa Ubunge/Udiwani CCM Kufungua Malalamiko Kupinga Matokeo.' Katika barua hiyo ya tarehe 9 Novemba, 2011, Katibu Mkuu Makamba aliwaelekeza

10 JUNI, 2013

wagombea hao "... kufungua malalamiko katika Mahakama ya Hakimu Mkazi (Madiwani) au Mahakama Kuu (Wabunge) ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kutangaza matokeo..."

Mheshimiwa Spika, Barua hiyo inathibitisha kwamba Makao Makuu ya CCM hapa Dodoma ndiyo yamekuwa mfadhili mkubwa wa kesi za uchaguzi dhidi ya wapinzani wanaochaguliwa na wananchi kwa kuwabwaga wagombea wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barua hiyo inasema yafuatayo:-
"Chama cha Mapinduzi Makao Makuu kitachangia gharama za mawakili kwa wagombea ambao hawana uwezo wa kifedha." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Aidha, barua ya Katibu Mkuu Makamba inaonyesha mikakati ya kuendesha kesi hizo dhidi ya demokrasia hapa nchini inavyowahusisha viongozi wa ngazi mbali mbali pamoja na wanaoitwa 'mawakili makada' wa chama hicho kikongwe: Inasema barua hiyo:-

"Kwa barua hii, mshirikiane na Makatibu wa CCM Wilaya na Kata na wagombea husika kuandaa hoja za malalamiko na vielelezo au ushahidi na kuwasilisha CCM Ofisi Ndogo Dar es Salaam au kuwasiliana na Mawakili ambao ni makada wetu moja kwa moja ili kuandaa hati za malalamiko ndani ya muda huo." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya barua ya Katibu Mkuu Makamba kusambazwa Mikoani, Wabunge kumi na wanne wa CHADEMA na Wabunge watatu wa Chama cha NCCR-Mageuzi walifunguliwa mashauri ya kupinga kuchaguliwa kwao katika Kanda mbalimbali za Mahakama Kuu ya Tanzania. Kwa upande wa Wabunge wa CHADEMA, ni Wabunge watatu tu ambao walifunguliwa mashauri hayo na waliokuwa wagombea wa CCM. Wagombea wengine kumi na moja walishtakiwa na 'wapiga kura.' Hali kadhalika, wagombea wote watatu wa NCCR-Mageuzi walishtakiwa

10 JUNI, 2013

na 'wapiga kura.' Kesi zote hizo zilitupiliwa mbali na Mahakama Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata baada ya kesi hizo za uchaguzi kutupiliwa mbali na Mahakama Kuu, CCM imeendelea kufadhili 'wapiga kura' na/au 'Mwakili makada' wake kuendeleza mapambano Mahakamani kwa kuwalipa fedha za kufungulia rufaa katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Ushahidi wa jambo hili unapatikana katika kesi inayomhusu msomaji wa maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara ya Mahakama Kuu ya Tanzania, hapa Dodoma kutupilia mbali Shauri la Madai ya Uchaguzi Na. 1 la 2010 kati ya Shabani Itambu Selema & Mwendake dhidi ya Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu & Wenzake 2 tarehe 27 Aprili mwaka 2012, wadai, ambao walikuwa Mwenyekiti na Katibu Kata wa CCM waliamua kuachana na kesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bila wao kujua na bila ridhaa au rufusa yao, tarehe 20 Mei ya mwaka huu Katibu Mkuu wa sasa wa CCM, Kanali Abdulrahman Kinana aliwaelekeza 'Mwakili makada' wa CCM kufungua rufaa katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu uliotolewa zaidi ya mwaka mmoja uliopita! Barua ya kampuni ya Mwakili ya Wassonga *Associates Advocates* ya mjini Dodoma kwa Katibu Mkuu Kinana inarejea 'makubaliano' kati ya Mwakili hao na Katibu Mkuu Kinana juu ya 'Mwakili makada' hao "... kusimamia kesi ya uchaguzi kati ya wanachama wawili wa CCM kwa majina Shabani Itambu Selema na Paschal Hallu dhidi ya Tundu Lissu na Mwanasheria wa Serikali. Katika shauri hilo ... Mahakama ilitupilia mbali kutengua Ubunge wa Mheshimiwa Tundu Lissu."

Mheshimiwa Spika, barua ya 'Mwakili makada' hao inaonyesha wazi yalikutoka maagizo ya kufungua rufaa hiyo katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania na inasema yafuatayo:- "Baada ya shauri husika nilipata maelekezo

kutoka kwa Wanasheria wa CCM kwamba tukate rufaa Mahakama ya Rufaa kazi ambayo tumeikamilisha.” Barua hiyo inaonyesha pia ni nani ambaye amekuwa anawalipa wapiga zomari wa CCM katika kesi za uchaguzi dhidi ya wagombea wa upinzani: Inasema barua hiyo:- “hivyo basi naambatanisha *invoice* ya malipo ya awali ya TShs. 2,000,000/= fedha za maandalizi ya awali ya sababu za rufaa, pamoja na vitabu husika. Ikumbukwe ya kwamba katika shauri la mwanzo nilikuwa nalipwa na CCM Singida Mkoa na hawakumalizia malipo. Pia shauri hili tutahitaji kuongezewa Wakili mmoja kutoka Dar es Salaam na malipo ya usikilizwaji. Wassonga *Associates Advocates* wanahitimisha barua yao kwa kuthibitisha ukada wao wa CCM kwa kauli mbiu ya kwamba “CCM daima kurudi nyuma mwiko”! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Desemba, 2012, Mahakama ya Rufani ya Tanzania – katika kesi nyingine iliyofunguliwa na makada wa CCM, ilitupilia mbali haki ya wapiga kura wasioathirika binafsi na matokeo ya uchaguzi kufungua mashauri ya kupinga matokeo hayo Mahakamani. Kwa maneno mengine, kwa mujibu wa uamuzi wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika Shauri la Rufaa Na. 47 la 2012 kati ya Godbless Jonathan Lema dhidi ya Mussa Hamisi Mkanga & Wenzake 2, wapiga kura ambao haki zao kama wapiga kura hazikuathiriwa na matokeo ya uchaguzi husika hawana haki ya kulalamikia matokeo ya uchaguzi huo. Hivyo basi, kwa uamuzi huo wa Mahakama ya Rufani, hujuma za CCM kuwatumia ‘wapiga kura’ kuendesha kesi za uchaguzi dhidi ya Wapinzani zimefikia mwisho wake kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ilitegemewa, kufuatia uamuzi huo wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania, kwamba Serikali hii ya CCM ingeleta kama sehemu ya Muswada huu mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 111(1)(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na kifungu cha 115(1)(a) cha Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ‘kuviwianisha’ vifungu hivyo na uamuzi huo wa Mahakama ya Rufani. Mapendekezo ya marekebisho ya aina hiyo,

hayapo katika Muswada huu. Badala yake, Bunge lako Tukufu linaombwa kupitisha marekebisho ambayo hata kama yatakubaliwa kama yalivyo sasa, hayatawanisha vifungu husika vya sheria hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu kama inaona haja ya kufanya marekebisho ya vifungu tajwa vya sheria zetu za uchaguzi, ili kwenda sambamba na matakwa ya uamuzi wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika kesi ya Godbless Jonathan Lema dhidi ya Mussa Hamisi Mkanga & Wenzake na haja hiyo ipo.

Mheshimiwa Spika, kama haja hiyo ipo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu ni kwa nini mapendekezo ya marekebisho hayo hayajaletwa Bungeni kama sehemu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali iliambie Bunge lako Tukufu kama Serikali ilikuwa na taarifa za CCM kufadhili kesi za uchaguzi dhidi ya Wabunge wa vyama vya upinzani na lini ilipata taarifa hizo na hatua ilizochukua dhidi ya matumizi hayo mabaya ya mfumo wa utoaji haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho. Kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria na Sheria ya Utumishi wa Umma, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaunga mkono mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria hizo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaridhika na Maoni na Ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusiana na Mapendekezo ya Marekebisho mengine ya Sheria yaliyoko kwenye Muswada huu na haioni haja ya kuyarudia maoni na ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani chini ya uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, kwa michango yao mbalimbali wakati wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ambayo hayahusiani na Muswada, ahsante. Sasa, majadiliano. Waheshimiwa Wabunge wafuatao ndio watachangia Muswada huu; yupo Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, yupo Mheshimiwa Felix Mkosamali, yupo Mheshimiwa Mwaiposa, yupo Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, yupo Mheshimiwa Lekule, yupo Mheshimiwa Moses Joseph Machali, yupo Mheshimiwa Mipata, yupo Mheshimiwa Shibuda, yupo Mheshimiwa Jenista Mhagama, yupo Mheshimiwa Sakaya, yupo Mheshimiwa Christina Mughwai, pole sana, tunafurahi umerudi. Sasa tuanze na Mheshimiwa Rajab Mbarouk.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili niweze kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita katika Kifungu kipya cha 29A, kama inavyooneshwa kwenye Ibara ya 13 ya Jedwali la Marekebisho. Marekebisho ambayo yataziwezesha Halmashauri nchini kuajiri kama watakavyoomba na kukubaliwa na Sekretarieti ya Ajira. Kwanza nataka niishukuru Serikali, kwa mara ya kwanza na nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kweli, kwa kuliona hili na kulileta hapa Bungeni kwa sababu hili lilikuwa ni pendekezo la muda mrefu au miaka mingi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Vilevile, pendekezo hili linasaidia au linatoa majibu ya Taarifa ambazo zinaletwa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC). Aidha, limesaidia kuondoa malalamiko ya Halmashauri zetu katika suala zima lililokumbwa na urasimu katika eneo la ajira.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa rasilimali watu katika Halmashauri zetu ni mkubwa. Katika mwaka uliopita, Halmashauri 25 zilichukuliwa kama sampuli kwa kuangaliwa uhaba huu wa rasilimali watu ambapo katika Halmashauri hizo 25, takribani watu 14,000 walikuwa wanahitajika katika Halmashauri hizo. Kwa hiyo, Sheria hii ambayo leo imeletwa hapa inaweza kusaidia kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, historia inaonesha kwamba, kabla ya Sheria hii ambayo ipo sasa hivi, katika Halmashauri zetu zilikuweco Bodi za Ajira, Bodi ambazo zilikuwa zinasaidia kuleta ufanisi wa ajira katika Halmashauri zetu. Tatizo likaja katika utovu wa nidhamu wa matumizi ya fedha za Serikali na namna ambavyo wenzetu walikuwa wanaitumia fursa hii katika kuajiri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sasa hivi Sheria hii imeletwa na inamtaja Mkurugenzi kama mhusika. Naomba Mheshimiwa AG, hili aliangalie na hapa badala ya kuwa ni Mkurugenzi, iwe ni hii Bodi ya Ajira ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Sheria hii ndio imeletwa, lakini nataka niwatahadharishe Wabunge wenzangu na niwaambie kwamba Sheria imeletwa lakini bado katika Halmashauri zetu tuna tatizo la mishahara hewa kwa wafanyakazi. Mishahara hewa hii ni ya wafanyakazi ambao ama wamefariki, ama hawapo katika kazi kwa hiyo, hili tatizo bado tunalo. Takribani shilingi 693 zillitumika mwaka jana kama mishahara hewa na vilevile zaidi ya shilingi bilioni 1.5 hizi ni mishahara ambayo haikulipwa na haikuweza kurejeshwa Hazina. Kwa hiyo, niwaombe Wabunge wenzangu katika maeneo yao na katika Halmashauri zao, mbali ya kwamba hii Sheria ya Ajira tunaipitisha sasa hivi, lakini tukumbuke kwamba bado tuna tatizo la mishahara hewa. Labda Wabunge wenzangu kwa sababu wapo hapa, niwaambie kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Newala ndio ambayo inaongoza, ina wafanyakazi hewa 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la rushwa. Niwaombe hasa hii Bodi ambayo itahusika na ajira katika Halmashauri hizi waondokane na suala la rushwa. Rushwa hizi kwa kweli zimegawika pengine labda sehemu 3 - 4, kuna suala la *Undugunisation, Uchamanisation, Udinisation*. Kwa kweli, haya tunaomba sana wahusika, hasa Bodi hizi, haya wayaweke pembeni kwa sababu lengo la Sheria hii ni kuleta ufanisi na uwazi. Watakapokwenda katika hali hiyo, kwa kweli, hili lengo la Serikali ambalo sisi Sheria sasa hivi tunataka kuipitisha litakuwa halina mantiki.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri kwa Serikali, wa kwanza, Mheshimiwa Waziri anayehusika na TAMISEMI ni lazima aangalie upya Kanuni zake za Utumishi katika TAMISEMI. Kuna tatizo pale katika Sheria zile. Ukiangalia Kitabu cha Sheria za Kanuni ambazo anatunga Waziri, inasema kwamba ajira zote zitatekelezwa Halmashauri, kwa hiyo, hii moja kwa moja itakuwa inapingana na baadhi ya Sheria ambazo sasa hivi tunazitunga. Vilevile Bodi za Ajira katika Halmashauri ambazo zipo, zinamtaja Diwani mmoja tu kwamba anaingia katika ile Bodi. Naomba hapa Mheshimiwa Waziri, tuangalie uwezekano wa kuongeza idadi ya Madiwani, badala ya Diwani mmoja wawe Madiwani wawili ili kuleta ufanisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kwa kuwa Sheria hii inatoa Mamlaka kiasi tu kwa Halmashauri kuajiri, ni vyema sasa zile nafasi ambazo ni za Kitaaluma, ziwe zinatolewa katika Bodi ya Ajira katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, vilevile ajira zianzie katika Kata na Vijiji na wale wanaoajiriwa wawe ni wale ambao wanatoka katika maeneo yale. Pia kuwe na muda maalum wa kuajiri, ambao Serikali, itaulekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Utumishi ndio *controller of manpower*, itoe idadi ya waajiriwa kulingana na uwezo wa Serikali, baada ya kupokea mapendekezo kutoka katika Halmashauri husika.

10 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa napendekeza, wengi wanaojiriwa sasa hivi, wanakuwa hawapendi kwenda katika zile Halmashauri za pembezoni. Nataka niombe Serikali, baada ya kupitishwa Sheria hii, wajaribu kutoa motisha kwa wale watendaji ambao watawapeleka katika Halmashauri zile za pembezoni ili waweze kukaa katika maeneo yale na waweze kufanya kazi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza yote hayo lakini naomba vilevile ku-*declare interest*, nisije nikaonekana labda nimetetea tu Halmashauri, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, pia nataka niunge mkono kipengele hiki kwa asilimia mia kwa mia ili sasa Halmashauri zetu ziweze kuajiri, hasa wale waajiriwa wa kada ile ya chini.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Felix Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa kama yupo.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimeusoma Muswada huu, nime-*compare* na Sheria zinazohusika...

SPIKA: Wewe ni Mjumbe wa Kamati, sio?

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Na ni Mjumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na baadhi ya vifungu lakini kuna vifungu vingine sikubaliani navyo kabisa. Kifungu ambacho sikubaliani nacho kabisa cha kwanza, ni Kifungu kinachofanya marekebisho ya Sheria ya *The Local Government (Elections) Act, Cap.292* ambacho kinaongeza muda wa miezi sita baada ya ile miezi 18 ya kwanza kwisha.

Mheshimiwa Spika, haki inayocheleweshwa ni haki ambayo inazuiwa na ni haki ambayo inayang'anywa. Leo

tunafanya chaguzi ndogo za Madiwani, watu wako kwenye kampeni, mnasema tuongeze miezi sita kwa watu ambao hawataridhika na matokeo ya uchaguzi. Ukiongeza miezi sita, miezi 18 ukianza kuhesabu mwezi wa saba, ukaweka miezi 18 inaisha 2015 mwezi wa kwanza. Ukiongeza miezi mingine sita, tukimpa haya mamlaka Waziri, kesi hizo zitakwenda mpaka 2015 mwezi wa saba. Sasa mtu ameibiwa kura kwenye *By Elections* ambazo zinafanyika sasa hivi, umwambie aende Mahakamani akapate haki yake 2015 mwezi wa saba ndio kesi iishe. Sheria inakataza kufungua kesi mwaka mmoja kabla ya uchaguzi, haya ni marekebisho ya namna gani? Sheria inakataza *By Elections!* Mimi kwa kweli nitaleta *Schedule of Amendment*, tukatae vifungu hivi. Tunataka Madiwani ambao wanachaguliwa wafanye kazi zao, hatutaki waende huko wasumbuliwe mpaka mwaka 2015 na kesi za hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, lakini hii pia inachochea watu kuiba kura, watu wanakwenda kuiba kura, akijua kwamba nikiiba kura nitakwenda Mahakamani, mpaka mwaka 2015 hakuna mtu wa kunifanya kitu kwa sababu, kesi itaendeshwa mpaka mwaka 2015! Sasa haya ni marekebisho ya namna gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi zote duniani mashauri ya uchaguzi lazima yaende kwa muda mfupi. Hata hii Sheria ya Uchaguzi, mnasema kesi za Ubunge ziishe ndani ya miaka miwili, miaka miwili ilishakwisha, watu hawajaomba kwa Waziri wa Katiba na Sheria kama *National Elections Act* inavyosema lakini kesi zinaendeshwa Mahakamani kinyume na Sheria. Haya mabadiliko hayakubaliki. Ni mabadiliko ambayo yanataka kunyima haki za watu, kesi haziwezi kuendeshwa mpaka 2015, miezi mitatu kabla ya uchaguzi, haiwezekani na hili halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, kuna kesi za Udiwani ambazo zinaendelea sasa hivi Mahakamani. Katiba ya nchi, Ibara ya 13(6)(c), inasema kama hilo jambo halikuwa kwenye Sheria, mtu hawezi kuadhibiwa kwa kosa ambalo halikuwa kwenye Sheria. Leo hii Sheria inatungwa, ili iende ikaongeze

muda kwenye kesi ambazo zimekwisha muda wake. Sheria hii, tumesema, kama haita-*apply retrospectively* itakuwa ni kinyume na Katiba yetu ya nchi, Ibara ya 16. Tunataka mabadiliko haya yasihusu kesi ambazo ziko Mahakamani, ambazo zimeisha muda wake, ambazo wamekuwa wanatufungulia hawa watu wa CCM kuhakikisha kwamba Madiwani wa Upinzani hawafanyi kazi zao, wanashughulika na kesi muda wote, tunataka Sheria hii izingatie Katiba ya nchi, Ibara ya 13(6)(c).

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye Mabadiliko ya Sheria ya *Law Reform Commissions Act*. Nafahamu nia nzuri ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anasema kwamba: "*Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia, kuchapisha, taarifa zozote za Tume ya Kurekebisha Sheria.*"

Mheshimiwa Spika, tunaomba kifungu hiki kizingatie Sheria nyingine za nchi. *The Copyright and Neighbouring Rights Act*, inaruhusu *fair use* ya *public document* kwa *issue* za kitaaluma, inaruhusu na niliuliza hata kwenye Kamati, sikujibiwa vizuri. Kama kuna watu wamekuwa wanaiba *document* za Tume hii, *Penal Code* hii hapa, *Cap 16*, ina vifungu vinavyozungumza *fodgery*; wangapi wamekamatwa na Tume hiyo kwa kutumia *document* hizo vibaya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala sio kuwabana tu, tuambieni mmewakamata akina nani? Nani ametumia? Kwa sababu haya mapendekezo hayana hata *sanction*, hayana adhabu, yanaeleza tu kwamba mtu asitumie, akitumia, mtamfanya nini? Kama mtatumia vifungu vya kwenye *Penal Code*, mmevitumia kwa akina nani ambao wametumia *document* zenu? Tunataka pia *fair use* izingatiwe kama *Intellectual Property Law* inavyosema, mtu akitaka kutumia *document* za Tume hiyo *academically* atumie, lakini kama ana-*forge* awe *punished under the Penal Code*...

MBUNGE FULANI: Ana haki ya kupata taarifa.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Pia kuna haki ya kupata taarifa.

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine inayofanyiwa marekebisho ni Sheria *The Public Service Act*. Haya mabadiliko bado ni madogo, Wabunge wengi wamekuwa wanalalamika kuhusu vibali vya kuajiri. Ndio maana tukasema tunataka Halmashauri na Idara mbalimbali za Serikali, ziweze kuajiri baadhi ya Kada. Ndio yalipaswa kuwa malengo hayo lakini marekebisho ya kumtaka Katibu Mkuu wa Wizara ambaye anatoa vibali hayajaletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tunasema vibali vinacheleweshwa Wizarani, sio na Sekretarieti ya Ajira. Tunataka tuletewe mabadiliko ya usumbufu huo ambao umekuwa unafanyika kwa sababu haya mabadiliko bado hayatatatua lile tatizo, tunaendelea kutoa *discretion* ya kusema kwamba anaweza, "*May publish on gazette to delegate these powers.*" Sasa tunataka iwe *mandatory*, sio ombi, iwe ni lazima. Mambo ya ajira kila Wizara, huwezi ukasema Sekretarieti ya Ajira, ifanye *interview* kwenye kila kitu, haina wataalamu wa kila kitu. Tunataka kama wanaajiri Madaktari, watu wa Wizara ya Afya wahusike kufanya *recruitment*, iwe ni *mandatory*, sio ombi kwamba Sekretarieti ya Ajira wafanye *recruitment* wao, isiwe ni kitu cha kuomba au kupewa, tunataka iwe lazima.

Mheshimiwa Spika, tumesema kwamba tunataka ile Sheria na Kanuni zake za mwaka 2003, zifanyiwe marekebisho makubwa sana. Mheshimiwa Waziri anayehusika, fanya marekebisho ya *Public Service Regulations* za mwaka 2003 kwa sababu zina upungufu mkubwa na zina mkanganyiko mkubwa lakini tunataka kama nilivyosisitiza mwanzoni, tunataka Katibu Mkuu ambaye anachelewesha vibali vya ajira kwa sababu hapa bado kuna *process*, unaomba kwa Katibu Mkuu, *then* unatoka kwa Katibu Mkuu, unakuja tena kusubiri huyu atoe hiyo ruhusa ya kufanya mchakato wa ajira.

Mheshimiwa Spika, huu bado ni urasimu. Sekretariati ya Ajira haiwezi kuwa na wataalam wa kila sekta. Tunataka *interview* zifanyike kwenye idara maalum kama ni watu wa madini Wizara husika ifanye na wala siyo mambo ya *may* tunataka *this thing* iwe *mandatory*.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa, lakini vile vifungu ambavyo sikubaliani navyo nitaleta *schedule of amendment*. Nashukuru.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, nishukuru kupata nafasi ya kuchangia na nitaanza kwa kuchangia katika kifungu kile cha *Local Government Act, 292* ambayo inahusika na kuongezwa kwa muda katika kesi za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya ni mazuri, lakini wakati naanza kutafakari mabadiliko haya nilikuwa najaribu sana kuangalia, ni sababu gani ambazo zilikuwa zinafanya au zinapelekea mpaka kesi hizi kuwa hazimaliziki.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa undani utakuta kwamba tatizo halikuwa muda. Tatizo ambalo lilikuwa linapelekea au linapelekea mpaka sasa kesi hizi zichukue muda mrefu, ni tatizo aidha la fedha za kuendesha kesi hizo, lakini pia liko tatizo la kutokuwa na watendaji wa Mahakama wa kuzishughulikia kesi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, kama sababu ni hizo na hizo nyingine na siyo muda, nachelea sana kusema kwamba hata tukiongeza muda tatizo hili halitapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba, Serikali inahitaji kuongeza bajeti ili kesi hizi ziweze kwenda kwa haraka, lakini pia ili kuweza kuendelea kuajiri Majaji ambao wataweza kuendesha kesi hizi kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe tu kwamba, pamoja na ongezeko hili la muda, basi Serikali ihakikishe

kabisa kwamba, Wizara husika inapata fedha za kutosha. Pia wanawaajiri wataalam wa Mahakama ambao watashughulikia kesi hizo ili ziweze kuendeshwa na kumalizika kwa muda.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo tukisema tu hali iendelee kubaki kama ilivyo sasa ni wazi kabisa kwamba tutafika tena baada ya miaka miwili tutabadilisha tena, tutasema kwamba tunahitaji kuongezewa muda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la msingi liangalie kwamba tatizo lilikuwa ni fedha, lakini pia uhaba wa wafanyakazi katika maeneo ya Mahakama na zishughulikiwe ili tatizo hili liweze kutatuliwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri huo, nije kwenye kile kifungu kingine cha *Public Service Act*, kile kifungu cha 298. Niipongeze sana Serikali imeleta mabadiliko haya kwa muda, baada ya malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi, lakini pia hata watendaji wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini kabisa kwamba Sekretarieti ya Ajira kwa sasa itakuwa imetua mzigo mkubwa. Pia nina uhakika kabisa kwamba, katika Manispaa zetu tutakuwa tumepata fursa sasa ya kuweza kuajiri waajiriwa ambao angalau watakuwa na ufanisi zaidi kwa sababu:-

Kwanza kabisa waajiriwa watakaoajiriwa katika Manispaa zetu nategemea kuwa wawe na uzoefu katika mazingira yenyewe, lakini wawe pia na ule uwoga wa kuwajibishwa na Sekretarieti ya Halmashauri ambayo itakuwa imewaajiri, tofauti na ilivyokuwa hapo mwanzo kwa sababu hapo zamani hata Mkurugenzi alikuwa hana *mandate* au hana ruhusa ya kumwajibisha kama hawajibiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwa sababu itakuwa na ufanisi mkubwa sana katika utendaji wa Manispaa zetu. Hata hivyo, nitoe tu angalizo pamoja na kwamba tumekubaliana hili liwe hivyo, nitoe angalizo sana kwa watendaji wa Manispaa ili katika kuajiri sasa, waweze

kutenda haki na waweze kuwa *fair* na waweze kuwa na utaalum wa kuajiri watu ambao watatuletea ufanisi katika utendaji wa Manispaa.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu maendeleo ya nchi yanaanzia kule chini na kama tunavyojua malalamiko makubwa yamekuwa yakianza kule chini pia. Kwa hiyo, nitegemee kabisa kwamba watu watakoajiriwa watakuwa na ufanisi mkubwa lakini wale waajiri pia watakuwa na ule uwezo wa kufanya *follow up* pamoja na *monitoring* ya utendaji wa watu hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hivyo, niunge mkono hoja na nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Laizer na Mheshimiwa Pindi Chana.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nami najisikia vizuri sana kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyotangulia kusema kwa kweli ni kuweka tu msisitizo, mengi yameshasemwa. Nitajikita kwenye sehemu moja tu, hii ibara ya 12, kifungu kipya ambacho kinaongezwa 29(a). Kwa kweli naipongeza Serikali, nilisikitishwa mara ya mwisho ambapo tulifikiria kwamba, Muswada huu ungepita, lakini haukupitishwa, lakini sasa nimefurahi kwamba umeletwa sasa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyokwisha sema kama nilivyosema kwamba, ni msisitizo zaidi kwa kweli, kimekuwa ni kilio chetu cha muda mrefu, kilio cha watendaji, wananchi kila unayemkuta suala ni hilo. Lakini niseme tu ukweli kumekuwa na tatizo kubwa sana kwenye kuajiri hasa kwenye Sekretarieti ya Ajira, pamekuwa na urasimu mkubwa kwa sababu nyingi tu.

Mheshimiwa Spika, kwanza fedha za kuitisha vikao, pili kuweza kujadili nchi nzima kwa kweli limekuwa ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, hapa tumeweza kuona kwamba, tulikuwa tunahitaji huku chini, kwenye Halmashauri sisi tunaathirika kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, unakuta saa nyingine mnahitaji labda ajira hata ya mtumishi wa chini kabisa, unaletewa mtumishi kutoka Kagera. Fikiria gharama ya kumhamisha kumleta mpaka Kilindi na familia yake, mbali hajakwenda likizo, hajauguliwa na mambo kadha wa kadha. Kwa hiyo, hili jambo kwa kweli naliunga mkono sana na nasema Serikali mmelileta kwa wakati mzuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nataka tu kuuliza vitu vichache kwa sababu nimesema hili suala limeshazungumzwa, nataka tu kuuliza masuala machache. La kwanza, hapa nimesoma lakini haijaainishwa ni ajira zipi, je, ni ajira zote kabisa za kitaalam na nyingine zote ndizo ambazo zimezungumziwa au kuna fungu la ajira maalum. Maana yake tusijepitisha leo Muswada huu, sheria hizi, halafu kesho ikaja mambo tukaanza kujiuliza, ni zote. Makatibu Wakuu nao wanakasimiwa yale mamlaka, ina maana ni ajira zote au kuna *specific*, naomba hilo tuambiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nataka kuuliza je, haya mamlaka hawa Maafisa Watendaji Wakuu wanapewa moja kwa moja au pindi panapohitajika ndipo wanapoomba kibali au ni kwamba, ikishakasimiwa basi ni wakati wowote ni moja kwa moja mpaka mwisho. Hili pia ni vyema kuliangalia vizuri kwa sababu kuna hatari saa nyingine ukawa na mtendaji ambaye pengine si mwadilifu sana au hana zile itikadi zinazotakiwa yaani bora kwenye maadili ya kazi, halafu mambo yakawa mengine, kwa hiyo nataka kufahamu hilo pia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka kuuliza kama mwingine alivyowahi kusema hapa mwanzo, kulikuwa na zile Bodi za Ajira ambazo kwa sasa ni kama hazipo. Je, kutakuwa na Kamati Maalum, kutakuwa na Bodi, au huyu Mtendaji

Mkuu ataamua tu kuteua watu wake ndani ya Wizara au ndani ya Halmashauri kusema hawa ndiyo nawateua, watakuwa wanafanya kazi hii hapa, tunaweza tukazidisha matatizo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kabisa tuelewe hilo na tuambiwe kama patakuwa na mwongozo utakaotolewa katika kufanya kazi hiyo. Lakini je, pia nataka kufahamu mamlaka haya Sekretarieti ya Ajira ina maana wenyewe hawahusiki kabisa tena huko kwenye Halmashauri au ni kwamba maana yake kule kuna tatizo pia la *capacity*, la uwezo wa kufanya hizo ajira hata kama ni zile za chini.

Mheshimiwa Spika, wale watakaoteuliwa kule pengine hawatakuwa na uwezo wa kutosha. Je, Sekretarieti ya Ajira ina maana imejitoa kabisa au wao watakuwa na ushiriki wa aina gani. Watakuwa wanaratibu au watakuja kufanya *monitoring* au ni vipi nao watahusika kwa kweli nisingependa watoke moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka kusema vibali vya ajira. Kwa kweli kabisa hata kama tunasema kukasimu mamlaka huko chini, kama vibali havitoki menejimenti ya utumishi tunafanya kazi bure. Sasa hivi tunashuhudia kwenye Mabaraza ya Ardhi, hakuna Wenyeviti wale wa kuendesha yale Mabaraza. Nafasi ambazo watu walishafanyiwa *interview* siku nyingi, lakini kibali hakuna kwa hiyo sasa hivi tunaathirika.

Mheshimiwa Spika, sasa kubwa hapa kwanza, ni kweli kabisa ni vema tujue hivi vibali tunavipataje. Je, ni sisi wenyewe tunajipanga kule chini tunaamua, halafu baadaye labda kama ni Halmashauri, nazungumzia kwenye Halmashauri ambako ndiko niliko zaidi. Je, kule wanapanga wao wenyewe na kuamua na kusema kwamba sasa kwenye bajeti yetu tumeweka hivi au tutakuwa na mlolongo ule ule wa kusubiri vibali.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu mfano mmoja, kwa mfano Kilindi tuna vijiji 102, Watendaji wako kwenye vijiji 57 tu, vijiji 45

havina Watendaji. Tunavyofanya kazi Mungu anajua, sasa hapa bado tunasubiri kibali, je, kisipotoka. Kwa hiyo, nataka hilo nalo liwekwe sawa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa kweli kama utaratibu huu utazingatiwa na kuratibiwa vizuri, utaleta tija na ufanisi na hakika tutaona mambo ya tofauti na ubora utaongezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibiwe hoja zangu ili niweze kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Michael Laizer atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Moses Machali ajiandae.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie Muswada huu. Kwanza nasikitika kidogo kwa sababu Muswada huu haujatungwa wala Chama cha Mapinduzi hakikuwepo kabisa katika Muswada huu, lakini katika maelezo yaliyokuja kuwekwa na mifano mingi inatoka Mahakamani ambayo haihusiki kabisa na Bunge hili wala Chama cha Mapinduzi hakihusiki kabisa na Muswada huu. Huu Muswada ni kwa wote. Kwa hiyo, wakati mwingine sisi Wabunge tusiwapotoshe wananchi kana kwamba tuko majukwaa ya chama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna marekebisho haya ya Sheria ya Uchaguzi, wakati mwingine inaleta shida sana kwa sababu kesi inaendeshwa kwa muda wa miaka miwili, endapo yule ambaye amelalamika, yeye ndiye alikuwa ana haki, lakini amekaa miaka miwili hayuko Bungeni, baadaye akaja kurejeshwa kwamba yeye ndiye mshindi, anakaa miaka mitatu au miaka miwili na nusu.

Mheshimiwa Spika, je, huyu mgombea haki yake iliyozuiwa miaka miwili naona hapo ni shida kabisa, muda huu ungekuwa ni muda mfupi siyo miaka miwili, kwa sababu yule atakuwa hajatendewa haki, akikaa miaka miwili na

alikuwa ana haki ya kuwa Mbunge, lakini hakuweza kuwa kwa sababu mojawapo ya visingizio vilivyowekwa au kama ni rushwa, pesa zimetumika na ikabainika kwamba mwenzake ameingia kwa rushwa na amekaa miaka miwili hayuko Bungeni. Naona huo muda ni muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni suala la ajira. Unasikia kila siku nikilalamika ajira, ajira. Hii Sekretarieti inayoitwa Sekretarieti ya Ajira imeshindwa kazi, haiwezi kuajiri watumishi wote walioko Tanzania. Vijijini hatuna Watendaji wa Vijiji, hatuna Watendaji wa Kata, tunasubiri ajira kutoka Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Spika, sijawahi kuona mtumishi aliyeletwa na Sekretariati ya Ajira katika Halmashauri ya Longido na tuna matatizo makubwa sana, Halmashauri yote ni Kaimu, Kaimu. Nafasi zingine ambazo watu wameacha au wamestaafu mpaka leo hatujapata watu wa kuingia katika nafasi hizo ambayo ni ajira iliyokuwepo sio ajira mpya. Ukija unazungushwa, unazungushwa na huku tunalalamika kwamba vijana hawana ajira, vijana wako chungu nzima vijijini hawana ajira, nafasi zipo kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Longido nafasi zinazohitajika ni 133, tuna vijana wengi sana ambao wanaweza kuingia katika nafasi hizo, lakini bado tunaambiwa Sekretarieti ya Ajira, Sekretarieti ya Ajira. Naomba sana utaratibu huu ufanyiwe haraka sana ili shughuli za maendeleo zizeze zikafanyika vijijini.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotumwa na Serikali zinakwenda mpaka vijijini kwa sababu miradi iko vijijini, lakini hatuna watendaji wa kusimamia miradi hiyo, hatuna watendaji wa Kata, watumishi walioko Halmashauri, wote ni Kaimu hata kama hana uwezo ni Kaimu. Tunasema kwamba kazi haiendi kwa sababu hatuna watendaji.

Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu huu urudishwe kwenye Halmashauri, nafasi za kitaalam wakasimiwe

Sekretarieti ya Mkoa, waajiri wataalam kwa Halmashauri zinazohusika katika Mkoa ule, kuliko kuwasubiri watu ambao hatuwafahamu ni akina nani, wanaoitwa Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Spika, namwambia Mheshimiwa Waziri hiyo Sekretarieti yenu ya Ajira imeshindwa kazi, haiwezi. Watumishi wanaohitajika hebu angalieni sasa vijiji vilivyoko Tanzania nzima, Kata zilizoko Tanzania nzima bila nafasi nyingine, tumeshindwa kuendesha miradi ya wananchi kwa sababu hakuna watendaji wanaofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana hasa katika Wilaya yangu, naomba kazi hiyo iende haraka sana. Kuna nafasi nyingi tu, hatuna Mhandisi wa Maji, nimelia hapa tunahitaji mtumishi wa maji. Afisa Elimu amestaafu hatuna Afisa Elimu, bado tunazungushwa tu na wako watu wengi sana ambao hawana kazi wanaweza kuingia katika nafasi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hili maendeleo ya wananchi yanakwama kwa sababu hakuna watu wanaofanya kazi. Naomba hii zile Bodi za zamani, Bodi za Ajira katika Halmashauri zetu wapewe mamlaka. Tulikuwa na Bodi za Ajira, Bodi hizo ndiyo zinaweza zikamchunguza mtu, ukiletewa Mtumishi kutoka Dar es Salaam aende katika vijiji vyangu vya Longido kule, aende Glaibomba, aende Matale hata hateremki kwenye gari, anasema sitaki kazi, anaacha kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo watu wanaoweza kufanya kazi katika Halmashauri ya Longido ni watu wanaotoka katika mazingira yale, ndiyo maana Walimu wanakataa kwenda huko. Mturuhusu tuwasomeshe hawa Walimu wanaotoka katika maeneo hayo, warudi waende kuwafundisha ndugu zao ambapo Wazaramo wa Dar es Salaam hawataki kwenda huko. Kuna Wamasai waliosoma wapelekwe huko.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili lifuatiliwe kwa sababu linawaumiza Halmashauri ambazo bado ziko nyuma

kwa sababu walioendelea, waliosoma hawataki kwenda huko, wanabaki bila elimu, zahanati zipo huko, lakini wanakosa Madaktari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mturuhusu, siyo kwamba nabagua, mturuhusu wale ndugu zao ambao wanaweza kwenda kusomesha, wanaweza kwenda kutibu kule katika vijiji hivyo waajiriwe huko huko katika Halmashauri zetu ili waweze kutoa huduma kwa sababu watu wamekaa bila huduma kwa ajili ya kusubiri Sekretarieti ambayo haiwezi kuajiri watumishi wote walioko Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Pindi Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Desderius na Mheshimiwa Shibuda watapata nafasi.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze kwanza kwa kupongeza marekebisho haya yaliyoletwa mbele ya Bunge letu Tukufu, lakini pia nayaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Ibara ya 114 ambayo inarekebishwa, inatoa mamlaka kwa Waziri kuongeza miezi sita katika kesi za chaguzi za Madiwani. Naunga mkono, lakini naomba tuangalie maana tukielekea kwenye mabadiliko ya Katiba, huko mbele nadhani ongezeko hili la muda wa miezi sita lingeweza kufanyika na mhimili wenyewe wa Mahakama badala ya Waziri, maana Waziri ni *Executive* na Mahakama ni mhimili mwingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nayaunga mkono, ni sahihi, lakini tuone ni namna gani, tunaweza kuipa nguvu mihimili hii. Tuna mhimili wa Bunge, Mahakama na Serikali. Hivyo, naunga mkono, lakini jambo hilo naomba tulitafakari kwa upana wake hata kama halitafanyika leo lakini huko mbele tuzipe mamlaka hizi Mihimili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kusema ni kuhusiana na hizi kesi za Madiwani. Nchi yetu haina *private candidates* ina Vyama vya Siasa, na hao Madiwani wanatokana na Vyama vya Siasa ikiwa ni pamoja na Wabunge. Nichukue nafasi hii kupongeza Chama cha Siasa ambacho katika muundo wake kina idara ya Sheria. Maana vinaposajiriwa, Vyama vya Siasa ni kwamba, vinapata mamlaka yaani *can sue or be sued*.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Siasa wadau wake ni hawa Madiwani na Wabunge, kwa hiyo, kama kuna Chama cha Siasa ambacho kinatoa ushauri kwa Madiwani wao na Wabunge wao, Chama hicho kinapaswa kupongezwa na ndiyo jukumu lake. Chama cha Siasa ambacho hakitoi ushauri kwa Madiwani ambao wamechukua fomu kwenye Chama cha Siasa, Wabunge ambao wamechukua fomu kwenye hicho chama lazima tujiwekee maswali, ni chama gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana isije ikiwa chama chenyewe hakitoi ushauri, lakini kinatumia baadhi ya watu ambao ni Mawakili, labda mtu ana taasisi yake au kampuni ndiyo inawatetea watu fulani. Jambo hilo tuliangalie sana! Hiki Chama cha Siasa ambacho kina Idara ya Sheria, *legal Department, Legal Officers*, maana kuna rasilimali watu, ambao wanatoa ushauri kwa wadau wake. Hicho chama kina afya, tena kidumu hicho chama, kinapaswa kidumu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, naunga mkono kabisa, kwa sababu hatuna *private candidate*. Tungekuwa na *private candidates*, tungesema huyu anajitegemea mwenyewe. Hata hivyo, Chama cha Siasa kinapotoa ushauri kwa kwa watu wake au *subjects*, kama wanavyoita Kiingereza, hicho ni chama ambacho kinapaswa kuenziwa, kidumu na kinafaa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Vyama hivi vya Siasa ambavyo watendaji wake wakuu ni Makatibu Wakuu, nadhani wanatakiwa wapongezwe, wanafanya kazi yao

vizuri, kutoa ushauri kwa watu wao. Kwamba, kesi hizi za Madiwani zingatieni muda, kesi hizi zina *limitation of time*; maana watu wanakuja na *profession* tofauti, mwingine mkulima, mwingine mfanyakazi, sasa ushauri akapate wapi?

Mheshimiwa Spika, hawa Madiwani wako vijijini, *Primary Court* hakuna Mawakili wanaoingia kule. Kule vijijini hakuna hata kampuni za wanasheria, sasa ushauri akapate wapi, kwenye Chama chake kinachomhusu. Kwa hiyo, kwa hakika hilo ni jambo la kupongezwa sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu Sekretarieti ya Ajira. Imekuwa ni kilio cha muda mrefu kwamba, ajira zetu hizi zimekuwa *centralized*, lakini leo hatimaye tumepata ufumbuzi mzuri, kwamba, Sekretarieti ya Ajira ikasimu baadhi ya madaraka yake kwenda Serikali za Mitaa na Makatibu Wakuu. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, ningepomba wakati wanatoa katika gazeti la Serikali, zile kada ambazo zitaruhusiwa Halmashauri kuajiri wenyewe, mwanzo tulisema angalau kada kumi, kwa mfano, Madereva, Madobi, Wapishi wanaopika chai, Masekretari, Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningedhani ile list iwe *exhausted enough*, yaani kuwe na *list* ya kutosheleza, ili wanapoandika tangazo la Serikali moja, hizi Halmashauri zipewe Mamlaka ya kuajiri yenyewe, pale ndio unakuja na ile sera inaitwa *D by D*, madaraka mkoani. Jambo hili la kupeleka madaraka na kuziruhusu Halmashauri ziajiri ni jambo ambalo ni muafaka hususan kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu katika eneo hili ni kwamba, ile *list* iangaliwe, iwe ni *list* ya kutosheleza, lakini uzuri ni kwamba, hata mbele ya safari endapo itatokea Kada nyingine muhimu ambayo yamkini mwanzo katika ile *list* ya zile Kada ambazo zinapelekwa Halmashauri ilikuwa

hijazingatiwa kwa kutumia tangazo la Serikali, basi Sekretarieti ya Ajira inao uwezo wa kutoa tangazo lingine la Serikali ili ajira hizo ziende Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka katika Serikali za Mitaa zetu, bado tunazo zile Bodi za Ajira. Bodi za Ajira zipo, kwa hiyo, uwezo wa kufanya hii kazi, katika Serikali za Mitaa wanao, lakini Bodi za Ajira zile kwa sasa zinatumika kwa ajili ya kuangalia masuala ya *promotion* na kadhalika. Kwa hiyo, Bodi hizi za Ajira zitasaidia sana, pia, zitapunguza hata gharama za uendeshaji wa masuala ya ajira.

Mheshimiwa Spika, badala ya mtu kutoka Kijiji fulani, Kata fulani kusafiri kwenda kwenye Ofisi ya Sekretarieti ya ajira na mtu anapotafuta ajira wakati mwingine hata ile nauli anakuwa amekosa. Tunapopeleka kwenye zile Halmashauri inakuwa ni rahisi Halmashauri ile kuajiri watu wake pale pale. Tunachoomba katika mchakato huo, kwanza kuwepo na ushirikishwaji wa wale wajumbe wa Kamati, lakini kuwepo na uwazi na zile taarifa za kutangaza hizo nafasi zifanyike kwa upana wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kwa kweli naungana kabisa na marekebisho haya yaliyoletwa mbele ya Bunge letu Tukufu. Nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Moses Machali simwoni, Mheshimiwa Desderius Mipata, atafuatiwa na Mheshimiwa John Shibuda.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii muhimu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ingawa hammalizi muda, kuchangia ni dakika 15 kwani sasa tuko kwenye Muswada wa kawaida.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye maeneo mawili, mojawapo ni hili linalohusu uchaguzi kumaliza kesi na hili la watumishi. Katika Mamlaka za Serikali

za Mitaa, marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kuhusu kesi, ukiisha uchaguzi zinachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri, kwamba pengine kwa sababu kesi hizo wakati mwingine hazienei sehemu zote, Serikali iwe inaweka utaratibu wa kuongeza nguvu zaidi katika maeneo yenye kesi ili ziweze kwisha na kulinda demokrasia.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka katika Vijiji vyetu tulipokuwa tunafanya uchaguzi, kuna Kijiji changu kimoja cha Msamba, Kata nzima Serikali za Vijiji ziliamua kufungua mashataka. Mpaka walifikia kukata tamaa wao wenyewe kwa sababu, kesi zinaahirishwa, mwisho hata maana ya kuitafuta hiyo demokrasia inakosekana kwani gharama zinakuwa nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pawepo na muda maalum, muda wa miezi iliyosemwa hapa, naona ni mkubwa sana, upungue ili demokrasia ipatikane haraka na watu wakafanye kazi. Hiyo ndiyo italeti maana ya nafasi zenyewe zinazokuwa zinagombaniwa kuliko ilivyo sasa hivi, inachukua muda mrefu na mpaka watu wanakata tamaa, mwisho mtu anasema ninachotafuta ni Udiwani tu, ninaotafuta ni Uenyekiti tu, basi naacha!

Mheshimiwa Spika, sasa hatuwezi kulinda demokrasia katika msingi wa namna hii, au vinginevyo basi katika maeneo yanayosikilizwa pawepo nguvu za watoa haki kama inavyofanyika kwenye kesi za Ubunge. Kesi za Ubunge tunakwenda wakati fulani tunakuta Mahakimu wako watano wanakusanyika, yaani jopo linakusanyika, wanasikiliza. Basi pawepo utaratibu wa namna hiyo pia, katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298. Naunga mkono, kwamba Mamlaka zetu za Serikali za Mtaa zipewe uwezo wa kuajiri, kuwaendeleza watumishi na pia kuwachukulia hatua pale ambapo wanakwenda tofauti na taratibu. Hii ni

heshima kubwa kwa demokrasia kwani tumekubaliana wote kuimarisha Serikali za Mitaa. Tulipowanyima nafasi hii, tumezidhallilisha Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki chote ambacho Sekretarieti imekuwa ikifanya hizi kazi, Halmashauri zimeharibika kabisa. Wezi wamerundikana, Halmashauri hazina uwezo wa kuwaondoa, kwa sababu, meno hawana. Pia, Halmashauri zimeshindwa kujaza nafasi muhimu, tena ndogo ndogo tu! Kwa hiyo, nafasi hii ni muhimu sana kwa Halmashauri na itaimarisha.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri kwamba, pengine tunapoangalia wale watumishi watakaohusika tusi-*limit* sana, wawe wa kutosha, ili nafasi ya Halmashauri ziendeleo kudumishwa. *Autonomous* ambayo tunaisema kwenye Halmashauri ambayo tunataka kujenga, iweze kupatikana. Wawe na uwezo pia wa kuajiri watumishi ambao wanadhani kwa maeneo yao ni muhimu sana. Kwa mfano, watumishi wa elimu, zipo shule zetu nyingine ziko katika maeneo magumu sana na ukipeleka Walimu hawakai.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano, mwambao mwa Ziwa Tanganyika, mpaka juzi mlipotusaidia Walimu wa Sayansi, shule nyingi zina Walimu wawili au mmoja. Tusingetarajia kuleta mabadiliko ya kielimu, lakini kwa utaratibu huu, unaweza hata ukawa-*recruit* wananchi na ukawaajiri watumishi ambao wanatokana na eneo lenyewe. Kwa sababu unawafahamu na wanajua jiografia na wewe unajua, kuliko wakikuletea na kesho wanaondoka.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi, hasa Wilaya ya Nkasi imekuwa ni mlango wa kuajiri tu siku zote. Imekuwa ni mlango wa kuajiri watumishi wa Serikali na kesho hawapo. Kwa hiyo, hii sheria ni muhimu sana kuwapa Mamlaka Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, pia Madiwani wahusishwe katika ile Bodi. Nashauri, hivi Mwenyekiti unamtengaje na hiyo Bodi

yenyewe, ataifahamuje Halmashauri yake? Mwenyekiti wa Halmashauri ni muhimu sana, kwenye Bodi ya sasa Mwenyekiti hayumo, yupo mtu mwingine, haiwezi kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, yeye ndiye kiongozi anayejua upungufu wote katika Halmashauri zetu. Kwa sheria hii, mlango wa kuingiza Watumishi kwenye mfumo wa utumishi, lakini siyo kulenga kwenda kutoa huduma katika eneo linalohusika utazibwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa kutumia utaratibu huu, tutaweza kupata tija inayotarajiwa. Kwa mfano, watumishi wapo wanakuletea, lakini hawafanyi kazi inavyotakiwa na wewe ndiyo unayewasimamia hapa, eti mtu mwingine, yuko mbali kule, ndiyo awachukulie hatua, ilikuwa ni shida kidogo na ilituletea shida. Ndiyo anakuwa na maamuzi na vile vile itaipa heshima Halmashauri kwa sababu gani?

Mtumishi mwenyewe atajua wasimamizi wake wako hapa, wanaompangia kazi, *royalty* yake kubwa itakuwa kwenye Halmashauri hiyo anayoitumikia, kuliko ilivyo sasa, mtu anafikiria kwamba, nililetwa. Maana Sekretarieti nayo siyo Malaika, wakati fulani walikuwa wanaweza wakatoa upendeleo, mtoto wa shangazi, mtoto wa nani, anapitia huko.

Mheshimiwa Spika, anakwenda kwenye Halmashauri ya Nkasi, hawezi kutoka kule na tumeshuhudia, tumepata hata watumishi wengine wakubwa wakubwa tu, lakini hawakutoa huduma nzuri, lakini hupati nguvu za kumwondoa, ana mizizi ya kutosha, lakini kwa utaratibu huu, itatusaidia sana kujenga utawala na kuziwezesha Halmashauri kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muhimu zaidi ni Halmashauri kulinda fedha zake pia. Wapo watumishi ambao ni wabadhirifu kupita kiasi. Kesi zipo tu huwezi kuimaliza, umeifungua lakini huwezi kuimaliza kwa sababu huna mamlaka nayo. Kwa hiyo, anaendelea kukuibia na mamlaka ya kumwondoa huna, hii itatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, sasa nitamwita Mheshimiwa Shibuda, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Tafadhali Mheshimiwa Shibuda!

MHE. JOHN P.M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa nimepata fursa ya kuchangia marekebisho ya sheria hizi, ambazo ni za mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuondoa upungufu uliosababisha kutotekelezwa haki na kuonekana haki imetendeka na kusimamiwa na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, nataka kujielekeza katika marekebisho Sheria ya Uchaguzi wa Tawala za Mkoa. Mchango wangu, unahusu marekebisho hayo kwa kuzingatia kwamba, wahenga husema; heri ya nusu shari kuliko shari kamili. Kesi za uchaguzi kusikilizwa hadi kukamilika ni uwazi na ukweli wa dhana ya kukuza utawala wa demokrasia na siasa katika uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, naomba ifahamike kwamba, marekebisho ya kuridhia kusikilizwa kesi hizi ni utimilifu wa hoja ya kuhakikisha kwamba, malalamiko yaliyowasilishwa Mahakamani yanatengewa muda wa kutosha na kutendewa haki kwa wale waliolalamika na wale walioshutumiwa ili nao wapate haki ya kusafishwa kwamba, walishinda kwa uwazi na ukweli. Kwa hiyo, pande zote mbili zitafaidika na marekebisho haya.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya ya kuongeza muda ni kukamilisha masikilizano ya kujenga imani ya umma kwamba, hata kule vijijini wana haki ya kusikilizwa na Bunge linatenda haki ya kutambua sheria za kuwalinda wanyonge na watu ambao wako vijijini waliogombea nafasi za Udiwani. Si kwa dhana ya umimi na ubinafsi wa kwamba, Wabunge

ikitokea dhana ya matatizo yoyote, tunajielekeza kusimamia haki zetu. Kwa hiyo, hiari ya sheria hii kuongeza muda ni muafaka kabisa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya kuongeza muda ni kutambulisha hitilafu na kasoro za matendo, ambayo yanapaswa kuja kufanyiwa uhakiki wa kuainishwa katika marekebisho ya kuboresha kanuni za uchaguzi na ni faida vile vile ya kutambulishwa kasoro na hila ambazo zikiboreshwa, basi Tume ya Uchaguzi tunayoipigia kelele itakuwa na fursa ya kuja kutenda kazi vizuri zidi.

Mheshimiwa Spika, kupitishwa hoja hii ya marekebisho ya sheria ya kuongeza muda ni kuhakikisha kwamba, tunaondoa hitilafu ya kuchelewa kufanyika kwa marekebisho ambayo yalipaswa kufanyika kwa muda uliopaswa kutendeka.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kufanyia marekebisho kesi hizi zikasikilizwa, ni kuondosha mazalia ya machukizo ya kisiasa, yenye nongwa na hila ya kuja kuzusha kwamba, chama fulani kilitetewa, kilibebwa na sheria au kilibebwa na Serikali, ndiyo maana hapakuwa na muda wa kuongozwa kesi. Hivyo, hii itakuwa inajenga uwazi na ukweli katika masuala ya kusimamia hiari za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kesi za uchaguzi zisipate uliberali wa utoro wa mfereji kupitia Bunge hili. Bunge hili lisiwe ni mfereji wa utoro wa uliberali wa kupitishwa kifuniko cha kwamba, muda umepita. Sisi Bunge letu ni kusimamia haki na kuhakikisha haki inaonekana kutendeka kupitia utungaji wa sheria. Chaguzi kupitia mgongo wa kuambiwa kwamba, muda umepita zisikilizwe na wakati zina hitilafu, ni dhuluma kubwa sana kwa demokrasia ya nchi yetu. Ni dhuluma Kimataifa ikitambulika Tanzania tuna mfumo wa sheria za kusimamia Sheria za Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria yatafungua ufunguo wa fikra za malalamiko ya wananchi kwamba, wana hifadhi ya kwenda kusikilizwa na wana

kimbilio la kwenda kutendewa haki. Kwa hiyo, sheria hii ni ufunguo wa fikra endelevu kwa maslahi ya Watanzania kujitambua kwamba, Bunge linajua na linatambua; ni sikio, ni sauti, ni jicho la kuhakikisha haki inatendeka dhidi ya mdudu ubinafsi na umimi wa kwamba, kwa sababu mtu fulani ulitendewa dhuluma, basi wote watendewe dhuluma, atendaye haki hulipwa mema na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli aliyeshinda kwa shutuma za matendo batili ataweweseka kwamba, sheria hii sasa inamuumbua. Nasikitika kusema ya kwamba, didimizo la kutotendeka sheria hii ni ufunuo wa kwamba, tunajaribu kuwabeba watu ambao wana matendo batili.

Mheshimiwa Spika, napenda kutanabahisha kwamba, hakuna kipindi chochote mwanasiasa yoyote anakosa adui. Mwanasiasa hawezi kukosa adui wa kisiasa wakati wowote, kwa sababu hiyo ni sawasawa na maskini kukosa utajiri.

Mheshimiwa Spika, demokrasia na siasa ni handaki la maficho ya *agenda* za kisiasa ambazo huwa tunaviziana kipindi cha chaguzi. Napenda kusisitiza kwamba, hili handaki la kisiasa, la demokrasia na siasa hutafuta mianya ambayo sheria haikuweza kuona au sheria haikuweza kurekebisha. Papo kwa hapo, huzaliwa shutuma za kutuhumu Serikali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusisitiza kwamba, kesi hizi za uchaguzi zikisikilizwa kwa uaminifu na utimilifu, tutakuwa tunaondoa dhana za kuja kusigana kwa malumbano ya kisiasa ya kuviziana na kushutumiana kwa sababu tu, Bunge lilishindwa kupitisha sheria ya kuongeza muda. Hapana Bunge lisiwe mfereji wa utoro wa haki za kutendeka.

Mheshimiwa Spika, uvundo wa yai moja, hugaribu uzuri wa mayai yote. Kama sheria hii haitaweza kupitishwa ni kutotoa fursa ambazo zitakuja kudidimiza mantiki ya haki za wachaguzi na wachaguliwa. Kujenga uvundo huko, kutaleta

hali ambayo nina hakika kabisa itakuja kuzaa kwikwi la kisiasa na litakuwa ni giza ambazo ni sawasawa na kukuza imani potofu kuhusu demokrasia.

Mheshimiwa Spika, hakuna haja ya kutosikiliza kesi, bali Mahakama isisitize sasa kwamba, baada ya ongezeko la muda huu, wahakikishe kwamba, ugoigoi unaothababishwa na Mwakili au ugoigoi unaozalishwa kwa visingizio mbalimbali unadhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumshauri Jaji Mkuu, kutenga muda maalum wa kusikiliza kesi hizi ili ziweze kutendeka na baada ya kutendeka haki hiyo, basi jamii itakuwa imeridhika kwamba tuna Kiongozi anayetuwakilisha safi na vile vile itatambulisha kwamba, aliyekuwa analalamika huenda alikuwa ni mzushi au alikuwa ana haki na haki kwa uwakilishi wa wananchi ni jambo kubwa sana ili kuonekana wewe una uadilifu dhidi ya malalamiko yoyote.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, ugoigoi ambao huwa unatokea Mahakamani unazalishwa sana na sababu za kisheria ambazo wanaziita sijui *Preliminary Objections*. Naomba Mahakama itambue umuhimu wa kusikiliza kesi hizi haraka na marekebisho hayo ambayo huwa ya kimkakati wa kisheria na yenyewe yadhibitiwe ili kuondoa tabia kifuniko kwa mfumo wa uchaguzi wa kutendewa haki wagombea.

Mheshimiwa Spika, Tanzania bila marekebisho ya kuongeza muda ni demokrasia ya uchaguzi kwenda likizo na kuhamishiwa katika mijadala ya malumbano ya Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wahenga husema, uhaba wa hekima huzaa hila na visa vya kukomoana, lakini tutanguliwe na hekima, tuondoshe hitlafu zetu za nongwa ambazo zinatokana na uzoefu wa maslahi binafsi, tutangulize maslahi ya umma kwamba, tunahitaji kuyatetea kwa maslahi ya uendelevu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya sheria hii ni utambulisho wa ushupavu na ni aminisho la Serikali kwamba wanatetea na kujenga utawala wa demokrasia na siasa, wanatengeneza vile vile mfumo ambao utahakikisha kwamba Tume huru itakayokuja itakuwa ina maboresho ya kutambua kasoro mbalimbali zilizotendeka.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya ni adui dhidi ya wapagazi wa kubeba shutuma za kisiasa kwa malengo ya kwamba, wanatolea mifano ya kesi ambazo hazikusikilizwa na kama kesi hizi zikisikilizwa, basi mtakuwa vile vile mmepaua hoja ambazo zingezaliwa na malumbano ya visingizio vya kesi hizi kuwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, leo tunarekebisha hizi sheria kwa maslahi ya utawala bora na vivyo hivyo napenda kuishauri Serikali na naomba kusesitiza, naomba kumshauri Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aanzishe kisomo au darasa la kuwatambulisha Wakuu wa Mikoa na Wilaya waweze kuwa na wenyewe ni mavuno ya kuletwa marekebisho ya sheria dhulumati dhidi ya maslahi ya uhai wa maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa wanaweza wakawa wanaona kuna sheria ambayo ni gandamizi na kwamba, haiendani na uhai wa marekebisho ya Taifa letu ambalo sasa hivi lina wananchi zaidi ya milioni 40, mifugo imeongezeka, lakini unakuta kwamba sheria tunazotumia ni sheria batili. Kengele ya kwanza hiyo?

SPIKA: Endelea tu.

MHE. JOHN P.M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kusema kwamba, Wakuu wa Wilaya na Mikoa na wenyewe wazalishe hoja ambazo ni batili na ambazo zinazaa kusigana kati ya Serikali na wananchi hasa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kusesitiza kwamba, marekebisho haya ya sheria ni kulinda na kutetea utu, usawa

na thamani ya kuhakikisha kwamba, wawakilishi wa wananchi katika ngazi za Tawala za Mikoa na wao wana hadhi zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya ni kukabiliana na tabia hasi za kuhujumu uadilifu na taratibu za uchaguzi wa demokrasia. Je, mtu aliyewa kama hakukamatwa kwa wakati muafaka, ndiyo kwamba anakuwa amepona mkono wa sheria? Marekebisho haya ni uamsho wa kuthaminika sheria kuwa ni radi dhidi ya dhuluma ya tabia vifuniko ambazo zina maovu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lisiwe mfereji wa utoro wa uhalifu ambao unaweza ukatendeka kwa kutopitisha sheria hii kwamba imepitwa na wakati. Naomba Bunge hili liwe ni msako kwa haki za wananchi na haki za demokrasia na uchaguzi, badala ya kuwa tabia kifuniko kwa visingizio. Waheshimiwa Wabunge lisiwe didimizo la haki za wananchi, na lisiwe didimizo na mfereji wa utoro wa maadili mema yanayohitajika kuja kuhakikiwa na Tume za Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kusema kwamba, tuna kilio cha kwamba, tuwe na Tume Huru ya Uchaguzi, je, kwa nini tusiwe na kilio cha kuwa na sheria huru vile vile za kulinda matatizo yaliyotokana na tabia hasi na desturi hasi katika vipindi vya uchaguzi. Ukiililia Tume huru ya Uchaguzi, lilia na sheria huru za kulinda maslahi ya wanyonge na kuwa sikio la wanyonge na kuwa sauti ya wanyonge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba sheria hii ipitishwe ili tuzibe ombwe ambalo litazaa ghillba, hila na visa ambavyo ni hatarishi kwa uendelevu wa demokrasia na siasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Sakaya, halafu nitamwita mmoja wa hawa Mawaziri, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwa kifupi kwenye Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamesimama wamechangia, nami pia naomba nitilie msisitizo japokuwa sitakuwa mbali sana na wenzangu. Nikianza na ile Sheria ya Uchaguzi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, pendekezo lililoko mbele la kuongeza muda kutoka kwenye miezi 18 kwenda kwenye miezi 24. Mimi binafsi sikubaliani na pendekezo hilo na nadhani pia halina tija kwa Taifa, kwa sababu halitatoa suluhisho la nchi yetu kuendesha kesi za uchaguzi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kesi nyingine, nilitegemea Serikali ingekuja hapa na mpango na mikakati jinsi gani ya kuhakikisha kwamba kesi za uchaguzi zinakwisha kwa muda. Leo tunavyozungumza tangu uchaguzi wa 2010 mpaka leo, *almost* ni miaka mitatu inakwisha sasa, kesi hizi hazijakwisha, sasa tunaziongeza muda kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa hapa, kwanza tutakuwa hatujatenda haki na sheria hii haitatenda haki kwa wananchi ambao wanaongozwa na Diwani ambaye hawakumchagua kwa kura. Diwani ambaye ameingia kwa wizi, ameingia kwa mbinu, kwa rushwa na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini pia haitatenda haki kwa Diwani ambaye amedhulumiwa, ambaye ndiye ameshtaki, amepeleka kesi yake Mahakamani. Bunge letu ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, haki inakuwepo, kwa hiyo, tuisije tukaipitisha sheria ambayo tunajua kabisa itakwenda kunyima haki baadhi ya makundi.

Mheshimiwa Spika, mtu ameingia kwa wizi, kwa rushwa, aendelee kukaa miaka mitano kwa sababu mpaka kesi iishe ni miaka mitano, lakini wale wananchi haki zao ziko wapi, lakini yule ambaye bado anaendelea kukaa *idle*, miaka mitatu, kesi yake haijasikilizwa, haijaisha, haki bado itakuwa iko wapi.

Mheshimiwa Spika, naomba sheria hii kwa kweli Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, aangalie namna nyingine ya kuja na mikakati na mbinu ya kuhakikisha kwamba kesi za uchaguzi za Madiwani zinakwisha kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, sheria nyingine ni sheria ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 200 ya Mwaka 1998. Hapa naunga mkono kwa asilimia mia moja, kwa sababu hili litasaidia sana zaidi ya kuondoa urasimu kwenye ajira, lakini litasaidia sana Mikoa ya pembezoni kuweza kupata watumishi wanaotulia na kufanya kazi kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa ya pembezoni kwa mfano, Mkoa wa Tabora, Wilaya zake, kule Urambo Kaliua, mtumishi anaajiriwa kutoka Serikali Kuu, akifika pale akisaini, akiangalia mazingira pale, baada ya wiki ameondoka, kwa hiyo, hiyo nafasi inabaki wazi pale kwa muda mrefu na hapo ni mpaka Halmashauri isubiri tena juu huku waje waajiri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye maeneo yetu ya vijiji, ukiangalia karibu asilimia kubwa ya vijiji sasa hivi vinakaimiwa, Kata nyingine zinakaimiwa. Kwa hiyo, napongeza maamuzi haya ya Serikali kwa sababu najua kabisa kwamba, yatasaidia kuweza kuwepo na utumishi mzuri kwenye maeneo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pia sheria hii itatoa fursa kwa wale vijana ambao wamezaliwa maeneo yale, wamesomea mbali, lakini wangependa kurudi nyumbani wakafanye kazi kwenye maeneo yao, lakini kutokana na utaratibu uliokuwepo walikuwa wanakosa hiyo fursa. Kwa hiyo, sasa hivi watakuwa ni wa kwanza ku-*apply* zile kazi ambazo ziko ndani ya fani zao kwenye maeneo ya Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wamezaliwa kule, mazingira walishayazoea, wanayapenda, watatulia watafanya kazi kwenye maeneo ambayo yamepangwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia sheria hii ikumbuke mambo mawili ya msingi sana, zipo taratibu gani zinatumika kwenye kukaimu nafasi kwenye ngazi za Kijiji na za Kata, pale ambapo watendaji wanakuwa aidha wamepata matatizo au wameacha kazi? Kwa sasa hivi utaratibu unaotumika, unakuta kwamba, kwa mfano, *particularly* kwenye Wilaya ninayotoka, unakuta Mtendaji wa Kijiji ameondoka au Mtendaji wa Kata, anakaimu mtu ambaye siyo Mtendaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anakaimu aidha ni Mwenyekiti wa Kitongoji au wanamchagua kiumbe yeyote ndani ya Serikali ya Kijiji anakaimu. Kwa hiyo, ndani ya miezi sita mpaka mwaka, unakuta yale maendeleo ya Kijiji yame- *slow* au yamelala kwa sababu yule hawezi kufanya kazi za kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba Serikali itusaidie na sheria iainishe wazi, nini wajibu wa mwanasiasa kwenye sehemu yake ya kazi, kwa sababu kwa maeneo mengine, wanasiasa wanaingilia nafasi za watendaji kwenye kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayo mifano hai tena mingi, naweza nikapewa muda hapa nikaongea mpaka jioni, jinsi gani Madiwani wakiamua kwamba hawamtaki mtendaji fulani, *simply because* hatekelezi matakwa yake, anaweza akamwekea vikwazo akamwambia achia ngazi au anamsimamisha. Hivi kweli, Diwani anaweza kumsimamisha Mtendaji wa Kijiji au wa Kata!

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine, ni viongozi wa chama, viongozi wa chama kushiriki kwenda kukwamisha shughuli za Watendaji Vijijini na kwenye Kata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina mifano hai, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Katibu wake Wilaya mpya ya Kaliua, amekuwa amesimamisha sasa hivi Viongozi Watendaji wasiopungua watatu katika maeneo mbalimbali na anawasimamisha kwa sababu tu, wameshindwa kufuata matakwa yao wanayotaka. Wanaamua wanafanya

mkutano, wana-*mobilise*, wanashawishi wananchi wawakatae viongozi wao kwenye mikutano ya hadhara. Ukifuatilia kwa chini, unakuta kwamba hawakuekeleza matakwa ya viongozi ya chama.

Mheshimiwa Spika, napenda sheria iainishe wazi, hakuna kiongozi wa siasa anayeruhusiwa kuingilia utendaji wa watendaji ndani ya nafasi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naweza kutaja mpaka Kata, juzi wiki iliyopita, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kaliua na Katibu wake, wameandika barua ya kumsimamisha kazi Mwenyekiti wa Kijiji cha Ugunga, ukiangalia sababu hakuna, kwa sababu tu walitaka miradi ya maendeleo wenyewe wapate chochote. Sasa yeye amesimamia misingi ya utawala, kila shilingi inayopatikana iko kwenye maandishi, inatoka kwa vikao, inakwenda kutekeleza kazi zinazotakiwa. Hilo wameona kwao ni vikwazo, tayari sasa hivi yuko kwenye taratibu za kusimamishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Kijiji cha Maboja, Diwani alimshinikiza Mtendaji wa Kijiji kufunga ofisi ya Kijiji kwa muda wa zaidi ya mwaka, tangu mwaka jana. Wiki iliyopita, kaenda kuitisha mkutano kuwaambia wananchi, kwa kuwa Mwenyekiti ameshindwa kuitisha mkutano kwa muda wa mwaka mzima, Mtendaji hakuwepo, namsimamisha uongozi. Utawala gani bora! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana, sheria hizi za Serikali za Mitaa, ziainishe wajibu wa wanasiasa na wa watendaji. Tuache kuingiliana, vinginevyo kama Serikali haitakuwa makini, nafasi za watendaji zikiingiliwa na wana siasa, hakuna kitakachofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matokeo yake tutakuwa tunapiga dana dana tu, kwa sababu ukisham- *frustrate* Mtendaji kule chini, maendeo yanaanzia Kijijini, yanapanda Kata, mpaka mwisho, leo kama tuna m-*frustrate*, hatuwezi kuwa na maendeleo mazuri.

Mheshimiwa Spika, cha kuisitiza zaidi ni kwamba, kwenye suala la ajira, kwenye Halmashauri zetu, kiwepo chombo madhubuti, chombo makini, ambacho hakitafanya upendeleo. Ajira zitolewe kwa uwezo, zisitolewe kwa kuangalia undugu, ukabila au sijui kufahamiana. Vinginevyo kama sasa mamlaka yanatoka Serikali Kuu yanakwenda kwenye Halmashauri wale wakishindwa kutumia mamlaka yale vizuri, tutakuta kwamba tunaanguka kwenye suala la utendaji ndani ya Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI, nakupa dakika 20.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kuunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu. Pia ningependa kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa nini tulianzisha Sekretarieti ya Ajira? Sekretarieti ya Ajira zilianzishwa kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zilikuwepo. Changamoto mojawapo ilikuwa ni ajira kwa misingi ya ukabila katika maeneo mengi sana Serikalini, ofisi nyingi watu walikuwa wanawekeana *succession plan* za kikabila, za kikanda na kadhalika. Kama Serikali kwa kweli tusingeweza kukubali suala hilo liendelee.

Mheshimiwa Spika, lakini pia walikuwepo baadhi ya watumishi au baadhi ya vijana ambao wao kwa sababu Sekretarieti ya Ajira ina-*deal* na wale tu ambao wanaanza kuingia katika utumishi wa umma. Wapo ambao wao walijifanya kazi yao wao ni kila siku wanakwenda kwenye mahojiano, anaomba nafasi ya kazi anapata, anakwenda anaripoti, anapewa fedha za kujikimu, akimaliza anaondoka, anakwenda katika eneo lingine. Kwa hiyo, walikuwa wanaishi hivyo, kwa mwaka wao wanakula fedha tu za kujikimu, suala ambalo kwa kweli ilikuwa ni gharama kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na tatizo la maeneo ambayo yalikuwa hayawezi kuwavutia watumishi, kwa hiyo, anakwenda baada ya siku mbili anarudi, anakwenda katika eneo lingine, kwa sababu kila Halmashauri, kila Wizara kwa wakati wake ilikuwa inafanya usaili.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa siyo rahisi kujua huyu aliajiriwa katika eneo X na asiajiriwe katika eneo hili. Kwa hiyo, tuliamua ajira ifanyike kwa pamoja ili tuweze kuwadhibiti wale ambao kazi yao ilikuwa ni kula fedha za kujikimu tu.

Mheshimiwa Spika, pili, kupunguza suala la kuajiriwa kwa kujuana na kuajiriwa kwa misingi ya ukabila, kikanda au kwa misingi ya udini.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaanzisha Sekretarieti ya Ajira, lengo lilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na ofisi kila Mkoa, ambazo zingeshughulikia na watumishi wa kada za chini, lakini kutokana na changamoto zilizokuwepo, Sekretarieti ya Ajira ilishindwa kujitana kufika katika Mikoa ambapo ingeweza kuajiri kada zile za chini na yenyewe huku juu ikabaki na kada zile za kitaaluma zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono suala la Halmashauri kupewa kuajiri zile nafasi za chini. (*Makofi*)

Kwa sababu uwezo wa Sekretarieti kwa maana ya kifedha, kuwawezesha kufika mpaka kwenye Mikoa, bado hatujafikia, naona itachukua muda, kwa hiyo, kwa kweli tunaafiki lile na pia ukizingatia kwamba, zile kada za chini, Wahudumu, Madereva, wanatakiwa wapatikane kutoka maeneo ambayo siyo ya mbali kutokana na Halmashauri husika, ili kupunguza gharama kwa mwajiri ya kupeleka watumishi wale, kuwapeleka likizo au katika masuala mengine ya kifamilia.

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba mtu kafanyiwa usaili na Sekretarieti ya Ajira na kwamba Halmashauri inashindwa kumchukulia hatua za kinidhamu. Kwa kweli hilo halina mahusiano, kwa sababu Sekretarieti ya Ajira, haiajiri,

inachofanya ni kusimamia mchakato wa ajira, kutangaza, kuwaita kwenye usaili. Wakimaliza wanakukabidhi Halmashauri husika au Wizara husika au Wakala husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya pale, wewe ndiyo unamwajiri, ndiyo unamthibitisha kazini, ndiyo unampandisha cheo na ndiyo unamchukulia hatua pale ambapo anakuwa labda amekwenda kinyume na sheria, taratibu na kanuni ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama wapo Wakurugenzi wa Halmashauri wanashindwa kuwachukulia hatua watumishi kwa kisingizio kwamba wameletewa na Sekretarieti ya Ajira, nasema hapana, huko ni kushindwa kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, pia hata unapoletewa na Sekretarieti ya Ajira, lazima ujiridhishe kwa uwezo wao na vigezo vinavyotakiwa, kwa sababu maeneo mengine aliyekwenda kwenye usaili Sekretarieti ya Ajira ni mwingine na aliyekwenda kuripoti kwenye kituo ni mwingine baada ya kuwa yule aliyeteuliwa hakwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wewe kama mwajiri lazima kwanza ujiridhishe kwa vyeti vyake, kama ni sahihi na kwamba ni mwenyewe. Kwa hiyo, niombe tu zile mamlaka za nidhamu katika Halmashauri zetu na katika Wizara zetu, kwa kweli zifanye kazi ambazo zinapaswa kuifanya.

Mheshimiwa Spika, suala la uwezo wa Sekretarieti ya Ajira kuweza kuajiri watumishi wa kada mbalimbali, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Sekretarieti ya Ajira inayo uwezo kwa sababu wanapoajiri watumishi wa taaluma au wa Wizara husika na wenyewe wanakuwepo katika mchakato mzima, wanahusika, kama ni taaluma fulani, taaluma husika inahusika katika kutunga maswali na wanashirikishwa katika mchakato mzima wa kuajiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Walimu na Madaktari, kwa sasa hivi Sekretarieti ya Ajira haishughuliki

kabisa na Madaktari na Walimu kwa sababu hawa hawasailiwi kutokana na uchache wao, wanapomaliza tu masomo wanapangiwa vituo bila kushirikisha Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nitoe ufafanuzi katika maeneo hayo na niombe tu Halmashauri kwamba tunaletewa hilo jukumu, bado suala la kufuata sheria, kanuni na taratibu litabaki palepale, tuajiri watumishi kufuatana na uwezo wao, kwa sababu kama tutamwajiri mtu bila kufuata vigezo, sidhani kama wenzetu Ofisi ya Rais Manajimenti ya Utumishi wa Umma huyo mtu watakubali aingie kwenye *pay roll*.

Mheshimiwa Spika, yale mengine ya Wenyeviti, sijui wa Chama kuingilia ajira za Watendaji wa Serikali za Vijiji, wote tuliopo hapa ni Wabunge na sisi ni Madiwani katika maeneo yetu. Naomba masuala ya katika maeneo yetu yale ambayo yapo ndani ya uwezo wetu, tuyamalize kule, badala ya kila kitu kukileta ndani ya Bunge hapa na wakati mwingine tukiambiwa tulete uthibitisho na vielelezo ili tuweze kuchukua hatua, unakuta mtu haleti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba yale ambayo kama suala la ajira ya Mtendaji wa Kijiji au kusimamishwa kazi Mtendaji wa Kijiji, nadhani hatulitendei haki Bunge letu, siyo suala la kuletwa ndani ya Bunge. Tusitumie fursa ya kuwa ndani ya Bunge hapa kuja kupumua kila kitu ambacho kinatushinda katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Nimekupa muda wangu wa bure. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi, nakupa dakika 20 ukimaliza maliza na ukiacha basi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba tutofautishe kati ya Waajiri na mchakato wa ajira katika Sekretarieti ya Ajira. Jukumu kuu la Sekretarieti ya Ajira ni kuwezesha zoezi la kuendesha mchakato wa ajira wa watumishi katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya waajiri. Kuendesha mchakato yaani *Recruitment Process* na ukisema kuendesha mchakato ina maana gani?

Mheshimiwa Spika, kwanza unaangalia nafasi ipo; pili, unatangaza hiyo nafasi; tatu, unafanya *short listing* na nne, unafanya *interview* na baada ya *interview* unafanya *shortlisting* au unateua hao watumishi ambao wame-*qualify* au *candidates* walio-*qualify*. Baada ya kuwapata *candidates* walio-*qualify* unawapeleka kwa mwajiri na mwajiri ndiye anayetoa barua ya ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuelewe kwamba, Sekretarieti ya Ajira haiajiri bali inasimamia mchakato wa ajira yaani inasimamia sheria, kanuni na taratibu za ajira kama zinafuatwa. Hilo ndilo jukumu lao kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu wanaosema kwamba Sekretarieti ya Ajira inaajiri, hapana, haiajiri bali inafanya mchakato wa ajira. Naomba hili tulitofautishe kati ya mchakato wa ajira na kuajiri. Naomba hilo kwanza niliweke wazi.

Mheshimiwa Hawa Ghasia amelieleza vizuri sana suala la kwamba kwa nini hiyo Sekretarieti ya Ajira ilianzishwa. Niongeze jambo moja tu kwamba, Sekretarieti ya Ajira imesaidia sana hasa katika Wilaya zilizopo pembezoni, kuna wakati kuna baadhi ya Halmashauri zilikuwa zikitangaza nafasi hawawapati watu katika sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, lakini Sekretarieti ya Ajira ikiajiri *Centrally*, inasema kabisa kwamba nafasi hii ni kwa ajili ya Makete, mtu anayekuja kufanya *interview* anajua kabisa anakwenda Makete. Kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kuwapeleka watumishi wengi katika sehemu zilizopo pembezoni.

Mheshimiwa Spika, hata kwa Mheshimiwa Laizer kulikuwa hakuna watumishi wala Wahasibu, wakati tunaanzisha ile Wilaya kulikuwa hakuna Wahasibu wala watendaji, lakini sasa hivi anasema kwa mfano *Engineer* tu ina maana wafanyakazi wengine karibuni wote wamepatikana, isipokuwa wafanyakazi wa Kada za chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusibeze sana kwamba hiyo Sekretarieti ya Ajira haikusaidia, imesaidia kwa kiasi kikubwa, kwani imeleta Utaifa, imepunguza mrundikano wa watu wa aina fulani kuwa katika sehemu fulani, wamerundikana Wapogoro watupu katika Wizara fulani, hiyo imepungua kwa kiasi kikubwa na Wabunge ninyi ni mashahidi.

Mheshimiwa Spika, kwani kulikuwa na watu wamerundikana katika Wizara fulani, wote kuanzia mwanzo mpaka mwisho na kama alivyosema Mheshimiwa Ghasia wanajiwekea kabisa *succession plan* kwamba nikitoka mimi, mwingine anayefuata atakuwa wa aina hiyo hiyo. Kwa hiyo, Sekretarieti ya Ajira kwa upande huu imesaidia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Sekretarieti ya Ajira siyo ya kuibeza kwamba haijafanya chochote, imefanya kitu kikubwa na imeleta Utaifa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo wamechangia ni kuhusu uwezo wa Sekretarieti ya Ajira. Tunasema kwamba wapo watumishi wa kada mbalimbali na wapo watumishi wa *profession* mbalimbali katika Sekretarieti ya Ajira. Ukiangalia kifungu cha 29(6)(d) wanasema kwamba Sekretarieti ya Ajira lazima iwa-*co-opt Ma-experts* kutoka sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati wa *interview* inawachukua *Ma-experts* kutoka sehemu mbalimbali na hatuna shida ya *Ma-experts* katika nchi hii. Kwa hiyo, kama wanaofanyiwa *interview* ni vyo vikiu wataletwa *Ma-professor*, Madokta ndiyo wanawa-*interview* wale wa Vyuo

Vikuu. Sekretarieti ya Ajira ipo pale kuangalia kwamba je, *rules na regulations* zinafuatwa? Ndiyo inachofanya pale! *Ma-experts* wanatoka katika sehemu fulani.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kabisa hata Ofisi ya AG tulikuwa tunawaajiri *Ma-state Attorney*, mitihani wametunga wenyewe sisi tuliwekwenda kusimamia, *interviews* zote wamefanya wao wenyewe, lakini lazima mkono wetu uwepo kuhakikisha kwamba je, sheria zinafuatwa? Kwa hiyo jamani, uwezo tunao na sheria inaruhusu ku-*co-opt members* kutoka sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, kwa vyyo vikuu ni hivyo hivyo na sehemu mbalimbali inakuwa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia, Waheshimiwa Wabunge wamehoji kwamba, je, kada zote mta-*delegate cadre* zote? Tunasema hapana! *Profession cadres* zitabaki bado kwenye Sekretarieti ya Ajira, lakini *common cadres* au kada za kawaida tutazishusha kwa waajiri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuta-*delegate whole* kwamba hata Wahasibu na kadhalika tuwapeleke kwenye Halmashauri, hapana, tunapeleka *common cadres* na siyo kwa Halmashauri peke yake ndiyo maana tunasema kwa Mamlaka za Ajira, hizo *common cadres* tutazishusha huko, lakini *profession cadres* zitabaki bado kwenye mikono ya Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Beatrice amezungumzia kuhusu vibali. Ni kweli vibali tunaangalia uwezo wa Serikali, kila mwaka tunatenga fedha kiasi fulani kwa ajili ya ajira lakini tunaangalia pia na vipaumbele vya Kitaifa. Kwa mfano, kwa miaka karibu kumi sasa hivi, kipaumbele namba moja ni elimu, kwa hiyo tunaajiri Walimu wengi kutoka Vyyo vya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, tunatenga kwanza mahitaji ya Elimu ni kiasi gani, tunatenga kwanza wa Afya kiasi gani na sasa hivi tumeongeza wa Kilimo pamoja na Mifugo, kiasi gani wanaobakia ndiyo tunawagawa katika makundi mbalimbali

kutokana na uwezo wa Serikali. Huwezi kusema kwamba tutaajiri Watendaji wa Vijiji wote kwa mwaka mmoja, hapana, hiyo haitawezekana! Kwa hiyo, tunaangalia vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa mwaka huu tunaajiri watumishi 61,000 tumegawa kabisa kwamba tunaanza na Walimu 34,000, tunafuata Madaktari 11,000, tunafuata mifugo na kilimo 3,000, halafu nafasi nyingine 11,000 tunazigawa katika kada mbalimbali yaani tunaangalia Wahasibu, wafanyakazi wa ardhi, wafanyakazi wa wanyamapori na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuwezi kusema kwamba, tutawaajiri wote hawa *common cadres* kwa wakati mmoja, bali tutawaajiri kwa awamu mpaka hapo nafasi zote tutakapozijaza, lakini kipaumbele ni elimu na kwamba tunatoa vibali kulingana na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, vibali wakati mwingine siyo vinacheleweshwa tu na Utumishi bali hata waajiri wenyewe, wanatakiwa kwanza waajiri waweke kwenye bajeti yao nafasi husika, bila kuweka kwenye bajeti mfumo wetu uliopo sasa hivi Utumishi hautakubali, unatema!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unatakiwa lazima nafasi iwepo na umeiweka kwenye bajeti, lakini usipoiweka kwa mfumo wa sasa hivi hata ukiajiri mtu wa aina hiyo hawezi akaingia kwenye mfumo wa *Human Capital Management Information System* tuliou-centralise Utumishi. Kwa hiyo, waajiri ni vema wakati wa ajira wakawa waangalifu sana katika kuchagua kada ambazo wanaona kwamba ni muhimu katika sehemu zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuchelewa kwa vibali, ni kweli, vibali vinachelewa kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tunaanza kwanza kwa vipaumbele, tunaangalia kwanza zile kada ambazo ni vipaumbele na tukishaajiri zile ndiyo tunatoa hizo kada nyingine. Huo ni utaratibu wa kawaida ambao

tumejipangia, tunaangalia kwanza zile kada ambazo ni muhimu tunaona tuajiri kwanza zile ndiyo tunaajiri watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wote ni muhimu, lakini tunaangalia kwenye pengo zaidi, elimu ni wachache sana, Madaktari ni wachache sana. Kwa hiyo, tunahakikisha tuna-*absorb* Madaktari wote, tuna-*absorb* watumishi wote wa elimu na baada ya hapo ndiyo tunaangalia watumishi wengine wa kada mbalimbali. Kwa hiyo, siyo tunachelewesha hivyo vibali kwa makusudi, bali tunakwenda kwa mahesabu na kwa vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba Sekretarieti ya Ajira haijafanya lolote, nasema kwamba, nimeshalizungumzia hilo na limesaidia sana kwa watumishi waliopo pembezoni na ya pili tumepunguza sana matumizi, ilikuwa kila mwajiri anatangaza kwenye magazeti kwa hiyo, mzigo ulikuwa mkubwa sana wa matangazo, lakini sasa hivi anayetangaza ni mmoja tu anatangaza kwenye Mtandao.

Mheshimiwa Spika, hivyo tume-*minimise cost* kwa kiasi kikubwa sana na sasa hivi tume-*delegate*, mtaona hiyo *cost* pia itaanza kupanda tena kwa sababu kila Halmashauri itatakiwa itangaze nafasi zake ambazo ni *common cadres* na kila mwajiri au kila taasisi inatakiwa itangaze hizo *common cadres*. Kwa hiyo, utakuta kagharama katapanda kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Taifa letu na kwa faida ya hizo kada ambazo zipo chini ambazo kwa kweli Sekretarieti ya Ajira ilikuwa ni vigumu sana kuwafuata kule chini na kufanya *interview*, kwa kweli tumeona kwamba ni muhimu kwa sasa nafasi hizo zikafanyiwa usaili kule kule, *the whole process* ya *recruitment* ikafanyika kulekule kwa waajiri husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kukaimu kwa muda mrefu. Suala la kukaimu kwa muda mrefu lipo na nalifahamu

lakini Waheshimiwa Wabunge mnalalamika hapa Bungeni kwamba kuna watumishi wabovu, wakuu wa idara wabovu, kuna wezi, kuna mchwa na kadhalika.

Sasa mnaposema kwamba tusitumie ile *process* ya *vetting*, tutumie *shortcut* kwa kweli hatuwezi tukatumia *shortcut* kwani watumishi wa aina hiyo ni lazima tuwafanyie *vetting* ili tupate watumishi waadilifu.

Mheshimiwa Spika, hatufanyi hivi kwa makusudi bali tunafanya hivi kwa manufaa ya umma kwamba huyo mfanyakazi au Mkuu wa Idara au Mkurugenzi kabla hujampandisha cheo au hujamfikisha huko, ni lazima tumfanyie *vetting*, tena *thorough vetting* kwa kina kwamba, je, ni mwadilifu? Je, ametoka wapi, amefanya nini? Je, historia yake ikoje? *Vetting* hiyo hatuwezi tukatumia *shortcut* hiyo ni lazima tutaifanya.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli kwamba wakati mwingine inachukua muda mrefu, lakini wakati mwingine inachukua muda mfupi, inategemea na huyo ambaye mnamchakachua je anafaa au hafai.

Mheshimiwa Spika, mtu mwingine anakaimu na anapokaimu unamfanyia *vetting* na ukimfanyia *vetting* anaonekana ana uchafu. Akiwa na uchafu inabidi uombe majina mengine uanze tena *vetting*, kwa hiyo una *rivet* yaani unafanya *vetting* kwa watumishi wengine, ndiyo maana inachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini tutajiahidi na tunashirikiana sana na TAMISEMI kwa sasa hivi kuhakikisha kwamba, tunafanya mchakato huu kuwa mwepesi, kuna njia ambazo tumetumia na kwa kweli baadhi ya sehemu tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ule mlolongo wa kuchukua muda mrefu labda miaka miwili au mitatu, hapana! Sasa hivi ni miezi sita na sanasana imezidi miezi tisa, tunashirikiana na wenzetu kuhakikisha kwamba, huo

mlolongo unapungua, lakini hatutumii *shortcut*, tunashirikiana sisi wenyewe kwa wenyewe ili kuhakikisha kwamba tunawapata watumishi walio bora.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuchangia tu hiyo *Public Service Act, Cap, 298* kuhusu hiyo ya ku-*delegate* kwa mamlaka husika nafasi mbalimbali ili waweze kufanya huo mchakato wa ajira.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, ni jambo la muda mrefu, lakini sasa hivi tumefanikiwa, nawashukuru. Tukilipitisha sisi mara moja tutahakikisha kwamba, tunatoa *Government Notice* ili kuhakikisha kwamba, waajiri wanaajiri nafasi mbalimbali ambazo tumeshaziainisha na tumeshirikiana na taasisi zote. Kwa mfano, TAMISEMI tumeshirikiana nao pamoja na taasisi mbalimbali kuhakikisha hizo *common cadres* tuna-*delegate* kwenda huko chini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Jenista Mhagama ndiyo msemaji wetu wa mwisho kwa asubuhi hii.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Kabla sijaendelea niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze sana hawa Mawaziri wetu, yaani akina dada wawili lakini kwa kushirikiana na Kamati yetu. Kwa kweli Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia tunawashukuru na tunawashukuru sana kwa kuleta marekebisho ya hii sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inazungumzia kupeleka maendeleo kwa wananchi. Unapozungumzia kupeleka maendeleo kwa

wananchi zaidi ya 80% ya Watanzania wanaishi vijijini na unaposema Watanzania wengi wanaishi vijijini, ina maana kwamba Watanzania hawa 80% wanahitaji sana watumishi wa kuweza kufanya kazi za uendeshaji katika Halmashauri zetu za Vijiji, Mitaa na kwenye ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuhamisha utaratibu wa ajira wa kada ndogo za uendeshaji za chini ninazosisema na kuzipeleka kwenye Tume ya Utumishi, tulikuwa tunajichelewesha wenyewe na tulikuwa tunachelewesha maendeleo ya wananchi na hasa kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni shida kubwa, Watendaji wa Vijiji katika Jimbo la Peramiho, Halmashauri ya Songea, wasubiri Sekretarieti ya Ajira ikawatahini Dar es Salaam, ikasimamie mchakato wao wa ajira Dar es Salaam, halafu waje kurudi kufanya kazi, ilikuwa ni kazi ngumu sana!

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kada hizi za uendeshaji ninazosisema yaani Watendaji na hata Madereva kwenye Halmashauri zetu wanapoonna mchakati ni lazima ukafanyike kwenye Sekretarieti ya Ajira ingawa wakati mwingine mchakato ulikuwa unaanzia Mikoani, mtu anapohitajika asafiri kwenda Dar es Salaam pesa ya kumpa ya chakula tu mtu asiyekuwa na ajira, hawezi kuwa nayo unapomwambia atafute sh. 100,000/= ya kwenda Dar es Salaam kutafuta kazi, anakata tamaa.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunapoteza vijana wengi na wazuri ambao wako tayari kufanya kazi na wenye moyo wa uzalendo wa Kitanzania, wanajua maisha ya Watanzania wenzao walipo na wako tayari kujitolea kwa hali na mali kuleta maendeleo kwenye Kijiji, Kata, Mtaa na kadhalika, walipotezewa ari ya kufanya kazi na kuitumikia Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unakuta tulipoteza vijana wazuri wengi sana kwa sababu huu mchakato ni kweli ulikuwa mzuri kusimamiwa na Sekretarieti, lakini huo mlolongo wa kuchukua hayo mamlaka na kuyaweka mbali na wao

tulikuwa tumejikuta badala ya kuendelea kwa haraka, tulikuwa tunachelewesha maendeleo kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, leo Mawaziri hawa wameelewa wajibu wao, wamepambana na wameamua kuleta mabadiliko haya, nakuhakikishia kwamba na sisi Wabunge tukienda kusaidiana na Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba, haya yote waliyoyagatua kwenda kwenye Halmashauri yanasimamiwa vizuri, tutapunguza sana tatizo hili la ajira katika Halmashauri zetu. Madereva watapatikana, tutakuwa na watendaji kwenye Halmashauri zetu, tena wale ambao sisi tunafikiri kwamba wapo tayari kufanya kazi kwenye mazingira yale.

Mheshimiwa Spika, nikuchekeshe tu, unapotoa tangazo, mtu aliyepo karibu na lile tangazo ataomba lile tangazo. Ukichukua picha labda Mtendaji wa Kijiji cha Magwamila aombe kijana kutoka Bukoba, anaanza safari kutoka Bukoba anakuja mpaka Dar es Salaam. Akifika Dar es Salaam anauliza bado sijafika? Anaambiwa bado una kilomita 1,000, anaanza safari kutoka Dar es Salaam, anafika Njombe kwako.

Mheshimiwa Spika, akifika Njombe anauliza bado kilomita ngapi? Anaambiwa bado kilomita kama mia tatu na zaidi, halafu anaanza kupanda Milima ya Ukumburu, akifika Songea anaambiwa Magwamila bado hujafika, bado kuna kilomita nyingine mia moja mpakani mwa Tanzania na Msumbiji ndiyo utakwenda kufanya kazi, anaghairi! Anafunga mizigo yake anarudi, wewe Jenista na Magwamila yako na Jimbo lako la Peramiho mtajjua wenyewe huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaona kiutekelezaji, sheria hii ilikuwa inatupa shida sana, lakini ukimleta Afisa Mtendaji kutoka Njombe, Songea anapajua, hata akienda Magwamila ile milima ya Njombe ni sawa na ya kule anaona alaah! Kumbe nipo mazingira hayohayo tu sina matatizo.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya yatatusaidia sana kuondoa tatizo la watumishi wa kada za uendeshaji katika Halmashauri zetu. Ndiyo maana nayaunga mkono kwa asilimia mia moja na nawaomba Wenyeviti wa Halmashauri zetu, Bodi za Ajira katika Halmashauri zetu, Waheshimiwa Wabunge wengine wamependekeza kwamba Mheshimiwa Waziri katika kutengeneza kanuni tuangalie kuongeza Madiwani watakaotusaidia kusimamia ndani ya Bodi za Ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kufanya hivyo yapo pia matatizo ambayo Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana na hasa Mama yetu Mheshimiwa Hawa Ghasia, hata kwenye Halmashauri bado tuna matatizo. Unaweza ukakuta masuala ya kuwachakachua wananchi katika mlolongo huo yakawa yameongezeka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kanuni zetu ziwe imara, ziwe na nguvu na tuongeze idadi ya Madiwani kwenye Bodi za Ajira, tutengeneze kanuni zitakazoweza kuwa na nguvu kufanya mchakato wa ajira uwe kweli kwa kupata watumishi bora, wenye moyo wa uzalendo watakaokwenda kufanya kazi kwa heshima ya maendeleo ya wananchi wa Tanzania na hasa Vijijini ambapo nimesema wako karibu 80%.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba, nakubali kabisa Sekretarieti ya Ajira kubakiwa na ajira za kada za juu na za kitaalam, hiyo nakubali kabisa. Leo hii kuanza kuiambia Halmashauri iajiri Madaktari aah! Tutapata tabu! Tunaweza kuajiri Madaktari huko katika utaratibu ambao kwa kweli haueleweki wa sintofahamu. Ukisema leo Halmashauri zianze kuajiri Ma-engineer wao wenyewe eeh! Tunaweza kupata kazi, tunaweza kuajiriwa huko Ma-*engineer* mwisho, tukachanganyikiwa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nakubali na ndiyo maana nasema hebu hizi kada za kitaalam tuziache huko kwenye ngazi za juu zishughulikiwe na Sekretarieti ya Ajira, lakini Sekretarieti hiyo ya Ajira Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri

Waziri wetu, pamoja na kusema kwamba unachukua muda mrefu kutoa vibali, kujaza mapengo ya kukaimu kwa sababu unafanya *vetting*, naomba hebu tafuta njia ya kufanya *vetting* kwa haraka na haya mapengo kwenye Halmashauri zetu yaishe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Waziri anaposema anafanya *vetting* kwa muda huo wote, hata hao allowafanyia *vetting* kwa muda mrefu na wao hivyo hivyo wana matatizo, wana matatizo makubwa. Hao anaosema Wabunge tunalalamika nao ndiyo hao hao allowafanyia *vetting* kwa miaka kumi au mitatu na kadhalika, bado wako hivyo hivyo tu.

Mheshimiwa Spika, anafanya kila siku *vetting* lakini hiyo *vetting* yenyewe bado inaleta watumishi wengine, ni taabu na ameona kwenye *report* mbalimbali za CAG za utendaji kazi, unakuta kabisa unashangaa huyu *Engineer* ametoka wapi? Ana vitabu vyote amesona na ana vyeti vyote, lakini ametoka wapi?

Mheshimiwa Spika, unaangalia huyu ndiye Mkaguzi wa Ndani, lakini unashangaa ametoka wapi? Anakaguaje hesabu za ndani halafu Halmashauri inapata hati chafu, mwaka wa kwanza hati chafu na mwaka wa pili hati chafu. Unajuliza sasa hizo *vetting* wanafanyaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hii isiwe ni sababu. Kwanza tunaomba kabisa suala la kukaimu madaraka kwenye Halmashauri zetu liishe, tuweke kigezo Halmashauri moja isiwe na Wakuu wa Idara zaidi labda ya wawili ama watatu wanaokaimu, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, tuna vijana wengi wamesoma, wanatafuta kazi, kama hatuna ndani ya Serikali, chukueni hao vijana wanaotafuta ajira, lakini Halmashauri moja unaweza ukakuta watendaji saba, Wakuu wa Idara sita wote wanakaimu, miaka inapita wanakaimu. Hiyo *vetting*

isiyokuwa na mwisho, tunamwomba Mheshimiwa Waziri *vetting* zake ziwe na mwisho na kweli ziwe zinasaidia maendeleo ya Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vibali vya ajira bado vinachelewa sana, sisi Waheshimiwa Wabunge humu ndani ni wajumbe wa Kamati za Fedha na Mipango, kila mnapokutana kwenye kikao ukiuliza hivi vile vibali vya ajira tulivyoviomba vimeshatoka? Unaambiwa bado.

Mheshimiwa Spika, nadhani tutakapoweka kanuni zetu na tutakapokuwa tunasimamia, suala zima la ajira na hasa kwenye Serikali za Mitaa, naomba sana tujitahidi ili vibali vya ajira viwe vinatoka mapema, mapengo yaliyoachwa wazi yawe yanazibwa mapema.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia sana Halmashauri zetu kupata watumishi wa kutosha wenye uzoefu na sifa zinazotakiwa watakaosimamia utendaji kazi mzuri katika Halmashauri zetu katika Sekretarieti za Mikoa lakini hata katika ngazi za Wizara kama vile Muswada unaosema kwamba hata Makatibu Wakuu watagatuliwa madaraka watakwenda kuajiri kulingana na mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja hii kwani inakwenda kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo kwa wananchi wa Halmashauri ya Songea, wananchi wa Jimbo la Peramiho na naamini sasa tutasimamia vizuri ili tatizo la wafanyakazi katika Halmashauri zetu liveze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuwapongeza tena sana hawa akina Dada hawa wawili Waheshimiwa Mawaziri, kwa kuamua kwa dhati kuleta mabadiliko ya hoja hii na mimi kwa ari kabisa na kasi nzito naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, Bunge lisitumike kama sehemu ya utetezi wa kesi zilizopo Mahakamani, kwani wachangiaji wananukuu kesi zilizopo Mahakamani, zinazoendelea ambazo maamuzi yake bado. Je, Kanuni zinasemaje?

Mheshimiwa Spika, pale ambapo watu wanatajwa hawana fursa ya kujitetea mfano katika mchango wa leo wa Kambi wa Upinzani Kanuni za Bunge zinasemaje?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa neema na rehema zake nyingi kwangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu una maana na faida kubwa kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tatizo nilionalo mimi ni uwajibikaji wa Serikali katika kusimamia sheria. Vyombo vya kutoa haki na kusimamia sheria vinakosa bajeti ya kutosha ili kutekeleza majukumu yao. Pamoja na hilo pia tatizo la kujuana (*undugunization, ukandanization*) ulioko kwenye vyombo vya kusimamia na kutoa haki.

Mheshimiwa Spika, muda huu wa miezi 18 mpaka miezi 24 kwa kesi za Udiwani ni mwingi sana. Hata kesi za Ubunge miaka miwili mpaka miaka miwili na nusu ni muda mrefu sana kwani muda huo ni nusu ya muda wa utumishi kwa Mbunge husika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa vyombo vinavyohusika vijengewe uwezo kwa kupewa *manpower* ya uhakika na ya kutosha, yenye weledi, ari na nia njema ya kuitumikia Taifa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo wapewe bajeti ya kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Pia kuwe na *"Supervising Secretariat"* ya kusimamia ufanisi katika kutoa haki. Hii *"Supervising Secretariat"* Jaji Mkuu awe ndio Kiongozi na *regulator* wa hilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo kuwe na kipengele cha adhabu kwa watoa haki pindi ikibainika wamepindisha haki kwa makusudi, upendeleo au wamepokea rushwa. Hii itasaidia sana ufanisi katika kutoa haki hasa kwa kesi za uchaguzi na kesi nyingine zote.

Mheshimiwa Spika, haki ndio msingi wa mambo yote mema katika nchi ikiwemo amani, utulivu, upendo na ustaarabu wote.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kupewa mamlaka ya kuajiri watumishi wa kada za chini ni jambo bora na zuri. Ushauri wangu hapa ni kuwe na Tume ya Uajiri ya kila Halmashauri ili kusaidia kuepusha rushwa, upendeleo, udugu na kadhalika na kuacha kuwapa haki ya kuajiriwa watu wema, wachapakazi, weledi na waaminifu kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri huo nilioutoa katika mchango wangu, kuwajibika na kuwajibishwa kwa wazembe, wezi, wabadhirifu wa mali na rasilimali za nchi ni jambo la msingi na muhimu sana ili kujenga misingi ya uwajibikaji katika nchi.

Mheshimiwa Spika, inawezekana, timiza wajibu wako. Ahsante sana.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, suala zito ambalo limeikabili nchi hii katika Halmashauri zetu ni matatizo ya ajira. Halmashauri nyingi zimewekwa watumishi ambao wanakaimu nafasi ambazo zinasubiri watumishi ambao wataajiriwa na chombo kinachoitwa Sekretarieti ya Ajira. Sekretarieti ya Ajira itaundwa lini ili iweze kutupatia watumishi wa kudumu na sio watu wanaokaimu nafasi zinazosubiri kuajiriwa kama wataalam?

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunalia na ubadhirifu unaofanywa katika baadhi ya Halmashauri zetu. Hivyo ikiwa watu hawana uhakika kwamba utendaji wao utapelekea ajira hizo, hivyo hatuoni kwamba ubadhirifu unaotokea kwenye Halmashauri husika unasababishwa na hii Sekretarieti ya Ajira ambayo haiwajibiki katika kutoa ajira kwa wanaohusika?

Mheshimiwa Spika, ni vyema Sekretarieti ya Ajira ikakasimu madaraka kwa Mikoja na Wilaya ili watendaji waajiriwe kisheria, tuondokane na kufanya kazi kwa kukaimu ili tuweze kufanya kazi kwa umakini na ufanisi ambao utaweza kuleta tija. Hata hivyo, Halmashauri ziajiri watu wenye uwezo kwani kuna baadhi ya Halmashauri zina watumishi ambao uwezo wao wa kiutendaji ni mdogo na hautoshi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kesi za uchaguzi zina wajibu wa kuwekewa muda usiozidi miezi mitatu tokea kufunguliwa na kupatikana haki kwa aliyechaguliwa. Vilevile endapo aliyelalamika ameshinda arejeshewe haki zake zote ambazo alikosesha kabla. Kinyume chake ni kukosesha haki kwa mlalamikaji ambaye alishinda na hakutangazwa.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura 292, kifungu cha 114 ni ya msingi kwa wale ambao kesi zao zimesimama Mahakamani kwa kupita muda wa miezi 18.

Mheshimiwa Spika, hata kama marekebisho hayo yatapita na kukubaliwa hapa Bungeni bado hakuna uhakika kuwa kesi hizo zinaweza kuisha kwa miezi sita kwani pamoja na sababu nyingine zilizochelewesha kesi hizo ni ukosefu wa fedha wa kuziendesha.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, nashauri Mahakama itafute fedha popote ili kesi hizo zikamilike. Nashauri kwa uchaguzi ujao Serikali itenge fedha maalum kwa ajili ya kukabili kesi za uchaguzi ili wananchi waendeleo kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 ni kukaimu madaraka ya uajiri kwa baadhi ya kada za utumishi kwa Wizara, Taasisi za Umma na Halmashauri za Serikali za Mitaa. Hilo ni jambo zuri lakini katika vikao vya ajira kwa Halmashauri inabidi apatikane mjumbe kutoka Utumishi na kwa hali ilivyo sasa mjumbe huyo anaweza akatoka kwenye Mkoa au Utumishi Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo, mjumbe huyo anaweza akasababisha gharama ya kifedha kwa Halmashauri. Hivyo ni vyema Utumishi wakaimarisha mfumo wa kiutawala mpaka Wilayani. Kwa kufanya hivyo, mjumbe kutoka Wilayani atapunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hautoshi kwa mtoa hoja kuweza kujibu hoja zake na nadhani kuna marekebisho mengine yameletwa, mkayaangalie vizuri, tutakapofika tutatoa hoja halafu tutasoma Muswada kwa mara ya pili kifungu kwa kifungu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mchana wote muwahi, kama itakuwa akidi haitoshi, basi sheria haipiti na sheria hii tumeipa upendeleo kwa sababu ya umuhimu wake. Sasa kama hamtakuja mchana na *quorum* itakuwa haitoshi tena, haitapitishwa. Kwa hiyo, naomba muwaambie na wenzenu waliopo huko najua wapo ili wawahi kuja siyo waje saa kumi na mbili bali waje mapema.

Baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 6.45 mchana Bunge liliahirishwa
mpaka Saa 11.00 jioni)*

10 JUNI, 2013

(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi, wachangiaji wetu waliokuwa wameomba kuchangia wote walipata nafasi. Kwa hiyo, sasa nitamwomba mtoa hoja aweze kutoa ufafanuzi katika hoja mbalimbali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 17, kati ya hao Wabunge 13 wamezungumza hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wanne wamechangia kwa maandishi na baadhi ya Wabunge wengine wamezungumza nami, kwa hiyo, pia nimechukua mawazo yao.

Mheshimiwa Spika, idadi hii ya wachangiaji ni ushahidi kwamba, suala la marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo, linamhusu kila mmoja wetu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati; kwanza, kwa maelezo yake aliyoyotoa ambayo yalifafanua sana maudhui ya Muswada. Pia maelezo yale yalikuwa ya kina, yalieleweka vizuri kwa Waheshimiwa Wabunge na nina uhakika pia kwa Wananchi ambao walikuwa wakimsikiliza nao walielewa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa hotuba yake na maoni yake kuhusu Muswada huu. Hata hivyo, mambo mengine ambayo ameyasema hayahusiani na Muswada huu na sitaweza kuyazungumzia.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho katika Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni suala ambalo limezungumzwa kwa kina. Nipende tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, kama Sheria hii itapitishwa, tumekwishamshauri Mheshimiwa Jaji Mkuu, kuagiza ifanyike Operesheni Maalum ya kusikiliza kesi za mashauri ya uchaguzi ya Madiwani na kuzikamilisha. Kwa hiyo, tutauzingatia ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Eugene Mwaiposa, kuhusu suala la bajeti na rasilimali watu. Pia tutazingatia wazo ambalo limetolewa na Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Desderius Mipata. Hata hivyo, hili la Mheshimiwa John Shibuda, labda nichukue nafasi hii kumpongeza kwa tanabahi yake ya lugha na jinsi alivyoweza kufafanua vizuri sana kwa kutumia lugha hiyo nyepesi, shabaha ya matokeo ya mabadiliko haya ambayo tunapendekeza.

Mheshimiwa Spika, ninatambua ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Felix Mkosamali na Mheshimiwa Tundu Lissu, kuhusiana na marekebisho haya tunayopendekeza kwenye kifungu cha 114 cha Sheria hii ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Ninawashauri Waheshimiwa hawa wawili kuutafakari sana mchango wa Mheshimiwa John Shibuda, Mbunge wa Maswa. Marekebisho haya yanatoa haki ya kusikilizwa. Kwa vile wote wawili hawa ni Wanasheria, marekebisho yanatoa haki ya kusikilizwa katika mashauri ya uchaguzi wa Madiwani ambayo yalipaswa kumalizika kwa kipindi cha miezi 18, yaani kufikia Mei, 2012. Mashauri hayo hayakumalizika kwa sababu ambazo hazikusababishwa na wadawa, yaani wale wenye kesi zile siyo waliosababisha hayo. Marekebisho haya yanaliomba Bunge kutoa mamlaka kwa Mahakama kusikiliza na kufikia tamati ya kesi hizo ili kutoa haki panapostahili.

Mheshimiwa Spika, nina hakika Bunge haliwezi kufumbia macho watu kupoteza haki zao kwa sababu ambazo hazikusababishwa na watu hao. Aidha, siyo sahihi kuelekeza lawama kwa kuwa Mahakama hazikupewa rasilimali fedha za kuendesha mashauri hayo. Hivyo, kwa

kuwa hizi ni haki zinazoweza kupatikana kwa njia hii, muda huu tunaliomba Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge, tukubali muda utolewe. Nirudie tena kwamba, ukisoma Jedwali la Marekebisho, mamlaka ya kuongeza muda huo siyo ya Waziri wa Katiba na Sheria, mamlaka hayo yanatolewa kwa mahakama zenyewe, zikiona inafaa kufanya hivyo na kwamba itakuwa ni utekelezaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, na hili kwa sababu Mheshimiwa Tundu Lissu alilisema sana, nafikiri alikuwa hajalionga au kuzingatia Jedwali. Ibara ya 4 ya Muswada lazima isomeke na Jedwali la Marekebisho. Kinachopendekezwa ninarudia, siyo kumpatia Waziri anayehusika na masuala ya sheria mamlaka ya kuongeza muda, ila ni kuipa mahakama iliyokuwa inasikiliza shauri yenyewe mamlaka ya kufanya hivyo kwa kuzingatia haki za kisheria za wadawa (wadawa ni wale wanaohusika na kesi, mshitaki au mshitakiwa) na kuzuia matumizi mabaya ya sheria.

Mheshimiwa Spika, maneno aliyotumia Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba, lengo kuu ni kuyaainisha masharti haya na kifungu cha 137 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, hayakutumika katika hotuba yangu. Tunachopendekeza sisi na ambacho kilisemwa kwenye Kamati ni kutumia dhana (*concept*) ya kuongeza muda ambayo iko kwenye Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, wa kusikilizwa kwa mashauri ya uchaguzi wa Madiwani kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu lizingatie kwamba, marekebisho haya hayafanywi kwenye Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na hivyo hayahusiani na uchaguzi wa Wabunge. Tunachozungumzia hapa ni Madiwani wanaochaguliwa kwa mujibu wa sheria. Ninakubaliana na Mheshimiwa Tundu Lissu, anaposema katika ukurasa wa tatu wa hotuba yake kwamba, mapendekezo ya kifungu cha 114 cha Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, hayawezi kuwianisha kifungu hicho na masharti ya kifungu cha 115 cha Sheria ya

10 JUNI, 2013

Uchaguzi. Ni kweli na ndivyo tunavyosema, sheria hii inajitegemea.

Ninaridhika na naomba Waheshimiwa Wabunge mridhike kwamba, kifungu hicho kitasomeka kama kilivyo kwenye Jedwali ambalo tumeligawa asubuhi. Tutakuwa tumepata ufumbuji wa tatizo la kushughulikia kesi ambazo zilikwishasilizwa au zilifunguliwa kwa wakati lakini haziwezi kusikilizwa kwa kuwa muda wa miezi 18 uliowekwa na sheria umekwishapita na Mheshimiwa John Shibuda amelieleza vizuri sana hili jambo.

Mheshimiwa Spika, imetolewa kauli kuhusu haki za watu wanaoweza kufungua mashauri mahakamani, anayeweza kulipia gharama za kuendesha mashauri hayo na uwepo wa Mawakili ambao ni makada wa vyama vya siasa. Hakuna katazo kwa chama chochote cha siasa kuwasaidia wanachama wao kulipia gharama za uendeshaji wa kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katazo pekee, narudia na mnisikilize vizuri, katazo pekee la msingi na la kistaarabu ni kwamba, vyama vya siasa na Mawakili ambao ni Maafisa wa Mahakama, wasishiriki katika vitendo vya kupotosha haki kutendeka. Hilo ndiyo katazo la msingi, hivyo badala ya kulifanya Bunge kuwa kituo cha malalamiko, Mheshimiwa Tundu Lissu kama mhusika katika kesi hizo, anaweza kuiomba Mahakama itamke kwamba, haki ilipotoshwa huko huko na siyo humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, marekebisho tunayopendekeza kufanyika ni machache sana. Hata hivyo, kutokana na mchakato wa kuipatia nchi hii Katiba Mpya unaoendelea hivi sasa, kutafanyika pia marekebisho makubwa katika sheria za uchaguzi. Nina hakika marekebisho haya yatazingatia maamuzi mbalimbali ya mahakama ya juu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni wakati unaofaa kuwakumbusha tena Waheshimiwa Wabunge kwamba, Muswada tunaoujadili na niliouwasilisha leo asubuhi,

unasomeka pamoja na Jedwali la Marekebisho; hivyo, marekebisho yaliyomo kwenye Jedwali yamependekeza marekebisho kwenye Ibara ya 4 ya Muswada, ambayo sasa inazingatia maoni ya Waheshimiwa walioshauri kwamba, mamlaka za kuongeza muda baada ya muda wa uchaguzi kumalizika ziwe ni za mahakama zenyewe. Tumezingatia hilo. Sasa kwa sababu hili ni la kitaalam, mambo mengine ningependa kuyazungumzia wakati tutakapopitia kifungu kwa kifungu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mapendekezo kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria; kwenye hili ninamshukuru sana Mheshimiwa Felix Mkosamali, ameleta Jedwali la Marekebisho akipendekeza Ibara ya 8 ya Muswada ifutwe. Ibara hiyo inabeba katazo la kutumia, kutoa taarifa, kuchapisha habari au hati yoyote ya Tume ya Kurekebisha Sheria, bila idhini ya Tume. Ili kufahamu, tutafika huko kama atakuwa bado anaendelea, tutazungumza na kuelimishana. Ili kufahamu tunachopendekeza ni vyema kurejea kifungu cha 24 kilichopo ambacho kinasema, kwa ruhusa yako naomba kunukuu:

“The records of the Commission shall be public records for purposes of the Records and Archives Management Act”. Hicho ndicho kifungu kilichopo na kifungu hicho cha msingi hakijaguswa. Mapendekezo tunayotoa ni kwamba, watu wasitumie taarifa za Tume kabla hazijatolewa hadharani au zile ambazo ni za awali, yaani *drafts*. Mantiki ya katazo hili ni ya msingi kwani zinaweza kutumika kupotosha kwa kuwa hazijakamilika au hazijazifikia mamlaka zinazotajwa kwenye kifungu cha 14 cha sheria hiyo. Kwa mfano; Tume ilifanya uchunguzi kuhusiana na hoja ya adhabu ya kifo. Kabla hajjamaliza kazi hiyo, watu wengine wakawa wanatumia hizo taarifa kupotosha kwamba, Serikali ina mpango wa kuondoa adhabu hiyo. Hayo ndiyo mambo ambayo tunafikiri yanastahili kuzuiwa. Siyo kuzuiwa tu, tunasema kwamba Tume yenyewe itatoa idhini na kama itatoa idhini basi itatumika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lilihusu Sheria ya *Public Service Act*. Kwanza, nawapongeza Wabunge wote

kwa ujumla wao, wamepongeza kwamba Serikali imeleta marekebisho na mapendekezo haya. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri; Hawa Ghasia na Celina Kombani, kwa ufafanuzi wao. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Pindi Chana. Rafiki yangu Mheshimiwa Rajab Mbarouk, alikuja mpaka kwenye Kamati akatupa mawazo yake kuhusiana na ile Ripoti ya CAG. Namshukuru sana Mheshimiwa Rajab Mbarouk. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine, wamelizungumzia jambo hili vizuri sana. Sasa hapa pia Mheshimiwa Felix Mkosamali, anashauri kwamba, pale kuna maneno tunatumia kwamba yule *Secretary may*, yeye anapendekeza badala ya kutumia neno '*may*' tutumie neno '*shall*' kwa maana kwamba sasa iwe ni lazima kufanya hivyo. Mamlaka ya asili ya Katibu ambayo ndiyo kiini cha pendekezo hili, yameelezwa kwenye kile kifungu cha 29 na sasa tunaweka kifungu kidogo cha 29 (a) kwamba, anaweza kuyatumia mamlaka yake yale kwenda mahala pengine. Kwa utaratibu wa kisheria, mamlaka ya asili yale uliyonayo au ambayo yameletwa kwako, yaani *powers delegated to you*, kwa kawaida hatakiwi kuzitoa tena. Wanasheria watajua ule msingi kwamba, mtu aliyepewa madaraka au mamlaka hawezi kuyapeleka kwa mtu mwingine. Kwa kilatini wanasema *delegatus non protes delagare*, kwa maana kwamba huwezi kupeleka mamlaka uliyopewa kwa mtu mwingine. Hata hivyo, hapa tunafanya hivyo kwa sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Katibu amepewa mamlaka na kutosema kwamba baadhi ya mamlaka haya ayapeleke, ni vizuri abaki na ile nguvu ya kujadiliana na kukubaliana na hao wanaopewa mamlaka hayo kusudi aweze kufanya ile *hands off, but eyes on*. Nafikiri ndiyo ilikuwa msingi wake.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza na mambo waliyoyazungumza kwa kweli yanahusu vifungu, na hayo niliyosema ndiyo nafikiri yalikuwa makubwa. Hata hivyo, kuna hili la Mheshimiwa Tundu Lissu,

10 JUNI, 2013

kwa kuwa yupo nilikuwa nasita kulisema kwa sababu hakuwepo; kama nilivyosema mwanzo, mapendekezo tunayofanya kwenye kifungu cha 114 ni mapendekezo yanayojitegemea; ni wazo zuri.

Hatujafanya mapendekezo ya kubadilisha Sheria ya Uchaguzi ya Taifa kwamba, kile kifungu cha 115 cha Sheria ya Uchaguzi ya Taifa kibadilishwe kwa msingi ambao Mheshimiwa Tundu Lissu anasema. Hayakuwa mapendekezo yetu na tunafikiri mapendekezo yanayopendekezwa kwenye Sheria ya Uchaguzi yasubiri wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na bila kutaja majina ya Wabunge wote, naomba kuishia hapo. Naomba Waheshimiwa Wabunge, waniunge mkono tuweze kupata hii sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)

MWENYEKITI: Sasa ni Kamati ya Bunge Zima, siyo Kamati ya Matumizi, wala siyo mshahara wa Waziri, maana mshahara wa Waziri unatafutwa hauonekani. *(Kicheko)*

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2013 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2013)*

Ibara ya 1

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.
FREDERICK M. WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL DURING
THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN
LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, 2013**

Made under S.O. 86(10)(b)

The Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act, 2013" is amended generally as follows:

- A: By deleting the phrase "The Written Laws Miscellaneous Amendments)" whenever it appears in the Bill, and substituting for it the phrase "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2)".
- B:- By deleting Clause 4 and substituting for it the following:-
- C: By deleting Clause 7 and substituting for it with the following:-
- "General Amendment **7.** The principal Act is amended by deleting the title "Secretary whenever it appears in the Act, and substituting for it the title "Executive Secretary".
- D: By deleting Clause 10 and substituting for it with the following:
- "Amendment of Section 6 **10.** The principal Act is amended in section 6(1) by-
- (a) deleting the title "Director of Local Government Authority" and substituting for it the words "Local Government Authority;
- (b) adding immediately after paragraph (b) the following new paragraph:
- "(c) oversee and ensure career development of employees in their respective organization."

E: By deleting Clause 11 and substituting for it with the following new Clause:

"Amendment
of section 14

11. The principal Act is amended in section 14 by- (a) deleting subsection (2) and substituting for it the following new subsections:

"(2) The Secretary shall be the chief executive and accounting officer of the Commission and shall, subject to subsections (3), attend meetings of the Commission but shall not vote at such meetings.

(3) The Secretary shall not attend Commission's meetings deliberating on disciplinary referrals of employees of the Commission."

F: By deleting Clause 12 and substituting for it the following:

"Amendment
of Part VI

12. The principal Act is amended in Part VI by-

(a) adding immediately after heading "SPECIAL PROVISIONS" the following subtitle:

"(a) The Public Service Recruitment Secretariat";

(b) designating subtitles (a), (b) and (c) as (b), (c) and (d) respectively."

G: By deleting immediately after Clause 12 the following new Clause:

"Addition of
Section 29A

13. The principal Act is amended by adding immediately after section 29 the following new section:

Delegation of
Functions and
Powers of the
Secretary

29A.-(1) The Secretary may, by Notice published in the *Gazette* delegate to any Chief Executive Officer, the functions and powers of the Secretariat to conduct recruitment process in the Service.

10 JUNI, 2013

(2) The functions and powers delegated to the Council under subsection (1) shall be exercisable pursuant to the Regulations made under this Act.

(3) For purposes of this section:

(a) "chief executive officer" includes the Permanent Secretary or Executive Director of Public Institution or of such other employing authority; and

(b) "Council" has the meaning ascribed to it under the Local Government (District Authorities) Act or the Local Government (Urban Authorities) Act."

Dodoma,
8th June, 2013

FMW
AG

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

MWENYEKITI: Mheshimiwa Felix Mkosamali!

10 JUNI, 2013

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. FELIX F. MKOSAMALI, MEMBER OF PARLIAMENT FOR MUHAMBWE CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, 2013"

Made Under S.O 86(9) & (11)

The Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2013" is amended as follows:-

- A: By deleting Part II.
- B: By re-numbering Part III and IV as Part II and III respectively.
- C: By deleting the proposed Clause 8.
- D: By deleting the word "may" appearing between the words "secretary" and "by" in the proposed Clause 29A and substituting for it the word "shall".

Dodoma

10th June, 2013

HON. FELIX F. MKOSAMALI (MB.)

MUHAMBWE CONSTITUENCY

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimependekeza kifungu cha tatu na cha nne; kifungu cha tatu kinaeleza mabadiliko haya yatahusisha Sheria Mama, lakini nimesema kwamba *Part Four* yote itoke, *Part Two* yote itoke kwa sababu kifungu cha tatu hakina mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachozungumza ni

kwamba, tukiruhusu marekebisho haya pamoja na Jedwali la Marekebisho aliyoyaleta Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuna *by-elections* ambazo zinafanyika sasa hivi; ni kwamba kesi hizo tukizipa miezi 18, halafu tukaipa Mahakama muda tena wa kuongeza, kesi hizo zitafika mwaka 2015 mwezi Juni au mwezi Julai na Sheria ya Uchaguzi inasema, miezi 12 kabla ya Uchaguzi Mkuu hakuna *by-election*.

Tunachotaka sisi ni kesi hizi kwisha mapema, lakini marekebisho haya yanataka kuwanyima haki watu watakaobiwa kura kwenye *by-election*. Mtu akiibiwa kura atakuwa anajua kwamba akienda Mahakamani kesi itasikilizwa mpaka 2015 na hatakuwa na haki ya kufungua shauri. Sasa ninachopendekeza, haya mabadiliko yafutwe, Sheria ibaki kama ilivyokuwa zamani, hatuna haja ya kuongeza muda hapa.

Mabadiliko haya pia yanakwenda kuingilia kesi ambazo zimekwishakuanza zamani Mahakamani. Nilieleza wakati ninachangia, Ibara ya 13(6)(c) ya Katiba inaeleza huwezi uka-*impose*, sheria imbane mtu wakati hiyo sheria haikuwepo wakati kosa hilo linafanyika. Sheria hairudi *retrospective*, nimezungumza hivyo. Kwa hiyo, nasema haya mabadiliko bado hayajakidhi matakwa ya sasa hivi, tunakwenda kuumiza watu, kura zitaibiwa na watu watakwenda Mahakamani wakijua kwamba, kesi zitaendeshwa kwa muda mrefu na hawatapata haki yoyote na hakuna *by-election* itakayofanyika.

Kwa hiyo, haya mabadiliko mimi nashauri tuyakatae, waende wakajipange upya watuletee vizuri ili tuweze kwenda kutibu tatizo lililoko huko.

MWENYEKITI: Mwanasheria Mkuu!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Ibara ya 13(6) ya Katiba haihusiki. Kwa msingi kwamba, hayo makosa anayoyasema ni makosa ya jinai na ni vizuri kwenye mambo haya ya uchaguzi, usitangulize mambo mabaya kwamba watu wanaiba kura,

wanafanya nini. Nafikiri hilo siyo suala la msingi. Suala la Msingi ni kwamba, tunazo kesi katika Uchaguzi uliopita ambazo zilipaswa kwisha miezi 18, yaani Mei, 2012, kesi hizo hazikusikilizwa hata kama ziliskilizwa bila ya kutolewa hukumu kwa sababu muda ulikuwa umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mapendekezo tunayoyafanya sasa hivi, ndugu yangu Felix Mkosamali, ukisoma tunasema *the court shall continue, we are talking about the past, shall continue the hearing. Sorry, naomba kusahihisha pale "The Court shall continue with badala ya the. "The court shall continue with hearing and determination of an election petition beyond the period prescribed by subsection (3) if, lapse of eighteen months occurred when the hearing had started and the court is of the view that abatement of proceedings is likely to result in denial of justice or abuse of court process."*

We are talking about the past, hizo kesi ambazo Mheshimiwa Shibuda amezeleza na nitumie nafasi hii kusema kwamba, Mheshimiwa Shibuda ndiye aliyetuamsha kwamba bwana kuna kesi na muda wake umekwisha. Kwa hiyo, *process* na hii kwamba tunazi-*cover* hizi kesi zingine na hizi kesi ambazo zinaendelea sasa hivi zitakuwa *covered* na miezi 18, lakini kama hazitakwisha wakati huo, Mahakama zenyewe zitatumia mamlaka haya kuzisikiliza mpaka zimalizike.

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba, kwa mujibu wa sheria na bila kuangalia kama hawa wanaohusika ambao watakutwa na kesi hii ni chama chako au ni wa chama cha ndugu yako mwingine, tuangalie tu haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni suala la haki na rafiki yangu Mheshimiwa Felix Mkosamali, amesoma sheria na anapenda sana haki. Juzi katika kesi yake moja, alikuja hapa akaniambia na mimi nikamwambia ni haki twende sawasawa, sasa ndiyo hii hapa tunafanya pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wa pande zote; wapo wa CCM wapo Madiwani

10 JUNI, 2013

wa CCM, wapo Madiwani wa CHADEMA, lakini CHADEMA najua wamo, nafikiri hata CUF wamo, kesi bado zinaendelea na kesi hizi haziendelei kwa sababu muda ulikuwa umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ndilo lengo hakuna hiyana, hakuna hila ni mambo ya wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba, nimeyaona mabadiliko hayo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na anachoeleza hakikubaliki moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosisitiza, mabadiliko haya yalitakiwa yaangalie pande zote, mshitaki na mshitakiwa, yaangalie kesi hizi zinazokuja mbele, kwa sababu wakati mwingine hata hii miezi 18 wengine tunaona ni mingi. Sasa unaposema tuongeze wengine hatukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachosema hata kama analeta mabadiliko kwamba tuiachie Mahakama i-*determine*, huwezi kuiachia Mahakama bila kuipangia muda wa kumaliza kesi. Sababu ya Bunge lako Tukufu kutunga sheria mara ya kwanza kuweka miezi 18 ilikuwa inataka mtu aliyechaguliwa, kuna wengine wanafungua kesi za uongo, wanabambikiza watu, afanye kazi yake bila kusumbuliwa. Pia yule ambaye amevunjiwa haki yake, apate haki yake ndani ya muda. Sasa hata ukiiachia Mahakama kwamba i-*determine* muda wa kuendelea na hizo kesi baada ya ule muda wake wa miezi 18 kwisha, hujatatua tatizo. Tatizo hapa na yeye mwenyewe amekiri wakati wanazungumza siyo kwamba ule muda wa miezi 18 ulikuwa hautoshi, tatizo ni fedha, siyo tatizo la kubadilisha sheria; ni kwamba Mahakama hazikuwa na fedha za kuweza kumaliza hizi kesi *on time*.

Kwa hiyo, hata tukibadilisha sheria ndiyo maana hata kuna kesi zingine zimekuwepo Mahakamani ambazo zinawahusu Wabunge, ambazo tulishapitisha Waziri wa Katiba na Sheria anaongeza miezi sita, ile miezi inapita na kesi hazijaisha kwa sababu ya rasilimali fedha. Ndiyo maana

10 JUNI, 2013

tunasema tatizo siyo kufanya haya mabadiliko na ndiyo maana ninasema tukatae haya mabadiliko, Serikali ilete mabadiliko yatakayokidhi, yatakayofanya hizi kesi zitazotokana na *by-election* ijayo ziishe ndani ya muda mfupi hata miezi 18 haitoshi. Pia ilete mabadiliko yanayoeleweka, ambayo yatatoa muda wa kutosha kwa kesi zilizoanza zamani kwisha ndani ya muda mfupi.

Kwa mabadiliko haya, hatutatatua tatizo lolote, Mahakama zitaongeza muda, kesi zitaenda mpaka mwaka 2015 mwezi wa Agosti na Sheria nimeeleza, inakataza *by-election* ndani ya miezi 12. Kwa hiyo, mabadiliko haya kwa kweli bado hayakidhi. Mimi ninaomba Serikali irudi ikajipange upya na msimamo wangu ni huo, sehemu hii ya nne ifutwe kwa sababu haikidhi, inakwenda kuleta matatizo huko Mahakamani.

MWENYEKITI: Mambo ya kisheria sasa tunasema hivi; wanaokubali mapendekezo yaliyoletwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali waseme ndiyo, wale wanaopinga watasema siyo. Sasa nitawahoji wanaokubali mapendekezo ya Mheshimiwa Felix Mkosamali yapite waseme ndiyo na wanaosema mapendekezo ya Mheshimiwa Felix Mkosamali yaspite waseme siyo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

MWENYEKITI: Tuanze na Mheshimiwa Felix Mkosamali, kama tutakubali ya Mheshimiwa Mkosamali ya Mheshimiwa Tundu Lissu yatakufa na ya Serikali yatakufa.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu cha nne hicho ni hayo hayo niliyokuwa

10 JUNI, 2013

nayazungumza. Sehemu ya nne yote ina kifungu cha tatu na cha nne. Naomba Mheshimiwa Tundu Lissu aendelee.

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. TUNDU
A. M. LISSU, MEMBER OF THE PARLIAMENT SINGIDA
MASHARIKI CONSTITUENCY, DURING THE SECOND
READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS
(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, 2013**

Made under S.O. 86(11)

The Bill entitled "The Written Law (Miscellaneous Amendment) Acts, 2013" is amended generally as follows:

- A: By deleting the full stop in clause 4 and adding immediately thereafter a semi-colon and the following words: "PROVIDED that the extension aforesaid shall not be made in any case where the last day of the extension shall fall within a period of twelve months preceding the following general election."
- B: The Principle Act is amended in Section 115(1)(a) by deleting the semicolon and adding the following new words "provided that his rights as a voter were violated by the results of the election to which the petition relates;"
- C: By deleting the entirety of Clause 8.

10 JUNI, 2013

D: In Clause 11 by deleting the entirety the proposed subsection (3).

Tundu A.M. Lissu (MP)
SINGIDA MASHARIKI CONSTITUENCY
10TH JUNE, 2013.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, niliandaa Jedwali la Marekebisho yangu kabla ya sijapata Jedwali la Marekebisho ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ninaona kwa kiasi kikubwa, kile nilichokuwa nataka kukibadilisha, kimebadilishwa na hizi *amendments* za Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa sijui nafanyaje; naomba maelekezo yako?

MWENYEKITI: Maana yake mnakubaliana. Tena kawaida hizi zilitakiwa ziletwe mkae pamoja. Jamani tunapofanya sheria, hatumkomoi mtu yeyote, ni ubora na mantiki ya kisheria ya kifungu kinachohusika. Kwa hiyo, kama hiki kifungu mnakubaliana na mapendekezo ya aliyeandika *amendment* za Serikali, basi mnafanya hivyo pale mnapokubaliana.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, ninakubaliana na *spirit* ya mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Isipokuwa kama utaniruhusu kwa sababu sina mapendekezo tena, kama utaniruhusu niyaseme tu kidogo, ila ninakubaliana na *spirit* ya mapendekezo.

MWENYEKITI: Sema tu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho anayopendekeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yanaipa Mahakama mamlaka ya kuamua kama baada ya miezi 18 iendelee na kesi na hilo ni jambo zuri kwa sababu moja; imetokea hasa hasa katika kesi zilizotokana

na Uchaguzi Mkuu uliopita kwamba, kesi za Uchaguzi zilianza kusikilizwa karibu mwaka mmoja baada ya kufunguliwa, kwa sababu fedha zilikuwa hazijatolewa kwa Mahakama kuendesha kesi hizo; na kwa hiyo, ukiweka msimamo mkali kwamba lazima ziishe ndani ya miezi 18, kuna uwezekano mkubwa kabisa kwamba, zitamalizika katika ngazi ya Mahakama ya Hakimu Mkazi halafu kwenye rufaa miezi 18 ikawa imepita, huyu aliyekuwa ameondolewa kwenye ngazi ya Mahakama ya Hakimu Mkazi akashindwa kupata rufaa kwa sababu muda uliowekwa na sheria umepita.

Kwa hiyo, mapendekezo haya yanaiwezesha Mahakama kuendelea na shauri kwa sababu kumnyima huyu anayepingana na uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi kukata rufaa, itakuwa ni kwenda kinyume kabisa na *spirit* ya sheria yenyewe na vilevile kwenda kinyume na Katiba ambayo inaruhusu mtu kupata nafuu kwa kukata rufaa.

Kwa hiyo, naunga mkono hii *spirit* ya mapendekezo ya mabadiliko yaliyoletwa na *Attorney General*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali, tunafuata kadiri walivyo-*submit amendments*.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu hiki ninapendekeza kifutwe kwa sababu sheria zingine kama nilivyoeleza wakati ninachangia zinaeleza jambo hili. Kwamba, nyaraka za Tume hii ya Kurekebisha Sheria zisichukuliwe bila ruhusa ya Tume, lakini hakijaweka vigezo gani na ni *documents* zipi ambazo haziwezi kuchukuliwa. Kwa mfano, mtu anaingia kwenye *website* ya Tume hii asichukue *document* yake. Pia nikaelize kwamba, kama kuna mtu ali-*forge document* yoyote ya Tume hii mmemchukulia hatua; je, Sheria za Jinai za nchi hii hazielezi makosa haya ya watu ku-*forge document* za Tume mpaka tuweke *specific*; kwa sababu nchi yoyote *intellectual property*, mtu aliyebuni kitu ni mali yake, siyo Tume peke yake na sheria zingine tayari zinaeleza? Ndiyo maana nasema hatuna haja ya kuwa na kifungu hiki.

MWENYEKITI: Hiyo *contention* na Mheshimiwa Tundu Lissu ipo hivyo, naye ali-*propose* kifutwe. Kwa hiyo, tukifuta ingawa ni tofauti lakini ni vyote mlipendekeza vifutwe; si hivyo ndivyo, Mheshimiwa Tundu Lissu?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimependekeza kifungu hiki kifutwe, lakini naomba niongezee tu sababu ya ziada ya kwa nini kifungu hiki hakifai kwa mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Tume ya Kurekebisha Sheria ni Chombo cha Umma, kinafanya kazi kwa kutumia fedha za umma. Matokeo ya kazi yake ni mali ya umma, ni mali yetu sisi. Sasa kifungu hiki mapendekezo haya ya mabadiliko ya sheria yanapendekeza kwamba, hawa wanaotumia mali zetu wakafanya kazi ambayo ni mali yetu, sisi ambao ni wenye mali, hatuwezi tukaitumia hiyo mali kwa ajili ya mambo mbalimbali bila kwanza kupata ridhaa yao, inakwenda kinyume kabisa na *spirit* ya *The Public Nature ya Law Reform Commission*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ni kwamba, Tume ya Kurekebisha Sheria inafanya kazi nyingi sana nzuri ambazo zinaweza zikawasaidia hata hawa Waheshimiwa

Wabunge humu ndani, kama wangekuwa wanajua, inafanya uchambuzi wa sheria nyingi sana na inafanya mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali. Matokeo ya uchambuzi wa Tume yanaweza kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge ambao wanaweza wakipenda, wakaleta Miswada Binafsi kwa ajili ya kurekebisha Sheria kwa kutumia uchambuzi na kazi iliyofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mapendekezo ya marekebisho haya, yanapendekeza kwamba, Mbunge anayetaka kutumia taarifa ya *Law Reform Commission* kuleta Muswada Binafsi hapa wa kurekebisha Sheria, hatafanya hivyo mpaka akaombe ridhaa ya Tume. Hawa watu siyo watu binafsi, hawatunii hela zao wanatumia hela za umma na kazi yao ya umma inatakiwa iwasaidie hata Waheshimiwa Wabunge kuleta Miswada iliyofanyiwa kazi na Tume ya Kurekebisha Sheria. Sasa kifungu hiki ni kinyume kabisa na haya matakwa muhimu ya umma.

Vilevile hivi kimetokea kitu gani juu ya haki ya kupata habari kama hatuwezi kupata habari za Tume mpaka wao watukubalie? Mapendekezo haya yanataka kutupeleka nyuma kabla haki za msingi za binadamu hazijawekwa katika Katiba. Ni mapendekezo yanayotrudisha nyuma zaidi ya miaka 30, ni kitu cha ajabu sana katika nchi inayotengeneza Katiba mpya, kupendekeza kitu cha aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niungane mkono na Mheshimiwa Mkosamali, kifungu hiki kifutwe. Tutakuwa kichekesho cha Kimataifa kwa kuruhusu kurudi nyuma miaka 30 kama inavyopendekezwa kwenye Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Sisi tulielezwa kabla hujafika, lakini naomba urudie kwa sababu ni *specific*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wawili waliozungumza

wote ni Wanasheria na kama ni Wanasheria, wanafahamu kwamba, ile haki ya msingi ya kupata habari za Tume ya Kurekebisha Sheria, imehifadhiwa kwenye kifungu cha 24 cha Sheria hiyo, imehifadhiwa kabisa. Mapendekezo haya yanasema; kwa mfano, kushughulikia Rasimu ya Tume, kabla Tume yenyewe haijafanya kuwa ni Ripoti ya Tume, mtu anachomoka nayo na tuna ushahidi hapa; kuna *issue* ya Mahakama za Kadhi, *issue* kuhusu adhabu ya kifo na mambo mengine.

Sasa Tume ilikaa, ikaona namna gani hizi taarifa zinatoka, tutafute njia gani tuingize kifungu. Mheshimiwa Mkosamali, huwezi kumshitaki mtu kabla huja-*create offence*. Tunachofanya hapa ni kukataza, hatutoi adhabu hapa kwa sababu itakwenda kwenye *penal code*.

Sasa mimi nilisoma sheria vizuri na nafikiri niliwafundisha vizuri kwamba, kama unataka kupata habari na mimi ni muumini wa uhuru wa habari, *by the way* naamini kabisa, lakini hizi habari zitolewe baada ya kazi hii kukamilika. Hatuzuii, tunachosema tupate idhini kwamba, je, pamoja na kwamba hii ni Rasimu haijatoka *into public eye*, haijawa *a public domain document*, ninaweza kuitumia. Ukiambiwa tumia utatumia, ukiambiwa usitumie usitumie. Sasa ikimalizika kwa mfano zile ripoti zilizokwenda kwa Waziri kwa mujibu wa kifungu cha 14 au kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali zikienda pale utaratibu wake kwamba zinaletwa Bungeni.

Kitu ambacho Waziri anakifanyia kazi apate uamuzi wa Serikali kwa vyombo vyote vya maamuzi ya Serikali wapate msimamo wa pamoja, wewe unaitumia ile; *that is a problem na in good governance that will be a problem*. Kama unataka kupata *public opinion*, nenda kwenye Tume waombe unaweza kutumia ile, wakikwambia *go ahead* basi utakuwa na ruhusa. Ndicho hicho tu tunachosema, hatusemi Watanzania wasipate habari za Tume; *no we can't say that* na mimi siwezi kuleta Muswada hapa kwa ajili ya kunyima watu habari, hapana. Ni matumizi na ndivyo nilivyosema nilipokuwa nawasilisha hoja yangu pale mezani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali ndiyo mwenye hoja!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna upungufu. Amejibu sawa, lakini sijakubaliana moja kwa moja kwa sababu nilieleza hata kuhusu *fair use* ya watu ambao wanafanya tafiti, inaruhusiwa, *fair use*, unaposema mpaka wakamilishe tutakuwa tunapimaje kwamba wamekamilisha kazi yao; nani atakuwa anatuambia kwamba kazi hiyo imekamillika?

Pili, ukiomba *document* usipopewa kwa sababu kifungu kinasema kutumia; hata kutumia nyaraka yoyote, vipeperushi, mpaka wao wakuruhusu, sasa usipopewa utafanya nini? Ndiyo maana tunasema kifungu hiki kitoke, Katiba imeshasema sasa hivi watu wana haki ya kupata habari hata kama kuna sheria zingine ambazo zinakiuka Katiba haziwezi kukubalika. Ndiyo maana hoja yangu iko palepale, kifungu hiki kiondoke, tunataka tuingie kwenye *website* yao tuone *documents* zao zitusaide kwenye mambo mengine.

MWENYEKITI: Nadhani ndivyo tunavyosema, *except* kama wao bado wanaifanyia kazi hawawezi kukuruhusu. Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa sababu una hoja ya namna hiyo!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Baada ya kumsikiliza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nafikiri tatizo ni la *drafting*, ni tatizo la namna alivyoleta mapendekezo yake. Kama lengo la mabadiliko haya ni kuzuia taarifa ambazo hazijakamilika, basi sheria ingesema hivyo, mapendekezo yake yangesema hivyo kwamba, taarifa zinazozungumzwa hapa ni zile *works in progress*, zile *notes* na *working papers* na za Tume ambazo hazijakubalika, *internal communication* za Tume, wangezi-*specify*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ilivyo ina-*cover* nyaraka na taarifa zote, *regardless of whether they are drafts, whether they are works in progress, whether they are internal memos,*

ina-cover kila kitu, ni mtego wa panya unakamata kila anayegusa. Sasa hii haiwezi ikawa sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili jambo ni muhimu sana, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama lengo ni hilo wa-specify hizo documents ambazo zinakuwa exempted ili kuondoa hii hatari ya kufunika kila kitu kuzuia watu wasipate taarifa muhimu za Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hizi taarifa tunazihitaji sana humu Bungeni. Tunahitaji kupata matokeo ya research za Tume ili tufanye kazi bora ya Ubunge humu ndani, tukizuiliwa in a blanket fashion namna hii, hata sisi humu ndani tutashindwa kufanya kazi na hii haiwezi ikawa spirit ya marekebisho ya sheria inayoletwa humu ndani na Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, hebu fafana tena maana naona mnabishana vitu ambavyo hata sisi ma-layman tumeelewa lakini ninyi hamwelewani.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo taarifa ambazo unataka uzitumie kwenye research utazipata kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria ya Law Reform Commission. It is not a problem here. Kama ni problem ya interpretation ndiyo a serious problem ya understanding of the law.

Tunachozungumza hapa ni kwamba, siyo tu zile internal communication, kuna zile nyingine ambazo zinakwenda kwa Waziri. Wao wameshamaliza kazi wanampelekea Waziri na Waziri anataka maamuzi ya Serikali. Sasa hizo nyingine ambazo unazungumzia kaka nenda kwenye kifungu cha 24. Kifungu cha 24 hatujakigusa. That is the best right under section 24.

Kwa sababu ni public record tayari na zile ambazo Mheshimiwa Waziri au Mwanasheria Mkuu akishaziwasilisha hapa mezani zipo kwenye public domain, huna haja ya kwenda kwenye Tume. Sasa mimi nashindwa kuelewa

10 JUNI, 2013

tunabishana kitu gani hapa na kama tumesoma sheria miaka mitatu au zaidi, nafikiri ni rahisi kujua kwamba *this is very easy*.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 9

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 10

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 11

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu yanafanya marekebisho kwenye mapendekezo ya Serikali. Pale ambapo kwenye kifungu kidogo cha tatu inapendekezwa kwamba, Katibu wa Tume asihudhurie Mikutano ya Tume kuhusu masuala ya nidhamu ya Watumishi wa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu yanasema kwamba, hicho kifungu kidogo kifutwe chote. Napendekeza hivyo kwa sababu kwa kuangalia mapendekezo ya Serikali na kuangalia sheria ilivyo, kuna *assumption* sijui *assumption* ni nini kwa Kiswahili! Kuna *assumption* kwamba, *referrals*, masuala ya kinidhamu ya wafanyakazi yatapelekwa kwenye Tume na huyu Mtendaji Mkuu wa Tume, Katibu, ndiyo *assumption behind the hii clause* inayosema asihudhurie hiyo Mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye sheria yenyewe huyu Katibu hajapewa mamlaka ya kupeleka hizo *disciplinary referral* kwenye Tume, hajapewa mamlaka na sheria kupeleka masuala ya nidhamu ya wafanyakazi kwenye Tume. Mapendekezo ya Serikali yana-*assume* kwamba,

atayapeleka na kwa sababu atakayapeleka, hawezi kushiriki kuyajadili kwa sababu kufanya hivyo itakuwa ni mshitaki na hakimu kwenye suala hilo hilo, kitu ambacho hakifai na nakubali.

Sheria ingekuwa inasema kwamba, hizo *referrals* kwenye Tume juu ya nidhamu ya wafanyakazi zitapelekwa na Katibu, basi haya mapendekezo ya Serikali yangukuwa sahihi kabisa. Kwa vile kwenye sheria yenyewe mimi sijaona mahali ambapo Katibu anapeleka *disciplinary matters* za wafanyakazi wa chini yake kwenye Tume, hii ya kumkataza kushiriki kwenye kujadili masuala ya kinidhamu ya wafanyakazi wa chini yake haiwezi ikawa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwa mujibu wa sheria hii na kwa mujibu wa mapendekezo yaliyoletwa, huyu Katibu wa Tume ndiyo *Chief Executive Officer* wa Tume, ndiye Mkuu wa Watumishi na Watendaji wa Tume wote. Sasa ni *CEO* wa aina gani ambaye hawezi kushiriki katika *decision making* ya masuala ya kinidhamu ya wafanyakazi ambao wako chini yake?

Kwa hiyo nimependekeza kwamba, hiyo *sub-clause (3)* ifutwe kabisa; vinginevyo, Serikali ituambie kama hizi *disciplinary matters, disciplinary referrals*, zitapelekwa kwenye Tume na Katibu mwenyewe, *in which case* itakuwa sahihi kuweka marekebisha hayo. Kama hakuna kifungu kinachompa mamlaka hayo *excessively*, ni vizuri akashiriki katika kufanya maamuzi juu ya masuala ya kinidhamu ya wafanyakazi wa chini yake. Ni hiyo tu Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa sheria unapoanza kuzungumzia haki za wafanyakazi, msingi wa kwanza kabisa ni haki kutendeka na siyo haki kutendeka tu, haki kuonekana inatendeka; *whether*, hayo mashitaka yamepelekwa na Katibu au na mtu mwingine. Kwa sababu gani? Huyu ni mfanyakazi ambaye yuko chini ya Katibu na mwenendo wa tabia yake au mashitaka yake hayawezi kwenda mbele bila ya mkono wa

Katibu. Kwa hiyo, hata Katibu kukaa pale hata kama hakuhusika kufanya maamuzi yale, kukaa tu utasema kwamba, Katibu ana-*influence* lile jopo linalosikiliza haki ya yule mtu na wewe unajua kuliko wengine hapa kwamba, *principles za natural justice* hiyo ni ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yetu ni kwamba, Katibu asikae kwenye Tume kama jambo linalohusika linatoka kwa watumishi ambao wako chini yake.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nafikiri tatizo hapa kama unasema kwamba, masuala haya lazima yapite kwenye mkono wa Katibu ndiyo yafike kwenye Tume, lazima kuwe na msingi wa kisheria wa kukuwezesha kusema hivyo. Lazima sheria iwe inasema kwamba, masuala ya nidhamu ya wafanyakazi yatapelekwa kwenye Tume na Katibu, lakini Sheria ya Tume haisemi hivyo. Sasa kama haisemi hivyo, unasemaje kwamba, yataenda kwenye Tume kwa kupitia kwa Katibu, *it cannot be assumed*; tunapojadili masuala ya haki na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anafahamu, kwenye masuala yanayohusu haki, kwenye masuala yanayohusu fedha, kwenye masuala yanayohusu *property rights*, sheria inakuwa inatafsiriwa *strictly*.

Sasa kama sheria haijasema kwamba, hizi *disciplinary referrals* zitapelekwa na Katibu wa Tume kwenye Tume, ukimzuia asiende kusikiliza matatizo ya rufaa za wafanyakazi wake, anakuwa ni *CEO* wa aina gani? Kama sheria ingekuwa inasema kwamba, ni yeye ndiyo anazipeleka wala nisingejaribu kuleta mapendekezo haya, lakini sheria haijasema hivyo. Sasa kama sheria haijasema hivyo; unamzuiaje Mtendaji Mkuu wa Taasisi kwenda kusikiliza mashauri yanayohusu wafanyakazi wake? Inawezekana akawa siyo lazima aende kule kuwashtaki tu, inawezekana uwepo wake ukasaidia kuwatetea vilevile. Kuna hiyo *assumption* kwamba, wakienda kule wanaenda kubanwa tu, siyo lazima, anaweza akaenda akawatetea vilevile akasema, huyu mfanyakazi wangu namfahamu ni mtendaji mzuri haya ni majungu.

Sasa ukimzuia bila sababu ya msingi, kwa kweli itakuwa siyo sawasawa, hawezi akawa *CEO* halafu mkamwita mkasema kwamba kwenye masuala ya nidhamu ya wafanyakazi hutakuwepo, haiwezekani. *I understand na I agree entirely* kwamba, haki lazima ifanyike na lazima ionekane ikifanyika. Haki itaonekana imefanyika kama *CEO* huyu hataenda kwenye masuala haya ya kinidhamu kwa sababu ndiye aliyeyapeleka kwenye Tume, hapo nitakubali na sitabisha; lakini kama hajayapeleka, kama *he is not involved* na sheria haijasema atayapeleka, unamzuiaje halafu *at the same time* unamwita *CEO*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo ya kwangu.

MWENYEKITI: *In your case*, kama siyo *CEO* aliyepeleka nani mwingine anapeleka? Kama siyo *CEO* aliyepeleka ambaye ni *Secretary General* nani mwingine anaweza kupeleka mashitaka?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi mwingine yeyote, inawezekana na Tume ikayachukua yenyewe *suo moto*. Tume hizi zina mamlaka ya kufanya maamuzi kufuatana na zinavyoona inafaa, wanaweza wakaianzisha *suo moto*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Umma ni mahali ambapo watumishi wanakata rufaa pale ambapo mamlaka zao za nidhamu hazikuwatendea haki. Sasa Katibu anaruhusiwa kuhudhuria vikao vyote, isipokuwa na yeye pale kwenye Tume yake anao watumishi wake. Sasa wale watumishi wake ambao yeye kama mamlaka ya ajira atawachukulia hatua, wanapokata rufaa, ndipo pale ambapo yeye sasa haruhusiwi kuingia katika kikao kile cha watumishi ambao wamemkatia rufaa yeye; ndiyo sheria inavyosema na ndicho anachokipendekeza. Hayo ndiyo marekebisho yanayopendekezwa.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa *very brief*. Kama hivyo ndiyo wangesema. Tatizo

la upande wa Serikali ni kwamba, wana hoja nzuri tu, lakini hawaisemi kwenye maandiko yao. Sasa kama unakaa nazo kichwani mwako tutajuwaje kama una hoja nzuri namna hii? Kama suala ni kwamba, haya masuala ni masuala ya nidhamu, ni rufaa za wafanyakazi dhidi ya maamuzi ya Katibu, *they should have said so*. Wakinyamaza wanataka tujuweje yaliyomo kwenye vichwa vyao? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Ngoja kwanza hapa. Nilivyofanya siyo sahihi, kwa sababu hoja hii ilikuwa ni ya Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa hiyo, hatuwezi kusema kinaafikiwa kama kilivyo kwa sababu inaelekea wameelewana na hizi *Miscellaneous Amendments* huwa haichukui sheria kubwa ni kishemu kile tu. Kwa hiyo, kifungu hiki kinaafikiwa?

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 12

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 13

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali, marekebisho kwenye marekebisho ya kifungu cha Serikali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi marekebisho yangu ni kwamba, nimemsikiliza Mwanasheria Mkuu akiwa anazungumza, mimi sizungumzii *sub-delegation*. Sizungumzi kwamba, Sekretarieti iki-*delegate* kwa hawa Wakurugenzi, sijui Makatibu wa nini, nao wafanye *delegation* sehemu nyingine. Kwa hiyo, anaposema *delegatus non potest delegare*, mimi sizungumzi hivyo, nazungumza ulazima kwamba, iwe ni lazima, huu mchakato wa ajira, kufanya usaili, kufanya nini, tuhamishe moja kwa moja, kwa sababu kumekuwa na malalamiko makubwa kuhusu mchakato wa ajira, usaili na kadhalika.

Sasa ninachosema ni kitu gani? Ninachosema ni kwamba, isiwe ni “*may*”, eti huyu huyu *Secretary* akijisikia tu ndiyo ana- *delegate* hizi *power* kwa Wakurugenzi wa Halmashauri na nini, kufanya hizi shughuli za kuwasaili hawa Wakurugenzi. Ninachosema ni kwamba, iwe ni lazima *recruitment process* ya ajira hizi ndogo ndogo ifanywe huko, iwe ni lazima, siyo akijisikia yeye, kiwe ni kifungu kinamlazimisha kufanya hivyo.

Tukiacha kama hivi ilivyo kwamba ni yeye atakapojisikia, tunaweza tukakaa hapa tukapitisha sheria na asi-*publish* na tutakuwa hatuna cha kufanya. Hata kwenye Kamati nilisema, kama hawataki hivi, wangetuletea kifungu kingine cha kuongeza hapa chini, cha kusema kama akikataa ku-*delegate* awe anatoa sababu kwa nini anakataa Halmashauri na Manispaa na watu hao wengine, *Chief Executive Officers*, wasifanye huo mchakato wa usaili wa ajira na vitu vingine, kuliko kumwachia mtu awe anafanya anavyojisikia, tunataka iwe *mandatory*, iwe ni lazima ku-*delegate*. Sizungumzii *sub-delegation*, nasema iwe ni *mandatory* ku-*delegate* ili akikataa, tumchukulie hatua.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo rahisi kwelikweli na sijui kwa nini inachukua muda mrefu kueleweka! Mamlaka ya Tume ya Ajira ni mamlaka asili na kinachofanyika kwenye kifungu hicho kinachopendekezwa ni kukasimisha madaraka, siyo kuhamisha. (*Makofi*)

Mimi naomba tu Wanasheria, maneno haya tumefundishwa kusomea maneno, kinachozungumzwa hapa ni kukasimisha, siyo kuhamisha na *he who pays the piper chooses the music*.

Nenda kwenye lile dude la kutumbukiza fedha pale, halisemi mpaka umeweka fedha, anayelipa ni Serikali, yaani hizo kazi unazosisema, mlipaji mkuu ni Serikali. Sasa lazima Serikali iwe na mchujo kwamba, hizi fedha ninazopeleka hapa zinakwenda huko na *control* ya ajira ina uwezo wa

kulipa *sustainably*; *that is the meaning* na tunasema kwamba, ukisema sasa "*shall*", umeshahamisha, hujakasimisha. (Makofi)

Msingi wa sheria, kifungu cha 29 kilichotungwa 2007, ilikuwa ni ku-*control* ajira za ovyo ovyo, ajira za undugu. Sasa sidhani kama hiyo tabia ya kuajiri ndugu imeshakwisha, kwa hiyo, ndiyo maana tunabaki kwamba unakasimisha lakini macho yako lazima yawe makubwa. Uwe mrefu kama Mlima Kilimanjaro na mfupi kama sisimizi, huwezi kuwaona hawa watu wanaofanya haya mambo na ndiyo maana tunasema kwamba, mamlaka hayo lazima yakasimiwe kwa njia hiyo. Hii ni *Principle* ya *Administrative Law*, itachukua muda mrefu kuelimisha juu ya *Administrative Law. Functions* ambazo mtu ana-*delegate* akiwa anabaki, hahamishi mamlaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kifungu hiki kilivyowekwa na Serikali, ndivyo hasa kinavyotakiwa kuwa na pengine useme kwamba, haya mambo atayafanya kwa muda gani; majibu tunayo kwamba, itakuwa ni *from time to time* kusudi aweze kufanya tathmini. Sasa ukisema *shall* ni kwamba, umeshaachia limekuwa shamba la bibi tena; huko ndiko tulikokuwa tumetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu *sensitivity* ya ajira kwenye Halmashauri na nililionga kwenye Kamati, nimelisikia leo asubuhi na mitaani pia nasikia. Mimi pia si ninakaa kwenye Halmashauri, lakini hatuwezi kuachia hiyo, hivi inavyopendekezwa tutakuwa tunarudi tena kule *pre-2007*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na sauti nzuri anayotumia Mheshimiwa Felix Mkosamali, kwenye hili, naomba twende na pendekezo ambalo Serikali imetoa kwenye hili jambo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali, ndiye mwenye hoja!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumza, nazungumza hicho hicho tu kwamba, ni lazima akasimisha, yaani iwe ni *mandatory* kukasimisha.

10 JUNI, 2013

Sizungumzii kwamba ahamishe, nataka iwe lazima na hapa ambacho ninakisema amekijibu hata Mheshimiwa Hawa Ghasia hapa, wanaotoa vibali vya ajira siyo Sekretarieti, watu wanaomba kwa Makatibu Wakuu huko ndiyo wanatoa vibali vya ajira na ndiyo wanao-*control* kwamba, tuwe na madereva wangapi Njombe, tuwe na madereva wangapi Kigoma, siyo hawa!

Tunachotaka Sekretarieti ni ule mchakato wa ajira, iwe ni lazima kufanyika huko na wakati nachangia hapa nikasema, Sekretarieti haiwezi kuwa na wataalam wa kila namna wa kufanya usaili kwenye kila kitu, ndiyo maana tukasema iwe ni lazima. Kama jambo ni la Wizara ya Nishati na Madini, ni lazima a-*delegate* na usaili ufanyike huko, wao wabaki wana-*control* tu vitu vichache. Sasa haya anayosema kwamba ananifundisha, mimi nimepata "A" ya *Constitutional Law*, "A" ya 89, kwa hiyo, niko vizuri tu.

Sasa, hakuna mtu wa kunipima, ukishapimwa kule unakuwa uko vizuri na *Administrative Law* nikapata "B+". Kwa hiyo, ninafahamu vizuri huu utaratibu. Ninachokisema ndiyo hicho; kumekuwa na kilio, Wakurugenzi wanaomba wafanye usaili. Sasa kama haya mapendekezo yanakuja, tunataka tuweke iwe ni lazima usaili ufanyikie kule, siyo yeye akiamua kwa *leisure* yake, itakuwa ni usumbufu kama ambao unaendelea sasa hivi.

Mnatuma kuomba vibali kwa Makatibu Wakuu huko, wanachelewesha kutoa vibali vya ajira, mje hapa msubiri naye huyu atakapojisikia kuwaruhusu kufanya mchakato wa usaili. Sasa hili kwa nini tusimwambie kwamba ni lazima ukasimishe madaraka, siyo akasimishe kwa *leisure* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndicho ninachokisema.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, kwa *clarification*.

10 JUNI, 2013

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, Mheshimiwa Mkosamali anachanganya vitu viwili; suala la vibali vya ajira na huo mchakato ni vitu viwili tofauti. Lakini kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba, kinachofanyika ni kukasimu, sasa wewe ukiwa na madaraka, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anayo ridhaa ya kukasimisha madaraka yake baadhi na unapokasimisha hukasimishi kila kitu, sasa una hiari. Tunavyopitisha hapa ina maana hizo kada tayari zimeshaainishwa, tukishakubaliana hapa ni kwenda kuweka katika Gazeti la Serikali, ina maana huo mchakato umeisha, kuanzia hapo Halmashauri zitaanza kuajiri zile nafasi tulizoziainisha. Haina maana kwamba kila mwaka Halmashauri zitakuwa zinakwenda kuomba, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiridhia hapa kwamba, Halmashauri ziajiri, zile nafasi ziko karibu 17, Makatibu Wakuu waajiri; tukikubaliana hapa, kinachofuata hapa ni Gazeti la Serikali kutoa na usaili unaendelea. Siyo kwamba Halmashauri zitakuwa zinaenda kupiga hodi kila mara. Mimi nadhani Mheshimiwa Mkosamali, ajifunze kuelewa pale anapoelewesha.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

(Bunge lilirudia)

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali
wa Mwaka 2013 *(The Written Laws (Miscellaneous
Amendment Bill, 2013)***

(Kusomwa Mara ya Tatu)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa taarifa, naomba kuwashukuru Wabunge wote, hasa marafiki zangu; Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Felix Mkosamali, kwa changamoto walizoleta.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa

10 JUNI, 2013

mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2013 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment Act, 2013)*), Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2013 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment Act, 2013)*), kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Katibu.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Bungeni
Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Muswada huu umepitishwa, bado kwenda kuwekewa saini na Mheshimiwa Rais. Napenda kutoa angalizo moja; hii siyo sawasawa na jinsi tulivyokuwa tunapitisha mafungu ya bajeti. Tunapokuja kwenye *amendment* ya Muswada wowote ule, ile *networking* jamani ni muhimu, kwa sababu tunachotunga hapa siyo Muswada wa CHADEMA, wala wa CCM au wa NCCR-Mageuzi, ni Muswada wa nchi. Sasa kinachotokea hapa, baada ya ile Kamati inayohusika na Muswada na ambayo yenyewe kidogo inashirikisha, lakini *amendment* zinazoletwa na *individual* hazishirikishi.

Kwa sababu wengine wote hata mngetamani kujadili mngekuwa mnasema kama alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini kwamba ninyi mliriki na mkapata *argument* nje

ya humu ndani siyo kweli, kitu ambacho siyo sahihi. Miswada ni kutunga Sheria ya nchi ya leo na ya miaka inayokuja. Naomba msiwe *selfish* kabisa, maana mtu anatunga ka-*amendment* kake peke yake halafu anakaa nako anakaleta humu ndani. Sasa hivyo sivyo, shirikisheni hata hawa mnaowaletea *amendment* wapelekeeni na waambieni kwamba, mimi naleta *amendment*, *argument* ni hizi. Mtabishana kule mtakuta hamkukubaliana basi unaleta humu ndani. Ndivyo inavyokuwa na naomba msianze kufanya siasa kwenye Sheria, Sheria ni Sheria ya nchi, shirikisheni. Hata ukiitisha watu, ama mkarudisha kwenye Kamati yenyewe, bado utakuwa na *ownership* ya wewe mwenyewe kuwasilisha, utakuta na wenzio wanachangia kwa mantiki, siyo tu kwa sababu ameleta Mheshimiwa Tundu Lissu, lazima tuunge mkono au lazima tupinge; sivyo. Kama kuna msingi kwamba, amesemea kitu kinachokubalika, lazima tukubali kwamba hii ni hoja. Kwa hiyo, hii ndiyo *weakness* tuliyonayo katika *amendments* za Miswada hasa, haya mengine ni hesabu tu lakini hii ni Sheria. Kwa hiyo, nategemea tutajifunza kwa muda uliobaki huu kufanya kazi kwa kushirikiana na ni *networking* katika Bunge, ni muhimu sana hasa mambo ya kutunga Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kesho tutakuwa na maswali kipindi cha asubuhi na mara baada ya kipindi cha maswali kutakuwa na Semina ya kuwaelezeni Awamu ya Tatu ya Mpango wa *TASAF*, kwa sababu wengine tunasikia tu. Kwa hiyo, kesho itafanyika hiyo kwenye Ukumbi wa Msekwa, mara baada ya kipindi cha Maswali tutaahirisha Bunge tutakwenda kwenye Ukumbi wa Msekwa. Semina hiyo ni muhimu Waheshimiwa Wabunge pia kushiriki, kwa sababu inagusa sana Wananchi ambao tunawawakilisha. Kwa hiyo, ni vizuri mkafahamu halafu mtaweza kushiriki vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, mimi sina tangazo lingine, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.15 Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 11 Juni, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*